ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
41.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
42.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
43.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
46.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
50.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
52.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
54.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
57. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
61.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 14 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Mohammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2011/2012. Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MJIBU
Nam. 229

Mgongano wa Kiutendaji Kati ya Mamlaka ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza**:-**
Kumekuwa na madai ya migongano inayotokana na kukosekna mipaka ya kiutendaji kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa.

(a) Mhe. Waziri serikali inaliangaliaje suala hilo.

(b) Je, ni ipi mipaka ya kiutendaji kati ya taasisi hizo mbili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 229 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba hapo nyuma mpaka mwishoni mw amwaka 2010 kulikuwa na madai ya migongano yanayotokana na kukosekana kwa kufahamika mipaka ya kiutendaji kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa hususan katika maeneo ya matumizi ya sheria kwa taasisi zote mbili.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, serikali iliona suala hilo na kutumia busara za kiutendaji ambapo imefanikisha kuondoa suala hilo. Ingawaje sheria hazijafanyiwa marekebisho hivi sasa tumo njiani katika mkakati huo. Mipaka ya kiutendaji inayodaiwa katika suala hilo ni katika maeneo ya wazi ndani ya Baraza la Manispaa na Mji Mkongwe, ambapo kisheria taasisi zote zinahusika.

Mhe. Mwenyekiti, katika maeneo ya utoaji wa vibali vya ujenzi mpya na matengenezo katika mipaka ya Baraza la Manispaa na Mamlaka ya Hifadhi na Uendeshaji wa Mji Mkongwe hasa eneo la *buffer zone*, vibali ambavyo ni vianzio vya mapato kwa taasisi zote mbili na maeneo ambayo kulikuwa na migongano. Kitaifa Mji Mkongwe unatunza hifadhi ya uasili wa miji mikongwe ambapo Zanzibar ni pekee kwa Afrika iliyopata hadhi hii ya kimataifa kwa uhifadhi wa miji ya kihistoria duniani.

Aidha, kitaifa Baraza la Manispaa lina jukumu kubwa la utunzaji na utoaji wa huduma zote za usafi kwa jamii na mazingira yao yanayowazunguka, ambapo Baraza la Manispaa hulipia ada zote za urithi wa Mji Mkongwe huko Quebec, Canada na gharama inayochangiwa kwa mapato yanayotokana na na vianzio vya huduma ziliomo katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria Nam. 4 ya mwaka 2010, Sheria ya Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe imeelezea mipaka ya Mji Mkongwe kiutendaji, ambayo inajumuisha eneo lote la Mji Mkongwe kwa upande wa Magharibi na kwa upande wa Mashariki Mji Mkongwe mipaka yake inaishia mita 50 kutoka barabara ya *creek road* na inajumuisha barabara ya Mchangani hadi Mlandege, kutokana na haiba au mazingira yanayofanyana na Mji Mkongwe.

Kwa upande wa Barazala Manispaa mipaka yake ya kiutendaji ni eneo lote la Wilaya ya Mjini ukiondoa eneo la mipaka ya kiutendaji la Mji Mkongwe ambayo imeainishwa hapo awali. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri nina swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri amekiri kwamba kumekuwepo na migongano kati ya Manispaa na Baraza la Mji Mkongwe, na amesema hadi sasa marekebisho ya sheria hayajafanyika, ila ni busara za

wizara na serikali kwa ujumla ambazo zimesawazidha migongano hii ya kisheria. Naomba kujua ni busara zipi za serikali ambazo zinatumika ili kusawazisha migongano ya kisheria hadi leo wakafanya kazi wakaelewana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyokubali na kama alivyoongezea Mhe. Hija, kwamba kulikuwa na migongano na hasa ya kiutendaji, kila mmoja akijiona yuko *right* kwa mujibu wa sheria kwa upande wake. Sasa sisi kama wizara tulichukua jukumu tukakaa na wenzetu wa Hifadhi ya Mji Mkongwe kupitia kwenye wizara, tukaona matatizo yako wapi na tukaamua kwa pamoja sasa tukae chini tuvipitie vipengele vyote vya sheria. Kwa hivyo, tumeunda kamati ndogo ya kitendaji inaifanya kazi hiyo, inaendelea hiyo kazi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi la Mhe. Jaku Ayoub, alieleza kwamba mpaka wa Mji Mkongwe ni mita 50 kutoka barabara ya *creek road*. Lakini pia alieleza kwamba maeneo ya Mchangani na Mbuyuni nayo yameingizwa kulingana na mazingira yake. Je, Mhe. Waziri huoni sheria kutamka mita 50 kutoka *creek road* lakini baadae kuyaingiza baadhi ya maeneo ambayo yamezidi zaidi ya mita 50 ni kuleta migongano ya kisheria kwa makusudi.

Lakini pili, sheria Nam. 3 ya mwaka 1995 ambayo imeanzisha Baraza la Manispaa la Zanzibar limeeleza kwamba, mipaka ya Baraza la Manispaa litaoneshwa kwatika *schedule* ya sheria hiyo, lakini *schedule* hiyo katika sheria hiyo haipo. Ni kwa nini haipo *schedule* hiyo ambayo inaonesha mipaka ya Manispaa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba nielezee tena ile mipaka. Baraza la Manispaa mpaka wake ni Wilaya yote ya Mjini, sasa Mji Mkongwe unachukuliwa Mji Mkongwe mpaka eneo hili ambalo tunaliita *creek road,* kuanzia *Malindi Police Station* mpaka kona ya Makumbusho.

Sasa kuanzia hapo mpaka eneo la barabara ya Mitumba, Mlandege mpaka Gofu ile ni *Buffer Zone* imewekwa, kwa kizungu nisaidie kutafsiri hili neno *Buffer,* yaani kama eneo la akiba kama kutenganisha, kama kutatokea huyu amezidi kidogo basi ataruhusiwa kwa kazi zake, hiyo ndio *buffer zone*. Sasa hapo mnaweza mkaelewana, mkagombana, lakini hiyo ndio *buffer* tena huzidi huko upande wa pili.

Kwa hivyo, kweli migongano imetokezea lakini hiyo ramani kama nilivyosema kwa sasa nafikiri iko haja ya kuipitia upya kwa sababu Wilaya ya Mjini tunaijua, lakini ukweli shughuli za Manispaa zimezidi.

Sasa hivi Kiembesamaki mpaka Magogoni huko imekuwa Wilaya ya Magharibi, lakini shughuli zake utakuta nyengine nyingi kama za Mjini za Baraza la Manispaa. Kwa hivyo, nakubaliana na wewe iko haja ya kuangaliwa upywa tuitizame halafu tushauri tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anatwambia *creek road* kutoka pale Baraza la Manispaa upime mita 50 kuelekea Mchangani na njia ya Mchangani kwenye maduka kutoka huku mita 50 na huku mita 50 ndivyo nilivyokuelewa Mhe. Waziri? Na eneo lililobaki itakuwa si dhamana ya Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, unajua Mhe. Jaku anazungumza haraka haraka, sikumpata vizuri naomba arudie tena swali lake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kutoka Manispaa barabara kubwa mpaka Mnazi Mmoja eneo lile ndilo lililogawa Mji Mkongwe mita 50 na zaidi ya mita 50 itakuwa si dhamana ya Mji Mkongwe.

Pili barabara ya Mchangani kuna barabara kubwa ile imegawa huku na huku kutoka kwenye milango ya duka mpaka mita 50 kulikobaki sio eneo la Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba eneo la Mji Mkongwe mipaka yake kwa sasa kuanzia *Malindi Police Station* mpaka Makumbusho, kule mbele baadae nilisema ni *buffer zone*. Sasa kweli wanaweza kutumia mita 50 kwenda na kurudi *plus* au *minus*, lakini ile ndio *buffer zone*. Naomba labda baadae tukae kidogo tufahamishane kitaalamu kuna *mape reading*.

Nam. 143
Skuli ya Sekondari ya Tumbe Kukosa Walimu wa Sayansi wenye Sifa

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza:-

Skuli ya Sekondari ya Tumbe imeanzisha madarasa ya Sayansi *Form III – Form IV* lakini haina Mwalimu hata mmoja mwenye sifa ya kufundisha madarasa hayo.

(a) Je, wizara yako imeandaa utaratibu gani ili kuondoa tatizo la kufeli kwa wanafunzi wa sayansi mwaka hadi mwaka jambo ambalo linachangiwa kwa kiwango kikubwa cha kutokuwepo kwa walimu wenye sifa.

(b) Je, wizara husika inatoa motisha gani kwa walimu wa sayansi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu katika utoaji wa taaluma katika masomo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.143 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Skuli ya Sekondari ya Tumbe ina madarasa ya Kidato cha Tatu na cha Nne yanayofundisha masomo ya Sayansi. Pia ni kweli kuwa skuli hiyo ina uchache wa walimu wenye sifa za kufundisha masomo ya Sayansi. Sifa za walimu waliopo hazitoshelezi kufundisha madarasa ya Kidato cha Tatu na cha Nne. Hata hivyo, katika hali ya uchache wa walimu wenye sifa, skuli ina walimu wawili wenye Stashahada ya ualimu wa msingi masomo ya Biolojia na Kemia. Pia ina walimu wawili wa sayansi wenye elimu ya Kidato cha Sita wanaofundisha Skuli ya Tumbe na Kinowe kwa utaratibu wa *part time*. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, wizara imeimarisha mafunzo ya Stashahada na Shahada ya walimu wa masomo ya sayansi. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinatoa kozi za Shahada na Stashahada za walimu wa Sayansi kwa ajili ya kuongeza idadi ya walimu wa sayansi katika skuli zetu za serikali.

   Pia hivi karibuni, wizara imetangaza nafasi za walimu wa masomo ya Stashahada ya ualimu kwa vijana waliomaliza Kidato cha Sita katika chuo cha Kiislamu, Unguja na Chuo cha Ualimu cha Benjamin W. Mkapa huko Pemba. Mafunzo hayo ya miaka miwili yatasaidia katika kuongeza idadi ya walimu wenye sifa za kufundisha masomo ya sayansi katika skuli zetu. Wizara pia inaandaa mafunzo ya ualimu kazini kwa walimu wa sayansi kupitia vituo vya walimu. Mafunzo hayo ambayo ni ya muda wa miezi sita inakusudia kutoa mafunzo kwa walimu wa sayansi 500 na hadi sasa walimu zaidi ya 300 wamepata mafunzo hayo.

b) Wizara kwa sasa haina utaratibu wa kuwapa motisha maalumu wanaofundisha masomo ya sayansi katika mazingira magumu. Hata hivyo, wazo hili si baya tunalipokea na tutalifanyia kazi.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kama alivyosema kwamba skuli nzima ina walimu wawili na walimu hao wanakwenda huku na kule. Kwa kuwa tatizo hilo bado lipo linaendelea katika skuli hiyo. Je. Wizara haioni kwamba huko ni kuzidumanza akili za vijana wetu.

Pili, kwa kuwa walimu wachache tulionao wanaotoa mafunzo ya sayansi kwa kukosa motisha je, huoni kwamba ni njia moja wapo inayowafanya kuhama kutokufundisha hapa nchini na kwenda nchi nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli na nilikiri mwanzo kwenye suala langu mama kwamba tuna matatizo ya walimu, ingelikuwa walimu waliopo wanatosha basi nisingesema kama matatizo hayo tunayo. Nimeelezea ni namna gani ambavyo tunatarajia baada ya muda si mrefu matatizo hayo yatamalizika. Mhe. Mwakilishi ninakuomba na wawakilishi wengine walioko katika Baraza hili, pia tujitahidi kuzungumza na vijana wetu ambao wanatoka Chuo Kikuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano juzi tu tuna tatizo la watoto wetu serikali inawasomesha kwa gharama zote, lakini wanaporudi Chuo Kikuu kusoma hawataki tena kurudi katika majimbo yao kuwasaidia wenzao. Juzi kijana wa jimbo lake Mhe. Rufai katoka chuo tumempangia kwenda kusomesha Skuli ya Tumbe kakataa katakata, anataka asomeshe Hamamni na sisi tukamwambia madhali unakataa kusaidia ndugu zako basi sisi hatukuajiri akakubali kuwa tusimuajiri aende *private*, lakini alikataa moja kwa moja kwenda kusaidia ndugu zake.

Sasa waheshimiwa Wawakilishi naomba hili mtusaidie, watoto wetu na ndugu zetu ambao wanatoka katika majimbo yetu tunapowasomesha kwa gharaba basi warudi kuwasaidia watoto wetu. Mhe. Rufai nikuahidi kuwa tatizo hili litatuka hivi karibuni iwapo na nyinyi wawakilishi mtatoa msukumo huo. Kuna skuli ya kisasa ambayo tunakujengea ya sekondari pale na ina nyumba za walimu. Kwa hivyo, nyumba hizo basi zitumike kwa kukaa walimu na kutusomeshea watoto wetu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri yenye hamasa ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Kwa kuwa kakiri kwamba upungufu wa walimu upo wa sayansi na motisha ni ndogo. Mbona amelishikilia suala la karibu kwamba patatuka ana miujiza gani aliyoipanga ili hilo suala litatuke.

(b) Hizo skuli ambazo zimejengwa mpya walimu wake ni wepi, watatoka Ulaya, India au wanasomeshwa huko nje ili waje wasomeshwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nimesema katika jibu langu mama kama suala la motisha si wazo baya. Kwa hivyo, wizara tunalichukua na tutalifanyia kazi, nilisema hilo kabla.

Lakini suala la hizi skuli mpya Mhe. Mwenyekiti, hata juzi nilipojibu swali nilisema kwamba, tuna mpango wa kuajiri walimu 800 katika bajeti yetu hii ambayo leo nimeomba kuwasilisha mezani kwa niaba ya waziri, kama tutaajiri walimu hao na walimu 500 katika hao ni wa masomo ya sayansi.

Kwa hivyo, naamini baada ya kupitisha bajeti yetu hii basi tatizo hilo litapungua kwa kiasi kikubwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kama alivyosema katika swali lake mama kwamba, watoto wanaokwenda kusoma kurudi majumbani mwao au katika sheria zao na maskulini mwao hawarudi kusomesha. Je, haoni kutokana na kiwango kidogo cha mishahara ambacho hakilingani na elimu zao ndio sababu ambayo inawafanya wasirudi kusomesha katika skuli zao

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, suala la mishahara kuwa ni mshahara mdogo ambao unatolewa si suala la Wizara ya Elimu tu Mheshimiwa, ni suala ambalo ni wizara zote tunakabiliana nalo.

Mhe. Waziri wa Fedha wakati wa bajeti yake alituahidi kama kuna asilimia 25 ya mishahara ya wafanyakazi wetu mbali ya wataalamu. Kwa hivyo, naamini baada ya nyongeza hii kama kweli mtu ni mzalendo na anajali uzalendo wake, uzanzibari na anajali kama nchi hii ndio ambayo imemsomesha basi hiki ambacho atakipata atakipokea na atatusaidia katika kujenga nchi yetu.

Nam. 131

Upandishaji wa Bei za Mafuta Kiholela

Mhe. Fatma Mbarouk Said - Aliuliza:-
Kumekuwa na tatizo linalojitokeza mara kwa mara la wamiliki wa Sheli za Mafuta kuzuwia kuuza mafuta kwa muda fulani na wanaporejesha huduma hiyo wanapandisha bei huku Wizara husika ikiwa imekaa kimya.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako huchukua hatua gani linapotokezea suala hilo.

(b) Wizara ina waahidi nini wananchi katika kukomesha kitendo hiki kiovu ambacho hupelekea ulanguzi, kupanda nauli za gari na kadhalika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 131 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tutalitafutia ufumbuzi suala hili ili kuona kuwa tabia hii hairejei mara kwa mara kwani inasumbua wananchi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu (a) wizara zetu zitabuni utaratibu mzuri ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua na adhabu kama ikibainika makosa haya yanatendeka katika Kampuni za Mafuta.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na kutokuwa udhibiti mzuri wa wamiliki wa vituo. Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba kupanda kwa bei za mafuta kiholela kunazidisha hali ngumu ya maisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba kupanda kwa mafuta basi inasababisha usumbufu kwa wananchi kwa hatua kubwa sana. Lakini kwa sasa tunachokitafuta kujua tatizo gain au sababu gani zinazosababisha kupanda kwa mafuta hayo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kutokana na jibu lake hili haoni kwamba inasikitisha kwa wizara ambayo ndio imepewa dhamana ya kusimamia suala hili kuwa hadi leo haijui sababu za kupanda kwa bei hizi holela kunakosababishwa na wafanyabiashara hawa kama alivyokiri mwenyewe.

(b) kuna taarifa kwamba bei ya mafuta inaongezeka kwa sababu pia kodi kubwa ambazo zinatozwa na serikali katika bidhaa hii. Je, suala hilo ni kweli na kama ni kweli serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi hizi ili wananchi wasiendelee kuathirika kupanda kwa mafuta.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kupanda kwa bei ya mafuta sababu zake tunazijua na sababu hizo ni za nje ya uwezo wetu kwa sababu zinatokana na soko la mafuta lilioko nje ya nchi, ambako sisi ndiko tunakopata mafuta hayo.

Kwa hivyo, tunajaribu kuzungumza na waagiziaji wa mafuta kujua namna gain wanaweza kudhibiti hizi bei au angalau zitulie kwa muda mrefu kidogo. Sasa hilo tunajitahidi lakini liko nje ya uwezo wetu, lakini linaigusa nchi, wananchi na kwa hivyo hatutochoka kuzungumza na waagiziaji wa mafuta ili ku-*stabilize* hizi bei.

Suala lake la pili la (b) lilikuwa ni kodi. Mhe. Mwenyekiti, nitalifanyia kazi na nitamjibu kwa maandishi, lakini nina hakika kodi iliyopo ni kodi hii hii inayotolewa nchi nzima na sidhani kama serikali imeongeza kodi ya mafuta. Lakini nasema kwa sababu sina hakika nitalifanyia kazi na baadae nitamjibu kwa maandishi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na mimi kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba moja linalosababisha kupanda kwa bei ya mafuta mara kwa mara ni kwamba Zanzibar tuna Wizara ya Ardhi na Nishati ambayo hiyo ndio mhusika mkuu wa mambo ya nishati yakiwemo mafuta na wakati huo huo ZRB niwakusanyaji wa mapato. Je, haoni kama kumpa mkusanyaji wa mapato kupanga bei za mafuta anazidisha kupanga bei mara kwa mara na je, wizara yake ikiwa ndio Wizara ya Nishati haioni kama kuna haja ya kupanga bei za mafuta kurudishwa katika Wizara ya Nishati ili kupanga bei kwa sababu huo ndio wahusika wakuu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kuna kamati maalum wanakaa pamoja inayokusanya Wizara ya Fedha, Wizara ya

Nishati pamoja na ZRB kuzingatia bei za mafuta, sio ZRB peke yake ndio inayopanga bei za mafuta. Kwa hivyo, kupanda kwa bei za mafuta zinahusiana na wizara mbili kwa tatu na tunakaa pamoja kuzingatia mahitaji ya wananchi, bei zinazozungumzwa na mikutano hii tunafanya mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba kama bei inapanda basi kuna sababu za msingi za kupandisha hiyo bei. Lakini si kwamba kuna mtu mmoja peke yake huyu anapandisha bei na huyu ndiye anayekusanya mapato, hiyo sio sahihi.

Nam. 132

Ukosefu wa Upatikanaji wa Viwanja
Vinavyotolewa na Serikali

Mhe. Fatma Mbarouk Said - Aliuliza:-

Kumekuwa na ugumu wa upatikanaji wa viwanja vinavyopimwa na Serikali kwa wananchi wa kawaida hata kama wamekamilisha utaratibu unaotakiwa.

(a) Serikali haioni kwamba tatizo hili ndilo linalowapelekea wananchi kujenga kiholela hata kwenye maeneo yasiyofaa.
(b) Ni sababu zipi zinazopelekea waombaji hawa kunyimwa viwanja hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 132 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali imetenga maeneo kwa ajili ya makaazi kwa bahati mbaya sasa maeneo hayo ni machache hali ambayo inapelekea usumbufu wa upatikanaji wa maeneo ya makaazi, aidha Serikali imo mbioni kutafuta maeneo zaidi ili kutatua tatizo hilo. Tatizo hili kwa kiasi kikubwa linasababishwa na hali ya kipato cha wananchi kinachopelekea kuvamia maeneo yasiofaa ambayo gharama za ujenzi katika maeneo hayo ni ndogo ukilinganisha na maeneo yaliyopimwa na kutolewa rasmi na Serikali.

(b) Mhe. Mwenyekiti, hakuna mwananchi anaenyimwa haki ya kupata kiwanja isipokuwa kuna uchache wa viwanja vyenyewe.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, pia nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mimi nataka kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe.

Mwenyekiti, ni maeneo gani wizara yako inategemea kuwapimia wananchi viwanja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, tunayaangalia maeneo ya Kisakasaka na hivi leo mchana nitakwenda kuliangalia hili eneo na liko tupu na ni kubwa, lakini pia maeneo ya Tunguu hayajamalizika tuyaangalia yaliyobakia. Kwa hivyo, bado Kisakasaka na Tunguu huenda tukapata nafasi yakuvigawa viwanja au yakupata viwanja hata 160. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi astahamili atupe muda ili tuweze kufanya hiyo kazi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba hakuna mwananchi aliyenyimwa kupewa kiwanja iwapo ameomba ile ni kutokana na uchache wa viwanja. Naomba kujua je, yeye kama Naibu Waziri anayo taarifa kwamba kuna wananchi waliomba viwanja Matemwe na wamelipia zaidi ya 200,000 na hadi leo hawajapewa hati. Kama anayo taarifa anakusudia kutufanyia mchezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, taarifa hiyo ya Kiwengwa mimi sina na kama nilivyoeleza mwanzo hakuna mwananchi yeyote ambaye amekoseshwa hati yakuomba kiwanja, na yeyote yule ambaye anayeomba kiwanja basi tunaangalia jinsi gani yakumpatia kiwanja hicho. Mhe. Mwenyekiti, tutakapovipata viwanja hivyo basi tutampatia kiwanja hicho.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri mwaka 1964 serikali ilitangaza kama ardhi yote ni mali ya serikali. Lakini hata hivyo kuna wananchi ambao kuwa wana maeneo yao ambayo wamemiliki na serikali inapotaka kupima viwanja inabidi mwananchi yule kwa vile ardhi ni mali ya serikali, basi pengine alipwe fidia au aondoke kwa ajili ya kuiachia serikali na kufanya haja ambayo kuwa inataka kutumia. Je, serikali inapotaka kupima viwanja na ardhi ile ni ya mwananchi ambaye kuwa ameimiliki. Je, serikali inachukua juhudi gani kumuona yule mmiliki wa ardhi inamuenzi vipi yeye.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, serikali haimpi mwekezaji kabla ya kulipa wananchi fidia, na wananchi wote hupewa fidia zao kwanza baadae eneo hilo ndio likakodishwa na serikali. Kwa hivyo, hilo ni moja la kumjali mwananchi kwamba kweli serikali inajali wananchi wake na inajitahidi kufuatilia kuhakikisha kwamba wananchi wamepewa fidia zao.

Nam. 144

Ukosefu wa Kituo cha Afya cha Kisasa – Tumbe

Mhe. Rufai Said Rufai - Aliuliza:-

Maeneo mbali mbali hivi sasa yameshakuwa na Vituo vya Kisasa vya Afya. Hata hivyo, Kituo cha Afya kilichopo kwenye Jimbo la Tumbe ambacho huhudumia wananchi walio wengi bado jengo lake ni dogo sana na lisilokwenda na wakati. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa Tumbe Kituo cha Afya cha Kisasa, ili kuwapunguzia mzigo wa kufuata huduma muhimu masafa marefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 144 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Tumbe ni cha huduma ya afya ya msingi *(1st line)* kilichofanyiwa ukarabati miaka miwili iliyopita. Kituo hicho kiko jirani na Kituo cha Konde chenye Daraja la Pili *(2nd line)* nategemea wawakilishi wanafahamu sasa hivi nikizungumza first line ni nini na second line ni nini kwa sababu nimeshalitolea ufafanuzi si mara moja wala mara mbili na pia Hospitali ya Micheweni iko karibu na kituo cha Tumbe. Aidha, wananchi wa Chimba wanakaribia kumaliza ujenzi wa kituo ambacho nacho ni jirani zaidi na Tumbe. Tunategemea vituo hivyo vitapunguza mzigo wa wagonjwa kwenye Kituo cha Tumbe.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata tena nafasi hii pia nashukuru majibu ya Mhe. Naibu Waziri lakini nina swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, amesema kwamba Kituo cha Tumbe kiko karibu na Konde na Micheweni, lakini Mhe. Mwenyekiti, kutoka Tumbe hadi Konde ni kilomita sita na kutoka Tumbe hadi Micheweni ni karibuni kilomita 12. Lakini kwa kuwa Mji wa Tumbe kila siku unakuwa na Tumbe ni sehemu yenye bandari kubwa wavuvi hutoka maeneo mbali mbali kuweka dago pale Tumbe. Kwa kuendelea na pale kuwa na kituo kidogo na kikongwe sana kina vyumba vitatu tu, chumba cha daktari ndicho hicho hicho chumba cha kupimia wagonjwa.
Je, Mhe. Naibu Waziri kuendelea kutumia kituo hicho si kuwadhalilisha wananchi wa Jimbo la Tumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, katika taratibu za Wizara ya Afya huwa zinapanga vituo kwa mujibu wa vigezo vilivyopo katika sehemu husika. Kama tunavyofahamu kwamba huwa tunaangalia katika sehemu ile vituo vimekaa vipi na ndio maana nikakutajia hivyo vituo ambavyo nimevitaja. Kituo cha Chimba kitakuwa karibu zaidi na pale kwa hiyo kama watu watakuwa wanagawanyika katika sehemu hizo nne nilizozitaja mzigo wa Tumbe hautokuwa mkubwa. *First line* na *second line* ni vituo ambavyo vimeanishwa kabla kwa hiyo huwa tunafuata utaratibu ule.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kigezo chengine huwa tunatizama idadi ya watu sasa hilo tutalifanyia kazi tuone jinsi gani kama kweli kuna haja ya kupandisha hicho kituo kuwa first line kwenda second line baada ya kituo cha Chimba kuanza kufanya kazi, tutapata takwimu ya watu wanaohudhuria katika kituo hicho. Hicho ndicho kitakachotuwezesha sisi kuamua nini kifanyike. Kwa hivyo, naomba usubiri kituo cha Chimba kifanye kazi halafu tutapata, tukipata tutajua nini chakufanya.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana aliyojibu Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa kituo cha Tumbe kinatoa huduma ya afya ya mama na mtoto kwa maana ya kupima ujauzito pamoja na kuwapima watoto. Na kwa kuwa ni chumba kimoja tu kidogo ambacho kinatumika kwa shughuli zote mbili hizo na kwa kuwa Tumbe, Micheweni na Vitongoji uwezekano wa wajawazito kuwa wengi ni mkubwa kutokana na mazingira yake ya bahari.

Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini atafikiria kuongeza chumba chengine kwa ajili ya kupimia mama na wajawazito ili ikitokea kesi ya kujifungua chumba kimoja aweze kujifungua mama na chumba chengine kitumike kwa shughuli za kupimia watoto na wajawazito.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kituo cha Tumbe kilivyojengwa na kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kimejengwa vyumba vitatu, hapo mwanzo kilikuwa kinatosha kwa huduma za first line. Kama ni first line tuna huduma ambazo zinatakiwa pale zitolewe na vyumba hivyo vingetosha kufanya hivyo, lakini kama kuna huduma za zaidi zinatolewa ina maana kwamba haifanyi sasa kazi kama huduma ya first line tena isipokuwa kuna ya ziada.

Na hicho ndicho kilichonifanya nikasema tuangalie Chimba itakapofanya kazi tutaangalia na sehemu ile yote tukiona kwamba hili linahitajika kufanya tutafanya sisi hatuna ubishi, tunataka kina mama wapimwe najua mimi unapochukua mimba ukaanza kwenda mbali mimi nimeshazaa kwa hiyo najua

yote hayo. Mhe. Mwenyekiti, katika watu ambao sitaki wapate tabu na nitakaowachukulia juhudi ya moja kwa moja katika kipindi hiki ambacho mimi niko hapa katika Wizara ya Afya hilo moja nataka kulihakikisha kwamba kina mama hawatopata shida katika jambo hilo.
Kwa hiyo kama nitakuja kumudu maana inategemea kina mama watapima karibu, kina mama watazaa bure, kina mama watafanyiwa huduma bure. Lakini hayo kama nitawezeshwa. Kwa hivyo, sasa Mhe. Mwakilishi mimi naomba nitoe ushauri kuna Mwakilishi na Mbunge hebu jitahidini basi hata chumba kimoja, wajengeeni wananchi wenu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe leo hapa tuna mgeni mzee wetu Mzee Ramadhan Nyonje Pandu tunamuomba asimame kidogo, mgeni huyu alikuwa ni Mwenyekiti Mstaafu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza hili wakati wa kipindi chake, lakini leo amefika hapa kwa ajili ya mwaliko wa Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kama alivyokuwa amezungumza Mhe. Spika, jana kwamba kulikuwa kuna wajumbe ambao walikuwa wana haki ya kuchangia leo, lakini kutokana na muda tunaomba wajumbe wale watustahamilie. Lakini tumepata fursa yakuweza kumkaribisha Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili aanze kuchangia.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa asubuhi ya leo na mimi niweze kusema machache katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kama ilivyo ada kwa kutujaalia sote tukawa wazima asubuhi hii na tukaweza kuja kutekeleza majukumu yetu. Kama ambavyo tumeomba kwa wananchi na wakatukubalia tukaweza kufika katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nguvu zote kabisa nimshukuru na nimpongeze kwa dhati Mhe. Waziri wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa hotuba yake nzuri aliyoieleza kwa kina na ameweza kuiwasilisha kwa ufasaha zaidi.

Nampongeza sana yeye pamoja na wasaidizi wake wote katika wizara hii, Mhe. Naibu Waziri, ndugu Katibu na Watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu sio mkubwa sana zaidi nikupongeza utendaji wa wizara hii kwa muda mfupi Mhe. Waziri aliokabidhiwa na kiwango kikubwa cha mafanikio ambayo tumeweza kuyaona. Mhe. Mwenyekiti, nianze na ujenzi wa jengo jipya la abiria la pale Kiembesamaki.

Mhe. Mwenyekiti, jengo hili siku zote tulikuwa tukilizungumza ndani ya Baraza hili kwamba lina umuhimu wa aina ya pekee endapo Zanzibar tutafanikiwa kulijenga jengo la kisasa la Uwanja wa Ndege. Nasema hivyo kwa sababu lengo kubwa la Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuifanya Zanzibar hatimae kuwa ni kitovu cha biashara, na tumesema ili kufikia lengo hilo basi hapana budi *airport* pamoja na bandari zikafanyiwa marekebisho ya hali ya juu ili ziendane na wakati. Na kwa muda mfupi Mhe. Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wake baada ya kukabidhiwa wizara hii tunaona mafanikio ambayo yanaendelea pale kwa kasi, nawapongeza sana tena sana.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mawasiliano tumeliona likipiga hatua kubwa ya mafanikio, tumekuwa na taasisi nyingi sana katika masuala ya usafiri, lakini pia katika masuala ya mawasiliano ya simu. Katika mawasiliano ya simu Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kulipongeza sana Shirika la Zantel. Zantel imekuwa ikifanya kazi zake vizuri, lakini zaidi tulikuwa tukihimiza mashirikiano ya karibu ya taasisi hizi pamoja na jamii kwa jumla. Hili limekuwa likionyeshwa na tumekuwa tukilishuhudia kwa Shirika la Zantel linavyosaidia jamii zetu. Mhe. Mwenyekiti, limesaidia kwa kiasi kikubwa taasisi binafsi tunazoziita *NGO's* za wananchi wetu kwa kuwasaidia kifedha, lakini pia kuwapatia taaluma za aina mbali mbali.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba basi kupitia wizara hii kwamba serikali inapowapa vibali taasisi kama hizi basi na wananchi nao wafaidike kutokana na taasisi hizi. Mhe. Mwenyekiti, mfano mzuri tunauona kwa Zantel hivyo naomba na taasisi nyengine ziige mfano huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesema sitokuwa na mengi kubwa ni kuipongeza wizara hii na zaidi kwa mashirikiano waliokuwa wakinipa tokea nichaguliwe na wananchi wa Jimbo la Fuoni kwa suala zima la ujenzi wa barabara. Mhe. Mwenyekiti, barabara inayoanzia Tunguu inayopita katika Jimbo la Fuoni, Mwanakwerekwe, Magomeni na hatimae Mkunazini Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba inajengwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimeiona na inakwenda kwa *speed* nzuri, nimesema sitomtendea haki Mhe. Waziri kama sitomshukuru kwa hili kwa sababu njia ile tulikuwa tunaona sote ilikuwa ishakaribia kuwa ni kero kubwa, lakini sasa kwa ujenzi ule Mhe. Mwenyekiti, tunafarijika na namuomba Mhe. Waziri kwamba apokee salamu za wananchi wa Jimbo la Fuoni pongezi zao kwamba wanashukuru njia ile inafanyiwa utanuzi lakini na pia ujenzi katika kiwango cha kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la njia za ndani nalo ni suala ambalo nimeona nimpongeze Mhe. Waziri kwamba wameanza kuliona kwa Jimbo la Fuoni. Mhe. Mwenyekiti, tumeanza na njia ya Meli Tano pale Msikitini kwendea mpaka Chunga kwa mashirikiano ya pamoja inaendelea vizuri. Lakini kwa kuwa Jimbo la Fuoni ni jimbo ambalo ni mji unaochipuka kwa haraka, wahamiaji wanakuwa ni wengi kwa hiyo njia zile wananchi wanapita mara kwa mara. Kwa hivyo, kuna umuhimu wakuzitilia mkazo ujenzi wa njia hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru viongozi kwamba wameliona hili na wameanza kulifanyia kazi. Lakini njia za ndani ni nyingi katika jimbo hili, tuna njia nyengine kutoka Meli Sita Fuoni pale kwenda Kitongani Skuli, lakini kuna njia nyengine kutoka Fuoni Sokoni ambayo inaenda mpaka Kisakasaka.

Njia hizi zilikuwa zimetolewa ahadi na viongozi wetu wa kitaifa, lakini sote tunafahamu viongozi wetu wa kitaifa wana ahadi nyingi sana wanazitoa katika maeneo mbali mbali, na kwa hivyo kwa uwezo wa serikali peke yake hatutegemei kwamba zitaweza kujengwa kwa haraka kama ambavyo wananchi wanategemea. Hivyo nilikuwa naomba nishauri Mhe. Mwenyekiti, kupitia kwako Mhe. Waziri kwamba nimeona katika hotuba yake kuna miradi ya njia za vijijini, kwa sababu viongozi wetu wanapotoa ahadi hizi ni maagizo kwa utekelezaji.

Kwa hivyo, basi tuangalie kama inawezekana miradi kama hii tuwe tunaielekeza kwenye ahadi zile za viongozi wetu wakuu, ili wananchi wasije wakalalamika kwamba mbona Mhe. Kiongozi katoa ahadi njia fulani itajengwa lakini sasa miaka mitatu au miaka minne bado haijajengwa. Kwa hivyo, badala ya kuibua miradi katika njia ambazo hazijatolewa ahadi basi tuone kwamba tunawatendea haki viongozi wetu wanapotamka kwamba njia zile zitatengenezwa basi tuibue miradi kwa kuanzia njia zile ambazo zimetolewa ahadi.

Kwa mfano, ni njia hizi mbili katika jimbo hili la Fuoni.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuna miradi ya njia za vijijini, ni kwamba nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu ya wingi wa njia hizi za Fuoni basi angalau kipindi hiki aangalie kwa jicho la imani Jimbo la Fuoni tupate utekelezaji wa njia hizi za ndani. Tuna njia ya Fuoni-Jumbi kwenda Kibondeni Skuli, tuna njia ya Fuoni inaanzia pale Njia Mbili kwenda Birikani, pia kuna njia ya Fuoni-Meli Tano pale Msikitini ambayo nashukuru Mhe. Naibu Waziri ameshaianza kuifanyia kazi hii inaishia mpaka Chunga nayo ni ndefu kidogo. Lakini pia kuna njia ya Mashine ya Maji pale Kijitoupele inakwenda mpaka Nyarugusu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anione kwa jicho la imani na njia hizi japo kwa sababu hapa nimeziorodhesha ziko saba pamoja na hii ambayo iko kwenye mradi wa ujenzi wa barabara za serikali ya Kwarara mpaka Maungani nashukuru imeshaanza kufanyiwa kazi imefika kiasi robo tu haijakaribia hata nusu, lakini nina imani kubwa kwamba itakamilishwa. Kwa hivyo, na hizi nyengine nazo tuziangalie ili wananchi wetu waweze kupita na hasa wanawake wanapokuwa wajawazito, lakini pia na wagonjwa na jamii nzima kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi nilikuwa na hayo nilisema niyasema hapa ili nimsikie Mhe. Waziri atakapojumuisha pamoja na hotuba yake hii nzuri naiunga mkono kwa asilimia mia moja mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Fuoni ambao wamenituma nije Barazani hapa kuja kuwakilisha. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Machano Othman Said (Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kushukuru sana kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Lakini pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kufika hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa wizara hii kwa utendaji wake pamoja na Naibu Waziri na watendaji wao wote. Wamefanya kazi nzuri, wana mipango mizuri na tunawaombea heri Mwenyezi Mungu awajaalie wafanikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilibahatika mara mbili kwenda wizara hii, nilikwenda mara ya kwanza nikiwa Naibu Waziri mwaka 2006 na kwa hapa naomba niwashukuru watu wawili. Kwanza namshukuru sana Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kwa kuniamini na kuniweka pale kama Naibu Waziri. Lakini pia namshukuru tena Mhe. Mwakanjuki aliyekuwa Waziri wa

Mawasiliano na Uchukuzi, tulifanya kazi vizuri na bahati nzuri ni mtu ambaye ana mashirikiano mema sana na anakusaidia kuelewa mambo sana. Kwa hivyo, natumia nafasi hii kumshukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, nilikaa pale mwaka 2006 mpaka 2007 nikateuliwa kuwa Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi na teuzi zangu zote zilikuwa mwezi wa 6 na kule ilikuwa mwezi wa 6. Mhe. Mwenyekiti, mwezi wa 6 tena mwaka 2008 nikateuliwa tena kurudi Wizara ya Mawasiliano, namshukuru sana Mhe. Rais. Lakini katika vipindi vyote viwili kuliwa na changamoto nyingi sana. Nilipokuwa Naibu Waziri na nilipokuwa waziri, niliporudi mwaka 2008 nilikuta kuna changamoto nyingi za barabara. Barabara ya Tunguu, Kinyasini ambayo ilikuwa ikijengwa na *S.S. MEHTA* ilikuwa karibu kuvunja mkataba.

Nazungumza haya halafu baadaye kuna jambo nitataka nilizungumze. Nilivyofika nikamuomba Mhe. Rais ile kazi aniachie niendelee nayo. Tusivunje makataba na *S.S. MEHTA* bahati nzuri akanikubalia, tukapanga na watendaji wangu, tukamsimamia, tukamsaidia kazi ile ikawezekana. Kuna kipindi mjenzi yule aliishiwa na lami, akatwambia sina lami. Nikamwambia sisi tutawakopesha lami. Uhisiano na mjenzi na mjengewa ni lazima uwepo. Tukamkopesha lami kwa misingi kwamba baadaye atulipe na alitulipa na bahati nzuri kazi yetu ikafanikiwa na tukaweza kumaliza.

Lakini kwa kipindi chote wajenzi wetu wakubwa Zanzibar ni Kampuni ya saizi za kati sio Makampuni makubwa, kwa sababu kazi zetu sio kubwa sana za ujenzi. Kwa kipindi cha miaka mitano tulikuwa na Kampuni ya *SPEACON, KUNDSINGH, S.S. MEHTA* hizi zote za Kenya na kampuni za Kitaliana *PRISMO* na *CO-GEAL*. Hawa ndio waliokuwa wakifanya kazi Zanzibar. Lakini kwa bahati mbaya hizi zote za Italii zilifeli kabisa. Barabara ya Mazizini Fumba, Amani /Dunga, Mfenesini/Bumbwini hizi zilikuwa zimepewa *PRISMO* na *CO-GEAL*. Wakashindwa na walishindwa barabara ya kwanza tu. Serikali ikamtafuta *MECCO*. Akaijenge barabara ile kwa kiwango kizuri kwa bilioni 5 nafikiri sote tukaridhika.

Tulipojenga kwa *MECCO* utoaji wa miundo mbinu pale ilikuwa ni yetu sisi, lakini tulikuwa hatuna fedha akatukopesha milioni 11 akawalipa Shirika la Umeme na watu wa Maji. *MECCO* huyu tumempa kazi Pemba lakini tukampa kazi ya Bumbwini, Kampuni ya *MECCO* imetukopesha au ilituazima milioni 240 na zaidi kuondoa miundombinu ya Bumbwini ili kazi ianze.

Sasa naomba waheshimiwa wawakilishi wenzangu katika mambo haya ni kutoa na kupokea huwezi ukawa unapokea wewe tu. Kama mtu anakujengea anakukopesha kiasi hicho, anapofika na yeye anaposema niazimeni gari nifanye

kazi yenu, mimi sijaona ubaya kama anakutengenezeeni na gari yetu. Sasa Waheshimiwa hii ni Kampuni ya kizalendo na historia yake kampuni hii mwanzo ilikuwa ni kampuni ya Serikali na imeuzwa kwa wanachi wa Tanzania na haijawahi kufeli tangu imeanza kufanya kazi Zanzibar.

Mimi namuunga mkono Mhe. Waziri kama kuna utaratibu wa kuazimana basi endeleeni na wananchi nafikiri waelewe tu kwamba hii Kampuni inasaidia. Imepita katika vipindi vigumu sana. Kama nilivyozungumza *ADB* baada ya kukwama ule mradi walitwambia SMZ mjenge wenyewe barabara. Sisi ndio tuliowambia kwamba tutajenga wenyewe kwa fedha zetu isipokuwa nyinyi *ADB* mtujengee ya Amani/Dunga na ya Mfenesini Bumbwini. Wakakubali na wamekuja kukagua kazi na wakaona inakwenda vizuri.

Nashukuru nimepita wiki iliyopita barabara ya Dunga/Amani wanakwenda vizuri tu na leo nimepita asubuhi nimewakuta wameshafika Amani pale wameikwangura. Natarajia kwamba watafanya kazi vizuri na Waheshimiwa wengine wamesema hapa. Mhe. Mgeni kazungumza kwamba kaiyona barabara inavyojengwa, inajengwa katika viwango. Mimi nahisi suala hili waheshimiwa tuende nalo na tutarajie kwamba tutafanikiwa.

Pia nizungumze barabara za Pemba zaidi Kaskazini Pemba. Kwa muda mrefu tulikuwa na tatizo la kisiwa cha Pemba kutokuwa na barabara. Tulivyoanza mradi wa Kaskazini Pemba barabara tatu ya Wete/Gando, Wete/Konde na Wete/Chake-Chake tulikumbana na matatizo makubwa ya wajenzi, mgogoro mpaka tukasaidiwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kati ya wabia hawa wawili wa ujenzi. Lakini kwa busara na maarifa tatizo limetatuka barabara za Gando zinajengwa na barabara ya Konde inajengwa. Naomba tuwape moyo hawa watu wa Mawasiliano Mhe. Waziri na watendaji wake waweze kuendelea mbele.

Mipango ya Serikali kwa sababu tunatengeneza mipango ya miaka mitano kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ukiungalia ukurasa wa ilani 175 mpaka ukurasa wa 178 utaeleza pale kazi na barabara ambazo zitafanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano. Lengo kubwa la serikali kwanza kumaliza miradi hii mikubwa kabla ya 2013. Wakati tunaendelea na miradi mikubwa na miradi midogo aliyosema Mhe. Waziri inaendelea. Sitarajii kwamba barabarazote za majimbo, *feeder road* na nini kwamba tutafanya kwa bajeti moja.

Mhe. Spika, serika tuna vipa umbele vingi sana. Nafikiri juzi tumeona kwamba na maji nayo ni tatizo na serikali nayo ikaipa kipaumbele kwenye maji. Kwa hivyo kwenye barabara tunakwenda kwenye maji tupo, na kwenye afya tupo.

Kwa hivyo waheshimiwa aliyekuwa mwaka huu hayumo naaomba astahamili mwakani atakuwemo. Kila kazi hizi zikipungua na kila mtu anazidi kuonekana. Kwa sababu kama barabara Kuu zikimalizika nina hakika barabara za vijijini na sehemu yengine zitafanikiwa katika ujenzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kidogo katika usafiri wa baharini. Tumezungumza hapa umuhimu wa sekta hii, lakini pia na mchango wake katika uchumi na matatizo yapo ambayo yapo katika sekta hii. Ni kweli sekta hii ina matatizo lakini kwa vyovyote inasaidia sana. Usafiri wa Zanzibar Dar-es-Salaam ni mkubwa, usafiri wa Zanzibar Pemba ni mkubwa na hatuwezi kuuepuka kutokana na hali yetu. Katika 2009 nafikiri kulitokezea ajali ya M.V. Fatih, meli ilizama katika bandari ya Zanzibar, tukaunda Tume. Tume ile Mhe. Mwenyekiti, iliongozwa na Mhe. Jaji Makungu, mtu mwenye busara, mtu makini na waliandika ripoti nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ile mimi niliisoma kwenye Baraza la Wawakilishi lile lilopita tukiwa katika ukumbi wa Mnazi Mmoja. Waheshimiwa kama wanataka kuona matokeo ya ripoti ile basi wakatafute Hansard za Baraza wataona kile ambacho kilizungumzwa pale. Kuna watu pale tuliwaadhibu akiwemo Kepteni wa meli tulimfungia sijui miaka miwili au sijui miaka mingapi. Kuna wengine wakapata adhabu mbali mbali na mwenye meli hukumu yake ilikuwemo mle. Kwa hivyo nafikiri jambo hili lishughulikiwa zizuri.

Nizungumzie kidogo uzwaji wa tiketi. Waheshimiwa wengine wamelipigia kelele. Hili lina pande mbili la shilingi. Tulianzisha utaratibu kwamba kila msafiri aende na kitambulisho chake chochote, hata kama barua ukiwa huna kitambulisho useme kwamba miye ndiye machano. Lakini pia wananchi wenyewe hawaipendi basi na wale walanguzi wanatokezea. Ni jambo baya na tunamuomba Mhe. Waziri ili ajitahidi kulishughulikia na alisimamie vizuri ili ile hali ikae vizuri.

Lakini kwa vyovyote tuwapongeze wenye meli. Mimi naona wanafanya kazi nzuri pamoja na umasikini wao na juhudi zao lakini wanatusaidia na mambo yanakwenda vizuri. Wenye meli wote mimi nawapongeza sana, wanajitahidi sana na lazima tuoneshe kwmba kuna jambo linafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie kidogo furaha yangu ya kuona kwamba hatimaye sasa Idara ya Anga inabadilika na kutoka Idara na kuwa Mamlaka. Hichi ni kilio cha muda mrefu wa waheshimiwa wawakilishi, wananchi na watu wenyewe wa Idara. Ndio maana kuna baadhi ya wajumbe wamesema uwanja wandege gani hauna maji. Inawezekana kwamba Uwanja wa Ndege utakuwa chini ya Idara. Idara hata shilingi laki moja lazima wakaiyombe

serikali, tupate hiki tukanunue hiki, tukanue hichi. Sasa hivi ni mageuzi haya. Mimi nayaunga mkono sana mageuzi haya. Kwamba tunatoka katika Idara tunakwenda kwenye Mamlaka yenye maamuzi.

Kwenye mabadiliko haya kuna mambo mengi yatatokezea na lazima tuwe tayari kuyakabili, watapekuwa kwenye mikataba iliyokuwepo Uwanja wa ndege. Wataangalia mambo yote ambayo yanastahiki kuwepo na kutokuwepo. Hilo sio jambo kwa sababu binaadamu anakwenda mbele. Pale *airport* tuna makampuni makubwa na madogo watu wamezungumzia jana kama *ZAT*, lakini kidunia sasa hivi na kwa masharti ya *IACOS* na *IYATA* hutakiwi kuwa na *handling* moja katika *air port* lazima unatakiwa uwe na ushindani kusiwe na *monopoly*.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama ni wa Kimataifa na kwa bahati mbaya au nzuri sasa hivi pia kuna chama cha kuwalinda watumiaji wa huduma za Anga na wao wanalalamika kwamba heeling lazima iwe na ushindani. Ukiangalia pale *airport* kuna matenki ya mafuta. Serikali imeingia mkataba na yule mwenye matenki, lakini mkataba wenyewe serikali inapata shilingi 2 kwa lita. Sasa hebu fikiria mafuta sasa hivi ni shilingi 2,000/- lakini wanapata shilingi 2.

Haya mambo lazima mamlaka mpya itayaangalia, tuwe tayari kuona kwamba inaangalia ili serikali iweze kupata uchumi iinue mapato yake. Kama maduka mengi wataangalia, watayatoa. Kwa sababu waliopewa pale wote wamepewa masharti kwamba tukipahitaji mnatoka. Nafikiri haya mambo yana uwezo wa kuangaliwa na wizara na wizara wakajipanga vizuri kama watawatoa nje au watawapeleka wapi ni wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, viwanja vya Ndege vyote jamani duniani vina maduka, si Dubai, si Nairobi si wapi. Huwezi kwenda kwenye *airport* msafiri halafu ukashuka chini halafu tena utoke tena urudi tena ndani, nafikiri hili halipo. Huo utaratibu nafikiri watajipangia mzuri ambao utaonekana unafaa.

Jambo jengine ambalo nataka kulizungumzia kwa ufupi ni Shirika la Bandari. Mimi nawapongeza sana wanajitahidi sana. tujue kwamba sisi Zanzibar sehemu zetu mbili kuu za uchumi ni bandari na *airport*. Bahati nzuri *airport* kwamba ilikuwa idara, serikali imewekeza katika kujenga *run way* ambayo tayari. Serikali ina mpango wa kujenga *tax way*, serikali ina mpango wa kujenga *apron* pamoja na new *terminal*. Pia serikali hii imejenga na uzio. Haya mambo manne yaliyofanyika kwa *airport* yataimarisha sana uchumi wetu na kuzishawishi mashirika mbali mbali kuja Zanzibar kutua na kuimarisha uchumi. Kwa upande wa pili wa Bandari naomba na serikali kama ilivyokusudia Wizara iendelee na utaratibu wa kuliimarisha Shirika la Bandari.

Waheshimiwa niwaombe kwamba vifaa vya bandari navyo ni ghali, tukisema tutumie mtaji wa Shirika la Bandari tutaliuwa.

Nafikiri Mhe. Waziri mipango yako sio mibaya endelea nayo kulihuisha Sherika la Bandari tushindane na bandari za Dar-es-Salaam, tushindane na bandari za Mombasa. Katika kipindi hiki ambacho tunataka kuelekea katika ujenzi mpya wa bandari. Wakati lengo letu ni kujenga bandari mpya tusiisahau na ile ya zamani. Inatutilia tija sasa hivi, tusiiwache. Waswahili wanasema, "Usiache mbachao kwa msala upitao.**"** Tuendelee na juhudi za kutafuta uwezo wa kujenga bandari mpya kama serikali zinavyoendelea nazo. Nakuunga sana mkono Mhe. Waziri lakini pia tuiimarishe ile bandari ambayo tunayo sasa hivi.

Jengine kuhusu Shirika la Meli. Sherika umelizungumza vizuri, bila ya utaratibu uliosema Mhe. Waziri Shirika hili litakwama. Na mimi naunga mkono suala hilo liendelee kama ambavyo umelipanga.

Naomba nimalizie kwa kuzungumzia Zantel. Zantel ni kampuni yetu kwa sababu serikali ina hisa 18, kwa hivyo ni kampuni yetu. *Zantel* ina walipa kodi wazuri kuliko kampuni zote hapa Zanzibar. Mpaka leo pamoja na kuhamia Bara lakini bodi ya Wakurugenzi ya Zantel na Serikali ina wawakilishi wake wawili. Kwa hivyo kile kitu ni chetu na kinasaidia maendeleo ya nchi yetu. Mimi niwaombe kama kuna Muheshimiwa hana laini ya *Zantel* basi ajitahidi awe nayo. Hata kama anayo laini nyengine, lakini Nam. 1 iwe laini ya Zantel ili kuimarisha pato letu.

Niwaombe Zantel kuna mambo mawili ya muhimu kwamba uwamuzi mkubwa umeshafanyika kwamba simu zote zisajiliwe lakini bado baadhi ya watu wanatumia simu ambazo hazijasajiliwa. Mhe. Waziri tunaomba suala hili kwa sababu wewe ndio Waziri dhamana ulifuatilie, ulishughulikie, ili liweze kukaa sawa.

Jengine kuhusu Zantel, miaka miwili nyuma kampuni hii ilikuwa inadhamini ligi kuu ya Zanzibar. Kwa bahati mbaya kulitokea mgogoro wa kimaslahi kati ya *ZFA* na *Zantel*. Kwa bahati nzuri Zantel sasa wana uongozi mpya wa kina bwana Moyo, *ZFA* ni wale wale. Hebu Mhe. Waziri tusaidie basi, wawezeshe ili Zantel wakubali kurudi tena kuizamini ligi ya Zanzibar, hata kwa kiwango kile kile cha mwanzo.

Maana mgogoro wao ulianza kwamba walikuwa wakizamini karibu milioni 110. *ZFA* wao walikuwa wanataka milioni 300. *Zantel* wakasema kama ni hivyo siye basi tafuteni kwahali muende. Lakini hatujapata mpaka leo. Mimi

naomba serikali izungumze na Zantel iwasaidie udhamini wa mpira. Mpira nao unasehemu yake katika maendeleo ya nchi hii na jamii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti la mwisho kabisa mawili kwa pamoja kwanza niseme naunga mkono bajeti hii ya Miundombinu na Mawasiliano kwa asilimia mia.

Pili nimeona kuwa baadhi ya waheshimiwa wamekuwe wazito kidogo, naomba watu wawili. Mimi Mhe. Hamza rafiki yangu sana siku tulipokubaliana tukachukue fomu tulikubaliana mimi na yeye mara ya kwanza mwaka 2000 na nikamwambia bwana weee leo ndio siku yetu tukachukue fomu. Tulikwenda kuchukua na sote tukashinda. Lakini niliyefuatana naye kwenda kuchukua fomu ni bwana Mtando. Alinisaidia sana kampeni jimboni kwangu alikuwa ana mkwe wake, alikuwa mgumu kidogo. Samahani lakini alinisaidia yeye na tukaipata hiyo kura.

Sasa naomba kama tulivyofanya mwaka 2000, kusaidia bajeti hii ipite vizuri kila mtu mwenye shida zake atasaidiwa. Serikali ipo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Nina hakika Mhe. Waziri ameyasikia mambo yao yatakaa sawa, Shauri moyo mpaka Mboriborini Mhe. Waziri analiweza hilo. Kuna mpango wa miaka mitano Mhe. Hamza nafikiri huwezi kukosa. Watu wanasema kila ukipata mwisho ndio kuna raha zaidi maana inakuwa kipya kipya. Maana ukipata mwaka 2014, 2015 mambo yako yanakuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo machache naunga mkono hoja hii kwa mara nyengine na nawashukuru waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sina budi na mimi kuungana na wenzangu katika kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, aliyetujaalia tukiwa wazima wa afya na kuwepo kwetu hapa.

Pili napenda nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuweza na mimi kutoa mchango katika kuijadili na kuichangia bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi na mimi tena kumshukuru kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi kwa ushindi mnono alioupata katika uchaguzi wa mwaka 2010. Pia sina budi kumshukuru Mhe. Rais kwa imani yake kwangu kuniteuwa kwa kushirikiana na Mhe. Hamadi Masoud Hamad kufanya kazi kwa maendeleo katika Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Pia nakishukuru kwa dhati kabisa Chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kunipa imani ya kwenda kusimama jimboni

kutetea kura kwa wananchi. Nawahakikishia kwamba imai hiyo haitopotea na nitakitumikia kwa nguvu zangu zote kwa mustakbali na maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Pia naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wenzangu wa Jimbo la Chwaka.

Baada ya utangulizi huo naomba na mimi nuchukue fursa hii kwa kuichangia bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kujaribu kujibu baadhi ya hoja zilizoelekezwa katika Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia tunajaribu kujibu hojia zilizoelekezwa katika Mamlaka na Viwanja vya Ndege. Wajumbe wengi wameeleza hisia zao, mitazamo yao na maoni yao. Ni imani yangu kwamba wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi tuna nia moja ya kutaka kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na nia ya kutaka kuwasaidia wananchi wetu wa Zanzibar. Malengo yetu viongozi sote ni kuhakikisha maisha ya wananchi wa Zanzibar yanaboreka kutoka pale yalipo leo kuwa mazuri zaidi kwa siku ya kesho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa viwanja vya Ndege kwa kuanzia na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alizungumzia suala la uwazi katika ujenzi wa uzio. Ni kweli kwamba katika ujenzi wa uzio unaoendelea katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume kuna sehemu zina uwazi. Sehemu hizo kuna sababu mbili.

- Ni utaratibu waliokubaliana kati ya Mkandarasi na wajengewa kwa maana kwamba Wizara ya Miundombinu chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

- Kuna baadhi ya wananchi ambao wamelipwa fidia hawakuridhika na fidia hizo.

Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege pamoja na Mkandarasi tumeendelea kuzungumza na watu hao na tunaamini fidia hiyo wataikubali na zoezi hilo litakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, kuendelea na mchango mengine wa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alichangia pia suala la ufungaji wa jenereta. Ni kweli kuna jenereta limenunuliwa na wenzetu wa Wizara ya Fedha kwa wakati huo. Katika ununuzi wa jenereta hilo kwa bahati mbaya hakukuwa na gharama za ufungaji wa jenereta hilo. Naomba nikiri kwa muda mrefu tatizo hili limechukua majadiliano marefu kati ya Wizara husika kwa maana kwamba Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu. Sote tunakiri kwa kipindi hicho mamlaka ya Uwanja wa Ndege ilikuwa ni idara na haikuwa na uwezo wa fedha wa

kuweza ku – *stole generator* hilo. Mhe. Mwenyekiti, imani yangu kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tatizo hili tumeliona na tunahakikisha kwamba tutajitahidi kutafuta fedha ili kuweza kuli – *stole generator* hili kunusuru matumizi na malengo ya ununuzi wa jenereta hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea na nchango wa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alielezea hisia zake na kutaka kujua sababu zilizopelekea kuwepo kwa duka la dawa baridi katika ukuta wa uwanja wa ndege.

Napenda nikiri hisia za Mhe. Mjumbe ni kweli duka hilo lipo na limejengwa katika ukuta wa uwanja wa ndege. Sababu zilizopelekea ni pamoja na ufinyu wa maeneo, mahitaji. halisi ya *pharmacy* hiyo na sababu nyengine.

Kwa upande wetu Wizara ya Miundombinu tumehakikisha kwamba tatizo hili linaondoka na tupo mbioni. Matarajio yetu baada ya Kikao hiki kitukufu cha Baraza lako tutakapoweza kupitisha sheria zetu mbili za mamlaka na usimamizi wa viwanja vya ndege, wizara yetu na mamlaka husika tutakaa na kujadiliana na kuona mikataba yote. Kuona kuwa mikataba hiyo tunaipitia upya na kuandaa mikataba ambayo kuwa itakuwa bora ikiwemo hasa suala la maeneo ikiwemo hasa maduka hayo na suala la *pharmacy*.

Pia naomba kujibu hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliyeeleza hisia zake juu ya hofu ya uvujaji wa mapato katika eneo la Uwanja wa Ndege. Tatizo la uvujaji wa mapato hivi sasa tayari tumeweka utaratibu mzuri wa kulikabili. Tunaweka njia nzuri za kuweza kuongeza makusanyo yetu. Miongoni mwa njia hizo ni kuona malipo hayo yanafanyika kwa njia za komyuta, tunafanya *reconciliation* pamoja na vitengo vya *ZAT control tours* na uhamiaji navyo pia vitaboreshwa katika ukusanyaji wa mapato hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jussa pia alionesha hisia zake na kutaka kupata taarifa kwa namna gani Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Mamlaka ya viwanja vya Ndege imejiandaa kwa kushirikiana na vyoo au taasisi nyengine za Kimataifa katika kutimiza dhima na malengo yake kuanzisha Chuo cha *Civil Aviation* hapa Zanzbiar.

Uanzishwaji wa Chuo hiki Mamlaka ya Ndege inashirikiana na vyombo vya kisheria ikiwemo chambo ha *TCAA* na *ICAO* pamoja na *UNDP* kwa ushauri wa kitaalamu. Serikali pia inaendelea kufanya mazungumzo na Mashirika na taasisi nyengine ili kuweza kupata misaada na ufadhili katika uanzishwaji wa chuo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Jussa alitaka kujua katika jaduweli lililooneshwa lilioneshwa tumeonesha kwa namna gani mizito imepungua katika Uwanja wa Ndege. Ni kweli mizio imepungua na sababu kubwa ni muamko wa wafanyabiashara wetu kupenda sasa zaidi mizigo yao kusafirisha kwa njia ya bahari. Sasa hivi kwa upande wa bahari muda unatumiwa ni muda mdogo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mahmoud Mussa alitaka kujua uhusiano uliokuwepo kati ya polisi na wafanyakazi wa Uwanja wa Ndege. Sheria za kimataifa zinazoongoza na kusimamia utendaji na uratibu wa shughuli za Viwanja vya Ndege zimeweka wazi. Masuala ya upekuzi na shughuli nyengine za pale katika Viwanja vya Ndege ni masuala yanayosimamiwa na wafanyakazi na watendaji wa viwanja vya ndege. Jukumu la polisi ni kulinda usalama kwa raia na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili pia Mhe. Hamza Hassan Juma alitaka kujua ni sababu gani zilizopelekea kuhamishwa kwa Afsa wetu kutoka nafasi ya uangalizi ya Ofisi hadi kuwa Afisi wa Mazingira. Kwa heshima kubwa sana ningependa kumjulisha Mheshimiwa kaka angu Hamza Hassan Juma kwamba utaratibu huu ni utaratibu wa kiutawala na ni jambo la kawaida katika shughuli zetu za kazi. Hakuna vitezo maalum au wababu maalum zinazolazimisha kwamba mtu apangwe katika eneo fulani. Huu ni utaratibu unaoendana na shughuli za utawala katika eneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuungana na hilo, Mhe. Wanu Hafidh Ameir alitusihi. Nasi tumezipokea nasaha hizo za kutaka kuboresha huduma za maji, umeme, kuweka vyombo vya ulinzi ikiwemo *CCTV*, vyombo vya matangazo na vyenginevyo, ili kuendana na hadhi tunayoitangaza Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, basi tunakiri kwamba tumepokea changamoto hiyo na tunaifanyia kazi na tunamshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, katika hilo pia Mhe. Mgeni Hassan Juma alitaka kujua kwamba katika ujenzi wa *new terminal* inayojengwa kwa kiasi gani ufanisi wa jengo hilo hasa sehemu za ndani utaweza kupatikana ili kuweza kuwaruhusu watu wengine kutoa michango yao.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa jengo jipya ni ujenzi unaojengwa kwa mfumo wa usanifu na ujenzi *(design and construct)* na sehemu ya *interior design* itatolewa baada ya kukamilika kwa *detail design* ya jengo hilo. Jengo hilo baada ya kukamilika litakuwa na uwezo wa kutumia abiria milioni 1.1 kwa mwaka ambayo ni sawa sawa na abiria 1900 kwa wakati mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili pia Mhe. Ali Salum Haji alitaka kujua kwamba serikali imekuwa ikimiliki henga ya Uwanja wa Ndege. Alitaka kujua hanga hiyo inamilikiwa na nani hivi sasa au wamekodishwa kwa kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hanga ipo na imekodishwa kwa kampuni ya mzalendo Kampuni ya *Aeroset* kwa mkataba rasmi na mkataba huo upo na hivi sasa ni kwa kipindi cha miaka minane. Mapato au ada ya hanga hiyo ni dola za Kimarekani 2,400 kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, narejea tena kwamba mategemeo yetu baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Mamlaka na Usimamizi wa Viwanja vya Ndege mikataba mingi hii utaikuta na kuungana na mikataba mingine mizuri yenye tija na maslahi mazuri zaidi kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea na kujaribu kujibu hoja za baadhi ya wajumbe sasa nijibu hoja za Idara ya Usafiri na Leseni. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Omar Ali Shehe na Mhe. Hija Hassan Hija walitaka kujua msimamo wa serikali katika kuimarisha Karakana Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Kuimarisha Karakana Kuu ni moja kati ya miradi iliyoahirishwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha kutokana na uhaba wa fedha na ndio maana haukutengewa fedha katika bajeti yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukieleza kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 imeipitia miradi mingi na kuangalia vipaumbele hasa kwa miradi ambayo itakuwa ina wafadhili. Ni imani yetu mradi huu bajeti ya mwakani *inshaallah* basi utaingizwa na naamini kwamba tutapatiwa fedha kwa ajili ya kuendeleza kwa kuuona umuhimu na mahitaji halisi ya kuwa na Karakana Kuu ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili hili pia Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu walitaka kujua sababu zilizopelekea kufungwa kwa barabara ya Forodhani pembezoni mwa Jumla la Kulelea Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, mji wa Zanzibar hasa Mji Mkongwe ni miongoni mwa miji michache iliyopata bahati ya kuwemo katika miji ya Urithi wa Kimataifa. Kwa Afrika inaungana na miji ya Lamu na Bagamoyo. Miongoni mwa masharti ya wenzetu wa *UNESCO* wameeleza wazi kwamba malengo makubwa ya miji hii ni kuhakikisha kwamba maeneo yale yanakuwa hayatumiwi na usafiri wa gari. Kwa maana ya kwamba maeneo hayo yanatumiwa kwa shughuli za matembezi ya miguu. Lakini kwa umuhimu na mahitaji yaliyopo Mji Mkongwe

inalazimika kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iombe ruhusa na uwezekano kwa kutumia magari katika eneo la Mji Mkongwe. Ruhusa hiyo inaendana na matakwa yale ya *UNESCO*.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kupunguza matumizi ya gari ili kuendana na hayo malengo na mahitaji ya *UNESCO* ya kupunguza matumizi ya gari katika eneo la Mji Mkongwe. Katika mikakati ya kupunguza matumizi hayo ya gari serikali inaona ni busara kutumia njia moja tu ya kuingia na kutoka Mji Mkongwe, ili pindi kama tutaendelea kutumia barabara zote mbili ile dhana na malengo ya *UNESCO* ya kupunguza matumizi ya gari katika eneo la Mji Mkongwe haitofikiwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana napenda nilikumbushe Baraza lako tukufu kwamba Baraza hili liliridhia na kupitisha *masterplan* ya Zanzibar. Miongoni mwa mambo ambayo yaliridhiwa na Baraza hili na kupitishwa ni kuthibitisha kwamba Mji Mkongwe ni *free traffic zone.* Kanuni hiyo ipo, mpango huo upo na umeidhinishwa na kupitishwa na Baraza lako hili tukufu. Kwa hivyo, kilichopo hivi sasa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni kusimamia hayo ambayo yamepitishwa na Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili pia Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kujua wizara yetu ina mpango gani wa kuandaa mipango na huduma mpya za usafiri hasa kwa maeneo ya mjini. Mhe. Mwenyekiti, wizara tayari ina mpango wa kuimarisha usafiri wa mjini kwa kuwaruhusu watu kuleta magari makubwa na ndio maana kuanzia sasa haturuhusu kusajili magari ya shamba. Isipokuwa kama tulivyoombwa na Baraza lako tukufu tutaendelea kuzitumia zile ambazo zilifanya kazi hadi zife wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako hili tukufu mwaka 2010 Waheshimiwa Wajumbe waliomba ni vyema kwamba magari hayo madogo yanayokusudiwa kupigwa marufuku kuingia katika eneo la mjini yaendelee kutumika hadi pale yatakapokufa basi magari mengine mapya yasisajiliwe kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, natumia fursa hii kuwaomba wawekezaji wetu na wafanyabiashara waingie hamu ya kuwekeza katika huduma ya usafiri na hasa mabasi makubwa. Mategemeo yetu kwamba tukipata wawekezaji watakaoweza kuwekeza kwa mabasi makubwa basi ile dhana na imani na malengo ya serikali ya kutaka kuboresha huduma hii yatafikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu walitaka kujua utaratibu wa uwekaji wa matuta katika maeneo. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 imeeleza wazi namna utaratibu wa uombaji kwa uwekaji wa huduma hizi za matuta pamoja na alama za *zebra*.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba tupeleke maombi yetu, vikao sita vitakaa na ni mategemeo yetu kwamba Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano hatokataa. Kwani maelezo na mahitaji ya kujenga matuta au kuweka *zebra* yamo kwa mujibu wa kanuni na sheria na hatuna uwezekano wa kukataa pale itakapokuwa vikao sita vimeelekeza na kutoa maoni yao kwamba kuna umuhimu na haja ya kufanya huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea pia Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa alitaka kujua kwa kiasi gani Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hufuata jukumu la ukaguzi kwenye *pole* kuwa katika mikono ya Jeshi la Polisi. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia tena Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 imetenganisha majukumu kati ya Jeshi la Polisi na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa upande wa Zanzibar kuhusiana na masuala ya usimamizi na uendelezaji wa vyombo vya usafiri. Jukumu la Wizara ya Miundombinu ni kuratibu na majukumu ya Jeshi la Polisi ni kusimamia na utekelezaji wa sheria hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saleh Nassor Juma alitaka kujua shughuli za udereva, mitihani kama ipo *temporary* na mambo mengine yanayohusiana na hilo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba skuli za udereva zinamilikiwa na watu binafsi, watu hao wanatoka katika kada tofauti, wamo wafanyakazi wa serikali, wamo wafanyakazi binafsi, wamo wafanyabiashara na wengineo. Hakuna kipingamizi kwa mfanyakazi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kumiliki skuli yake ya udereva.

Mhe. Mwenyekiti, katika skuli hizi utaratibu ni kwamba Idara ya Usafiri na Leseni inaandaa mitaala kwa skuli zote. Utendaji wa mitihani katika vyuo hivyo wanasimamia na kufanya wao wenyewe, lakini baada ya kukamilisha mitihani hiyo wahitimu na wanafunzi hao hutakiwa kwenda katika Idara ya Usafiri na Leseni ambapo hufanyiwa mitihani miwili, mmoja wa vitendo na mwengine wa maandishi. Kwa maana ya kwamba ili aweze kupata *certificate* na kukamilisha mafunzo yake basi ni pale baada ya kupata mitihani hiyo inayoratibiwa na kusimamiwa na Idara ya Usafiri na Leseni.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alisema kuwa Idara ya Usafiri na Leseni haina vitendea kazi ikiwemo gari hasa kwa upande wa Pemba. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikiri ni kweli kuwa Idara ya Usafiri na

Leseni hasa upande wa Pemba ina gari moja. Lakini pia kwa mashirikiano mazuri tuliyonayo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kila inapotokea haja au ulazima wa kuwe kuna gari, basi idara hii hupatiwa gari na Afisi Kuu Pemba ili kuweza kutekeleza majukumu iliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Omar Ali Shehe alitaka kujua matengenezo ya gari za SMZ katika Karakana Kuu ya Serikali yanaimarishwa. Mhe. Mwenyekiti, napenda tena nirejee kwa kusema kwamba suala la magari ya serikali kufanyiwa matengenezo katika Karakana Kuu ya Serikali ni suala liliopo kisheria. Naamini kwamba viongozi wote Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na watendaji wengine wanalitambua hilo.

Lakini Mhe. Mwneyekiti, lazima tukiri kwamba kwa muda huu karakana yetu ina mapungufu. Malengo yetu na makusudio yetu kuboresha karakana hii ili wenzetu hawa viongozi wa serikali waweze kutekeleza matakwa hayo ya sheria kwenda kufanya matengenezo hayo katika Karakana Kuu ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak alitaka kujua serikali imejipanga vipi kukabiliana na manyanyaso wanayoyapata walemavu na wanafunzi hasa kwa madereva na makondakta wa gari za daladala. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu tayari imeshaandaa kanuni za magari ya biashara ambapo itatoa kadi maalum kwa walemavu na wanafunzi ili waweze kuingia kwenye magari ya abiria kwa nauli tahfifu.

Wizara yangu pia kwa kutekeleza kanuni ya magari ya biashara imeweka masharti maalum kwa madereva na matingo wa magari ya abiria na yeyote atakayekwenda kinyume atakuwa ni mkosa. Kwa hivyo, dereva yoyote atakayemnyanyasa abiria ataripotiwa Polisi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe wito kwa wananchi wa Zanzibar kwamba yeyote yule atakayepata matatizo ya kunyanyaswa au kutendewa kinyume na taratibu apige ripoti katika Kituo cha Polisi au amtafute Afisa wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili kufikisha malalamiko hayo. Sisi tunamuahidi tutahakikisha kwamba aliyefanya utovu huo wa nidhamu anachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria na taratibu ziliopo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea na hilo Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa alitaka kujua utaratibu wa nauli za abiria na makondakta na madereva kuvaa sare zao. Mhe. Mwenyekiti, suala la sare kwa madereva na makondakta wao tayari tumeshalitolea utaratibu kwa hiyo tunachosisitiza kwamba madereva na makondakta wafuate utaratibu huo. Sisi kama Wizara ya Miundombinu na

Mawasiliano tunaosimamia tutahakikisha eneo hili nalo tunakaza kamba ili kuona maelekezo yetu hayo yanafanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mussa Khamis Silima alitaka kujua taratibu za leseni kwa madereva. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kupata leseni kwa msingi wa umri unalingana na ngazi au *division* ya leseni yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, kuna leseni karibu *division* 5, kuna leseni ya *grade E, A, B, B 1, C* na *C 1*.

Kwa mujibu wa sheria yetu kijana mwenye umri wa miaka 18 anaruhusika kuwa na leseni ambayo itamruhusu kuendesha vyombo vya maringi mawili ikiwemo kiciao, pikipiki na vespa. Hivyo basi, naomba nimtoe shaka Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba vijana ambao wana umri huo wa miaka 18 kumiliki kwao leseni hakujawa kinyume kwa mujibu wa sheria. Wale vijana ambao watakuwa na umri wa miaka 21 wanaruhusiwa kwa mujibu wa sheria hiyo kuwa na leseni za magari yale ya nyumbani *(private hire)*. Pia atakayekuwa amepata leseni na kuwa na uzoefu usiopungua miaka mitano na atakuwa na umri wa zaidi ya miaka 25, basi anaruhusika kuwa na leseni kwa magari ya abiria, kwa maana ya kwamba grade *C* na *C 1*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea na hoja sasa naingia katika Mamlaka ya Usafiri Baharini. Mhe. Mwenyekiti, katika mamlaka hii Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alitaka kujua kwa nini safari za boti hazina mpangilio na kwa nini boti zinachelewa kuondoka kufika eneo lililokusudiwa. Pia alitaka kujua kama meli zinakaguliwa na kwa nini zinakuwa chafu hasa maeneo ya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, safari za boti zina ratiba zake ambazo zimeridhiwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini. Boti au meli ni kama vyombo vyengine huweza kupatwa na matatizo ya kiufundi ambayo huweza kutokezea hata zikiwa katika safari zake. Hali ya bahari nayo pia huchangia kwa kiwango kikubwa kuongeza au kupunguza kwa mwendo kwa meli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba Mamlaka ya Usafiri Baharini imekuwa ikivikagua vyombo hivyo vyote na kuviridhia baada ya kuridhika kwa mujibu wa taratibu na sheria kwamba chombo hicho kimekidhi matakwa ya sheria, hakina matatizo ndio kinapatiwa ruhusa ya kufanya safari zake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa usafi jukumu hili linasimamiwa na wenzetu wa Wizara ya Afya kuwatuma maafisa wao wa afya kwenda kuzikagua meli hizo na wanaporidhika na usafi uliomo ndani huwa kwetu hakuna kipingamizi.
Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kujua kwa nini Zanzibar tusifikirie kuwa na mpango wa *club of conveyance* kwa ajili ya kuongeza

mapato na kwa nini Zanzibar isiweze kutumia *club* yake kama *club of conveyance.*

Mhe. Mwenyekiti, katika mamlaka hii Zanzibar tayari inayo *club of conveyance* ambayo iko chini ya sheria ya *Maritime Transport Act No. 5* ya mwaka 2006 ambayo inajulikana kama ni *Tanzania Zanzibar International Registers Shipping.* Taarifa rasmi ya suala hilo iko kwenye kitabu cha bajeti cha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ukurasa wa 30 kifungu cha 81.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na Zanzibar kutumia *club* yake kama *club of conveyance* kwa muda huu bado tunaendelea kutumia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hija Hassan Hija anauliza kwa nini wafanyakazi wa meli wa *Seagull* hawana mikataba. Mhe. Mwenyekiti, sheria ya *Maritime Transport Act* inawataka wamiliki wote wa meli lazima wafunge mikataba na mabaharia wao. Mhe. Mwenyekiti, tatizo liliopo ni tatizo la pande mbili.

Sote tunatambua matatizo ya ajira yaliyopo nchini kwetu na mahitaji ya vibarua. Wamiliki wengi wa meli wamekuwa wakitumia udhaifu huo kuwahadaa vijana wetu kuwaingiza katika ajira kwa kisingizio cha kutokuwapa mikataba. Utaratibu huo ni kinyume na sheria na tunawaomba wale wote ambao watakuwa wameingizwa kazini katika makampuni haya ya meli bila ya kupewa mikataba waje waripoti katika mamlaka husika na sisi tunawaahidi kwamba mamlaka hii itawachukulia hatua.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka hii tayari imeshaanza kuchukua hatua kwa mifano ya watu ambao walikuja kuripoti matatizo haya, miongoni mwao ni meli ya *MV Sepideh* iliwahi kutokewa na tatizo hili mabaharia hao wakaja katika mamlaka husika na mamlaka ikachukua hatua.

Hivyo basi, biashara hii iko kama rushwa, pande mbili hizi zinakuwa zimekubaliana, wasisubiri kwenye matatizo ndio wakawa wanasema. Tokea awali wanapoingia kwenye ajira hizi tunawaomba sana vijana wetu hawa wafike mamlaka husika kutoa taarifa hizo ili mamlaka iweze kutekeleza utaratibu kwa mujibu wa sheria ya *Maritime Authority* kama inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rufai Said Rufai anauliza kwa nini usafiri wa baharini ni mbovu na abiria wanachukuliwa kama mizigo. Suala jengine ni kuwa kwa nini tiketi haziuzwi kwenye ofisi za meli badala yake zinauzwa majiani na vibandani. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kila meli inayo ofisi yake inayouza tiketi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, lazima tukiri kwamba kuna tatizo aidha katika

uongozi wa kampuni au wafanyakazi wanaouza tiketi wanashirikiana na walanguzi katika kutoa tiketi zile.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu uko wazi kwamba ili uweze kupata tiketi ni lazima uende na kitambulisho aidha cha Mzanzibari Mkaazi au barua nyengine yoyote inayoweza kukutambua kwamba wewe ndio mhusika unayetaka tiketi hiyo. Jambo la kushangaza ni kwamba wanakwenda watu anapewa tiketi zaidi ya mbili mpaka 50, mtu huyo mnamjua wazi ni mlanguzi, anakwenda kuwauzia watu kwa bei maradufu ya ile bei iliyohalalishwa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba sisi Mamlaka ya Usafiri Baharini tatizo hilo tumeliona na tunajiandaa kwa kushirikiana na wamiliki wa makampuni hayo kuliondoa tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa meli kama nilivyokwisha kueleza kwamba meli zote zinazofanya safari ni meli salama ambazo zimethibitishwa na mamlaka hii baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kina na kuonekana kwamba hazina tatizo. Pale linapotokea tatizo basi mamlaka hii na wizara huwa haisiti kuizuia meli hiyo kuendelea na safari.

Mhe. Mwenyekiti, hata meli yetu ya MV. Maendeleo tumekuwa tukiizuia isiendelee na safari pale linapotekezea tatizo hadi ifanyiwe matengenezo na kukidhi mahitaji na matakwa kwa mujibu wa kanuni na sheria za usimamizi wa usalama baharini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Asha Bakari Makame aliuliza pia suala la tiketi, hili nimekwisha kulieleza matatizo yake yako hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Assaa Othman Hamad aliuliza kwa nini abiria hukatishwa tiketi na wanapofika bandarini huambiwa kuwa meli au boti zimejaa. Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili linarudi kule kule kwa maana ya kwamba aidha wamiliki au wafanyakazi wao hawako makini na wao ndio wanaochangia tatizo hili. Hawa watu walanguzi wanapewa tiketi na hawa na hakuna udhibiti. Lakini sisi kama mamlaka tunaomba mtupe imani na tutahakikisha kwamba tatizo hili linapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Assaa Othman Hamad pia alitaka kujua kwamba je, Mamlaka ya Usafiri ina vyombo vya kufuatilia vyombo vya kigeni vinavyoingia katika maeneo ya bahari yetu kwani baadhi yao wanaifanya kama shamba la bibi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa mamlaka hatuna lakini imani yetu kwamba ulinzi wa mipaka hii uko chini ya vikosi vya ulinzi na usalama na matarajio yetu kwamba vikosi hivi vinafanya kazi vizuri kwa ulinzi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Ali Salum Haji walitaka kujua suala la doza la Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kufanya kazi katika chelezo cha mfanyabiashara huko Bumbwini. Mhe. Mwenyekiti, naomba nilieleze Baraza lako tukufu kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wakati huo ikimiliki doza hilo. Doza hilo lilikuwepo Pemba na ni kwa muda mrefu tokea mwaka 1994 lilikuwa limelala kutokana na kuharibika kwake.
Mhe. Mwenyekiti, tayari walikuwa wametokea watu wengi ambao waliomba kuuziwa doza hili, lakini busara zilitumika kuona kwamba doza hili haliuzwi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kushirikiana na mwekezaji huyu walikubaliana kwamba mwekezaji alichukue doza hilo kwa ajili ya kulikarabati na baada ya kupona wizara itakwenda kulikagua, fidia ya ukarabati huo ataitumia kwa kazi ambayo atakayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, doza hilo lilipona likafanya kazi kwa muda mchache likaharibika tena. Hadi muda huu Mhe. Mwenyekiti, doza hilo bado ni bovu na malengo na madhumuni ya wizara chini ya usimamizi wa Idara ya UUB tukenda kulichukua na kulirejesha katika makao makuu ya UUB Saateni.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Hamza Hassan Juma alihoji namna gani Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imehaulisha kiwanja. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa wakati huo ilikuwa ikimiliki kiwanja namba 181 kilichokuwepo eneo la Maruhubi. Malengo ya kiwanja hicho ilikuwa ni kujenga ofisi ya kudumu ya makao makuu ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunatambua harakati na shughuli zinazoendelea katika eneo hilo. Hivyo basi, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iliomba kupatiwa kiwanja chengine kwani isingekuwa vyema na busara kwenda kujenga ofisi katika eneo hilo. Baada ya kupatiwa eneo jengine Mazizini, wizara iliomba ruhusa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kukihaulisha kiwanja hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kiwanja hicho hakikuhaulishwa kiholela, taratibu zimefuatwa likiwemo suala la kuomba idhini kutoka serikali kuu, serikali kuu ikaridhia ikaja kwetu na serikali kuu ikaiomba Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa wakati huo ihaulishe kiwanja hicho kwenda kwa huyo mlengwa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika uhaulishaji huo kwa kuwa kulikuwa tayari kuna maendeleo ambayo yalikuwa yamefanyika kwa makubaliano na mkataba wetu na mwekezaji huyo kwamba atatusaidia fedha za ujenzi katika jengo letu jipya tunalotarajia kujenga eneo la Mazizini.

Mhe. Mwenyekiti, kiasi cha fedha shilingi milioni 200 kipo katika mikono salama na tutakapokihitaji kwa ajili ya kuanza ujenzi katika jengo letu jipya la Mazizini kitapatikana. Mhe. Mwenyekiti, naomba nilithibitishie Baraza lako tukufu kwamba uhaulishaji huu haukuwa uhaulishaji wa kiholela, ulifuata taratibu zote za kisheria kama nilivyoeleza katika maelezo yangu.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wengi waliendelea kuchangia hasa suala la Shirika la Meli kuona serikali ina mkakati gani katika upatikanaji wa meli mpya kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inaendelea kufanya juhudi kubwa kusaidia upatikanaji wa vyombo vyengine vya baharini na mazungumzo yanaendelea na wawekezaji mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kuna karibu makampuni manne yanaendelea na mjadala huu, kampuni ya Italy imeshaonesha nia hiyo ya kutusaidia na wanategemea kufika Zanzibar mwishoni mwa mwezi huu wa Julai kwa ajili ya maendelezo ya mazungumzo tuliyoyaanzisha.

Mhe. Mwenyekiti, kampuni hii itakutana na wataalam kwa kuendelea kushauriana nasi kwamba hiyo Kampuni ya Uturuki ya uwekezaji ambao nao tayari wameonesha nia hiyo, Kampuni ya *Fazah Cooperation Ink* ya *England* nayo imeonesha nia hiyo, Kampuni ya *MTKA* ya Abudhabi nayo imeonesha nia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, makampuni hayo yote yameonesha nia ya kutaka kuja kuwekeza katika eneo hili. Mazungumzo yetu tunayoendelea nayo ni namna ya uwekezaji. Aidha, mazungumzo yetu kwanza tunakusudia kuwahamasisha kuja kuwekeza kwa maana ya kwamba serikali kupata hisa katika meli hizo au ikiwezekana basi watukopeshe hata kwa njia ya mkopo.

Mhe. Mwenyekiti, ni mategemeo yetu kwamba wawekezaji hawa ni makampuni ambayo yana nia nzuri, tupeni muda tuendelee kuzungumza nao. Matarajio yetu ni kwamba tukifikia mazungumzo mazuri tutaiarifu serikali na Baraza lako tukufu litapata taarifa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe pia walitaka kujua kuhusu suala la MV Maendeleo kuendelea kuharibika, ilipoharibika na kuzuiliwa halafu inaendelea na safari. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba meli ni kama chombo chengine, kinafanya safari zake. Wakati wa safari inapopata hitilafu mamlaka husika inakizuia baada ya kukamilisha hitilafu hizo mamlaka husika haina sababu ya kuzuia. Kwa msingi huo ndio iliyopelekea meli ya MV Maendeleo kuzuiliwa baada ya kwenda kwenye matengenezo na kurudi, mamlaka husika baada ya kuridhika na uchunguzi wao na kuona kuwa marekebisho yale yamekidhi haya haikuwa na sababu na hivyo ikaruhusiwa ikaendelea na shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Jaku alitaka kujua kwamba Shirika la Meli limefikia wapi suala lake la deni linalodaiwa na Kampuni ya *Mkunazini Shipping Cooperation*. Mhe. Mwenyekiti, suala hili lipo mahakamani na naomba sana isingekuwa busara kuendelea kulizungumza hapa hadi hapo maamuzi ya mahakama yatakapofikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kujaribu kujibu hoja hizo, basi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chwaka, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Muumba Mbingu na Ardhi, Mnemeshaji wa Neema ndogo ndogo na kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka niwatambuwe, niwashukuru na niwapongeze wajumbe wako wote ambao wamechangia hotuba hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wajumbe wako wamekubali ombi letu la kuipokea, kuijadili na naamini baada ya wajumbe kupata ufafanuzi wa majibu na hoja na maswali mbali mbali, basi wataipitisha bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba wajumbe wametuuliza, wametuhoji, wametushauri, wametuelekeza, wametukosoa lakini zaidi wametusaidia mno na wamefanya yote haya kwa nia moja tu ya kutuimarisha. Mapungufu yaliyojitokeza katika hotuba hii na katika utendaji wote wa wizara hii Mhe. Mwenyekiti wajumbe wako wameyaonesha katika kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwahakikishie wajumbe wako wa Baraza hili tukufu kwamba yote waliyotueleza ni mambo muhimu, ya msingi na ni hali halisi ilivyo na tutayafanyia kazi mara tu bajeti hii watakapoipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, mtu pekee haoni mwezi na ndio maana hatuko Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano peke yetu hapa leo. Baraza zima la Wawakilishi la Zanzibar liko hapa. Uwezo wa Baraza hili ni mkubwa sana, ndilo linalowawakilisha watu wote wa Zanzibar. Kwa hivyo, hapa ndipo mahali sahihi ambapo wawakilishi wanalazimika kusema kila ambalo wanaona linafaa kusemwa.

Muhimu pia ni kwa wajumbe wako wa Baraza lako tukufu kuhusu jinsi ya kuwasiliana na wananchi wao. Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wako 50 wa Baraza hili wamechaguliwa majimboni na 20 wamechaguliwa kwa nafasi maalum za wanawake. Wote hawa wanapenda kuridhisha wapiga kura wao, naomba wenzangu hawa na mimi nikiwa miongoni mwao kuwafurahisha wananchi kwa taarifa ambazo sio sahihi zina matatizo yake. Kwa hivyo, ni vyema wananchi wetu wapiga kura wetu tuwaambie ukweli ulivyo.

Mhe. Mwenyekiti, matumaini ya Wazanzibari katika Serikali ya Awamu ya Saba ni makubwa mno, hasa katika Wizara kama hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Wananchi Wazanzibari matumaini yaoni kuona kwamba wana usafiri wa anga unaoridhisha, wanapata usafiri wa baharini mwepesi ambao kila mnyonge ataumudu na wa uhakika. Wazanzibari hawa hawa matumainio yao makubwa ni kuona bandari yetu ndio uti wa mgongo, bila bandari hakuna mchele, hakuna sukari, hakuna nguo na hakuna vifaa vya ujenzi utaviletaji kwa ndege, vitanunulika. Kwa hivyo, wananchi wanataka kuona bandari yao ni muhimu ipo na kila siku ina imarika na kukua.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wanataka kuona kwamba kiwanja chao cha ndege au viwanja vyao vya ndege kila siku vinapanda hadhi, vinavutia ili kuvutia wageni zaidi waje kuona. Kuja kwa wageni zaidi ni *promotion* ya kuitangaza Zanzibar duniani.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni matumaini makubwa waliyonayo Wazanzibar. Wizara hii ndio iliyobebeshwa chano. Mhe. Mwenyekiti, katika vilinge wako wanaodai vyano, ng'ombe, mbuzi, kuku hawadai nguruwe, hawadai punda kwa sababu hawaliwi hao. Wanadai ndizi mbivu, halua, tende, mayungiyungi na mikate ya tope. Vyote hivyo hutiwa kwenye chano. Halafu hutishwa mtu chano kile akakiweke njia panda, anayeliwa na jini ni yule anayetwikwa chano, siye anayepanga chano.

Kwa hivyo, majukumu haya yote ninayozungumza, usafiri, bandari, madaladala na barabara zetu wanaotwishwa chano ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa hivyo, sisi kuliwa na jini ndio stahili yetu. Mhe. Mwenyekiti, nataka niwashukuru kwa Kiingereza wanaitwa *backbenchers*, wajumbe wako wa viti vya nyuma. Mimi ningeshangaa mno kama wajumbe hawa katika wizara hii hawangechangia hivi walivyochangia.

Hapa ndipo mahali pake hakuna pengine, hayo uliyoyasema hapa ukiyasema Darajani hujasema kitu, haya ukiyasema kwenye mikutano yako ya ndani iwe ya chama iwe ya chochote basi hujasema kitu, hapa ndipo panaposemwa na hapa ndipo panapotolewa maamuzi. Nawapongeza mno.

Mhe. Mwenyekiti, katika michango mbali mbali tumepongezwa, tumesifiwa, tumeombewa dua na wengi tu waliochangia. Lakini furaha yangu mimi na watendaji wote wa wizara hii ya pongezi hizo na sifa hizo ni furaha hiyo hiyo kwa lawama, namna tulivyokosolewa, tulivyoelekezwa na tulivyosaidiwa vina uzito mmoja. Kwa hivyo, niwatoe hofu mimi ndiye ninayejenga barabara, hata kama umesema umechangia kwa *style* yoyote unayojua, kwangu mimi ni faraja. Nitatenda haki sawa kwa wote, lakini sitatenda haki sawa sawa kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, narudia. Nitatenda haki sawa kwa wote, lakini sitatenda haki sawa sawa kwa wote. Kama Mhe. Abdi Mosi nimemjengea barabara ya kilomita 11, basi na zile mita 600 za Kwahani, kilomita 11 na mita 600 sio sawa sawa. Lakini ukimjengea wa Kwahani na ukimjengea na Mhe. Abdi Mosi basi umewapa haki sawa. Naitafsiri.

Mhe. Mwenyekiti, lazima nikiri Baraza limenisaidia mno kupita kiasi. Hii mimi naitafsiri ndio kutafsiri Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa vitendo. *Backbenchers* tunawajua *they are very strong*, lakini *the cabinet is the strongest*. Ndivyo tunavyotakiwa tuwe na waheshimiwa. *Backbenchers* na *cabinet* likiwa lao moja haku, basi hakuna vita vyovyote ambavyo hatutoshinda. Sio vita vya OIC, sio vita vya Muungano, sio vita vya kero za Muungano, hakuna vita ambavyo tutashindwa. Humu tunaelekezana tunakosoana na tunashauriana lakini letu hili moja. Hata tukitoka humu bado letu ni moja. Hii ndio tafsiri ya (*GNU)*, yaani *Government of National Unity*. Mwanzo mwanzo tulipondwa serikali hii wanajidai tu, haifiki hata mieizi mitatu. Basi itafika hata miaka mia tatu *Inshaallah*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kumshukuru Mhe. Machano Othman Said. Mimi nimempokea kijiti hizi ni mbio za *relay* unachukua unafika mahali unampa mwenzako. Yule ambayo umempokea yeye anashangilia, aapizi kwamba yule niliyempa kwa nini haanguki. Amekuwa akinisaidia sana,

anatumia uzoefu wake, hata pale ambapo sijamwita anakuja na kuniambia kuna moja, mbili na tatu. Namshukuru sana na nampongeza sana. Ushahidi wa haya ni huu mchango wake wa leo.

Mhe. Mwenyekiti, Naibu Waziri wangu, mimi namwita kamanda. Kama utamchukua matu asiyejua kuwa huyu ni CUF au huyu ni CCM ukaja katika vikao vyetu baada ya kikao ukamuuliza mtu huyo, unaonaje kikao hiki. Basi atakuambia watu wote hao ni wa chama kimoja. Namshukuru Naibu Waziri wangu, mimi na yeye tumekubaliana siasa nje katika utekelezaji wa shughuli za serikali. Siwafichi, nilipoingia katika wizara hii mazoea yanatabu, watendaji wengi hawakuwa na *confidence* na mimi, walikuwa wananiogopa. Kwa sababu walijazwa fikra za kiajabu ajabu, niko pale kama polisi natafuta nani kafanya kosa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, baada ya muda wale ambao wakinisinzilia, yalikuwepo hayo si nilikuwa nayaona mwenyewe. Pamoja na fitina ambazo nikitiwa, *secretary* wako yule ni mtu wa Donge, mkereketwa, usikubali kupewa chai atakuuwa. Karani wako yule muogope kweli kweli, Katibu Mkuu wako ni mtu mbaya sana. Lakini Waheshimiwa Wajumbe, nawaambieni tena, nikasema mimi liwe litakalokuwa Mwenyezi Mungu mbele. Tumefanya kazi na sasa hivi *Alhamdulillah Rabil Alamina*.

Mhe. Mwenyekiti, katika Waheshimiwa Wajumbe waliochangia naomba niwataje hapa ni 45. Wajumbe 37 wamepongeza utendaji wetu wa wizara. Sasa hebu wewe sema 37 katika 45 ni asilimia ngapi. Nashukuru sana tena sana. Mimi nasema haya naomba munivumilie. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, mkuu wa shughuli za serikali nayasema haya mchana, sioti na nina akili zangu timamu, nashauri sana kama kuna wizara bado watu wanaogopana, watu wanapigana majungu, basi wakati huo umeshapita. Viti hivi vya uwaziri hatukuwa navyo, leo tunavyo na kesho hatutokuwa navyo ukitaka usitake. Lazima tufanye kazi kwa ari hiyo.

Leo Mhe. Machano Othman akiingia ofisini pale utafikiri tumeingia pamoja. Hakuna tofauti na alivyokuwa waziri, huu ndio mfano kila mtu ni rafiki yake na kila mtu anacheka naye. Nawaombeni mawaziri wenzangu tujenge tabia hiyo, ndipo ambapo tutaweza kufanya kazi kwa pamoja na ndipo ambapo *GNU* itakapopata sifa na wengine wakaiga.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitowe maelezo juu ya mambo ambayo yanahitajika kutolewa ufafanuzi. Napenda nitamke kwamba hotuba ya wizara yangu imechangiwa na wajumbe wako 45 naomba niwataje. Katika hao wajumbe 45 wajumbe 28 wamechangia, na wengine wanaleta sasa hivi. Wajumbe 28

wamechangia katika Baraza hili kwa kusema baada ya kupewa ruhusa ya Spika au Mwenyekiti. Waliochangia kwa maandishi ni wajumbe 17, kwa hivyo 28 na 17 ni wajumbe 45 hesabu ya darasa la pili.

Wajumbe waliochangia hotuba yetu kwa ruhusa ya Spika au Mwenyekiti ni hawa wafuatao:

1. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
2. Mhe Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
4. Mhe. Raya Suleiman Hamad
5. Mhe. Hija Hassan Hija
6. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
7. Mhe. Mgeni Hassan Juma
8. Mhe. Rufai Said Rufai
9. Mhe. Nassor Nassor Juma
10. Mhe. Asha Bakar Makame
11. Mhe. Hamza Hassan Juma
12. Mhe. Farida Amour Mohammed
13. Mhe. Omar Ali Shehe
14. Mhe. Assa Othman Hamad
15. Mhe. Abdi Mosi Kombo
16. Mhe. Mohammed Haji Khalid
17. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
18. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
19. Mhe. Hassan Hamad Omar
20. Mhe. Ali Salim Haji
21. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
22. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
23. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
24. Mhe. Jaku Hashim Ayuob
25. Mhe. Subeit Khamis Faki
26. Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi. Pia alichangia kwa maandishi.
27. Mhe. Machano Othman Said
28. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, waliochangia kwa maandishi nawashukuru sana, maandishi yalikuwa mafupi, lakini yalieleza kila kitu ambacho walitaka kueleza nao ni:

1. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla

3. Mhe. Nassor Salim Ali
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
5. Mhe. Mussa Khamis Silima
6. Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi
7. Mhe. Asha Abdu Haji
8. Mhe. Salim Abdalla Hamad
9. Mhe. Kazija Khamis Kona
10. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
11. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
12. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
13. Mhe. Amind Iddi Mabrouk
14. Mhe. Panya Ali Abdalla
15. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
16. Mhe. Mussa Ali Hassan
17. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni binadamu na nina mapungufu yangu, naomba radhi kama kuna yeyote ambaye sikumtaja ni mapungufu ya kibinadamu. Sijakusudia wala sijadhamiria.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nichukuwe muda wako mrefu

UTARATIBU

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kama ingekuwa ni mimi peke yangu radhi ingenitosha, lakini Mhe. Waziri ameiwacha kamati nzima na ripoti yake. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nimetanguliza kuomba radhi. Yale mambo muhimu hata pengine kuliko mambo mengine unaweza ukayasahau. Naomba radhi na nataka nitamke kwamba miongoni mwa waliochangia ni Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano na Ujenzi. Vile vile na Mhe. Rashid Seif Suleiman ambaye ni Makamo Mwenyekiti. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, pia nakushukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze na sitaki nirudie yale ambayo Naibu Waziri na Mhe. Machano Othman ameyazungumza au yamezungumzwa na mtu mwengine yeyote ambaye amejibu hoja ambazo wajumbe wamezileta. Nitajitahidi kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na deni la *ATC* kulipwa haraka. Mhe. Mwenyekiti, wizara inakubali kuwa deni hili lipo na serikali inalitambua. Kwa hivyo, *ATC* hivi sasa iko chini ya Wizara ya Uchukuzi ya Serikali ya Muungano wa Tanzania. Hivyo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya Zanzibar na Wizara ya Uchukuzi ya Serikali ya Muungano wa Tanzania zimekubaliana kulitatua tatizo hili kwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na kikao cha mashirikiano cha Wizara hizi mbili. Moja katika *agenda* ni deni la *TAC*. Kwa hivyo, tumekubaliana na hivi sasa tunafanya *procedure* hizo ambazo tulizokubaliana, ili deni hili lilipwe. *(Makofi)*

Ujenzi wa jengo jipya la abiria usimamiwe vizuri. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii tunaichukua na nimesema kwamba tumeelekezwa, tumekosolewa, tumeshauriwa, tumeongozwa kwa hivyo mengine mengi tutayachukua, kwa ajili ya kuyafanyia kazi. Kwa hivyo, na pale ambapo tumekosea basi tutasema kwamba hapa kuna kosa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hii tunaichukua na tutaifanyiakazi. Lakini pia katika kutekeleza hilo serikali imeajiri Mshauri Mwelekezi Kampuni ya *ATN* ya Turkey kusimamia ujenzi huu. Kwa hivyo, usimamizi wa ujenzi ule serikali imeajiri, kwa maana hiyo unaangaliwa vizuri, yaani *very close supervision*.

Hoja ya Uwanja wa Ndege Pemba kutowekewa fedha za kuuimarisha. Mhe. Mwenyekiti, fedha za kuimarisha Uwanja wa Ndege Pemba zimeingizwa katika kifungu cha Uimarisha Viwanja vya Ndege Zanzibar, ambavyo vimepangiwa shilingi milioni 300/=. Vile vile wizara inafuatilia bakaa ya bola za Kimarekani laki 340 zilizobakia wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Uwanja wa Ndege Pemba chini ya Ufadhili wa *Saudi Fund*, ili ziweze kutumika kwa ajili ya kuimarisha Uwanja wa Ndege Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia wizara kwa kushirikiana na Jumuia ya Afrika ya Mashariki tunafuatilia kwa karibu sana uwezekano wa kupata ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *ADB*, ili kuendeleza juhudi za kuimarisha Uwanja wa Ndege Pemba. Kwa hivyo, mule haikutajwa *specifically* kwamba Pemba, lakini fungu hili liko katika Uimarishaji wa Viwanja vya Ndege Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya uanzishwaji wa Chuo cha Ubaharia Zanzibar haikuekewa bajeti. Idara ya Mipango imewekewa bajeti ya kusimamia shughuli zote za kuratibu tu, fedha za uendelezaji shughuli za Uazishwaji Vyuo vya Mabaharia na kile cha Marubani, zitatoka katika Mfuko wa *Maritime Authority* na *Airport Authority*, ikisaidiwa na Idara ya Mipango kupata fedha kutoka Wahisani wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mamlaka moja tayari imeshaundwa inafanyakazi na nyengine inafanayakazi zake na *Inshaallah* baada ya Baraza hili au bajeti hii, basi sheria itakuja hapa. Kwa hivyo, tunaamini kwamba hawa wataweza kutoa fedha kwa ajili ya kila *authority* kushughulikia uazishwaji wa chuo chake.

Hoja ya Chelezo cha Mwekezaji wa Kizalendo huko Mwangapwani Bumbwini. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano zimeshaiandikia Shirika la Bandari kufuatilia eneo linalopendekezwa kwa ujenzi huu na pia kuwaandikia *ZIPA* kupata maelezo juu ya mradi yaliyowasilishwa kwetu na mwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya *ZIPA* ni kwamba mradi huu ni mzuri, lakini mwekezaji anatakiwa kufuata taratibu za kupata idhini kutoka taasisi husika.

Aidha ada ya kupata kupata maelezo kamili kutoka taasisi husika, yaani *ZIPA* na Shirika la Bandari kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu itatoa maelekezo juu ya maombi haya kulingana na mipango ya wizara juu ya shughuli hizi za *Dry Dock* hapo Bumbwini. Pamoja na maelezo hayo, mradi huu utatolewa maamuzi ya utekelezaji na Wizara ya Fedha kupitia *ZIPA* na wizara yetu ni mshauri tu. *(Makofi)*

Hoja ya fedha za bajeti za kufanya utafiti katika Idara ya Mipango. Mhe. Mwenyekiti, shughuli za utafiti katika Idara ya Mipango zinafanywa baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano (SMZ) na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Kwa hivyo, fedha hizi hutolewa na wahisani wa Maendeleo na hivyo ziko fedha nyingi zilizotengwa kwa kazi hii. Mhe. Mwenyekiti, wizara imetakiwa kupeleka maombi ya vielelezo vya maeneo ya utafiti, ili kupata ufadhili wa fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *research* limekuwa *centralized*. Kwa hivyo, wizara zote kama wanataka kufanya utafiti, basi fedha ziko na zimekuwa *centralized* na zitakuwa *coordinated* na wizara hizi mbili, yaani ile ya SMT na SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya huduma za *Internet*. Kwa kweli fedha zilizotengwa kwa matumizi ya huduma ya mawasiliano ya *Internet* ya shilingi milioni 1,000,000/= kwa matumizi ya *Internet* ya Makao Makuu ya Wizara tu, masuala ya uratibu wa *Internet* kama mawasiliano hapa Zanzibar yameekewa bajeti yake katika Idara ya Mawasiliano. *(Makofi)*

Hoja ya mikataba mikubwa ya Miradi ya Maendeleo na Uratibu wake. Mhe. Mwenyekiti, mikataba mikubwa mara nyingi inafuata masharti na vigezo vya wahisani, yaani *Standard Format of Contracts*. Kwa hivyo, jukumu la wizara ni kuratibu miradi hii kwa kushirikiana na Washauri Waelekezi pamoja na Wakandarasi. Vile vile wizara inateua Mwakilishi wake *Project Coordinator* anayeiwakilisha wizara katika mradi huu. Kwa maana hiyo, kila mradi wizara inatoa *Project Coordinator* kuhakikisha na sisi pale kama wenyewe tunashuhudia kinachofanyika hata kama mradi ule umefadhiliwa na *donor*.

Hoja ya Ujenzi wa Bandari Mpya ya Mpigaduri Unguja. Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kushirikiana na wafadhili Serikali ya Watu wa China imo katika ukamilishaji wa upembuzi yakinifu, yaani *feasibility study* ya mradi huu, ili hatimaye iwasilishwe kwa wahisani kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa bandari hii.

Mhe. Mwenyekiti, imechukua muda mrefu, lakini ni bora uende polepole lakini uwe na hakika ya unachokifanya na hicho kimefanyika. Kwa mfano, *study* iliyofanywa mwanzo haikutosha na tukasema ifanywe tena au iongezwe tena, ili kukidhi haja ya bandari tunayoitaka. Kwa hivyo, hiyo *study* hivi sasa imemalizika na kinachofanywa sasa ni *process* ya maombi ya fedha kutokana na hii study ambayo imefanywa.

Mhe. Mwenyekiti, *study* hii wamefanya ndugu zetu wa China na hao ndio ambao wako mbele katika kuhakikisha kwamba tunapata mkopo huu kutoka *Exim Bank*, kama ambavyo tulivyopata mkopo kwa ajili ya jengo la abiria katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume.

Hoja ya ununuzi wa meli mpya kwa Shirika la Meli la Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa ikifanya mazungumzo na mashirika mbali mbali binafsi katika kuwashajihisha uwekezaji wa Sekta hii ya Usafiri wa Meli. Hivi sasa serikali imo katika mazungumzo na makampuni matatu, kampuni hizo zimeonesha kuwa na nia ya kushirikiana na Shirikali la Meli kwa njia ya mkopo nafuu *higher purchase* au mashirikiano ya pamoja *joint venture*.

Kwa hivyo, tumeagizwa na Serikali Kuu tufufue shirika kwa kupata meli nyengine na uwezekano wa kununua meli kwa dola milioni 25 serikali waliuona kwa sasa na mgumu. Kwa maana hiyo, wizara inafanya juhudi zote na haya makampuni matatu ndio ambayo yamesema yanakuja, lakini kuna nyengine zimeonesha kwamba zinakuja. Sasa atakayekuja na kukubaliana naye, basi ndiye huyo ambaye tutakayekwenda naye na baada na hapo ndipo tutakapolipeleka kwenye Serikali Kuu kwa taarifa pamoja na maamuzi ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya matumizi ya fedha za ujenzi wa ofisi. Kweli fedha hizo shilingi milioni 100/= zilitengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Sasa fedha zilizotumika ni sahihi shilingi milioni 49/= nazo zilitumika kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii kabla haijakuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilikuwa imo katika jengo la Nyumba za Mji Mkongwe. Mhe. Mwenyekiti, nyumba ile tunakumbuka wakati mmoja dari yote iling'oka ikaanguka juu ya dari nyengine kwa bahati nzuri hapakuwa na mtu, lakini kama pangekuwa na watu basi hivi sasa wangekuwa marehemu. Kwa kweli nyumba nyingi za Mji Mkongwe ni mbovu tena zina hali mbaya.

Kwa hivyo, baada ya Mji Mkongwe kutushauri kwamba hali ni mbaya na sisi tuliona, basi tulitumia shilingi milioni 15/= katika 49/=, ili kulifanyia marekebisho angalau kuacha nafasi ndogo na wengine wabakie mule, lakini wengine wote tulihama. Kwa mfano, mimi mwenyewe Waziri nilihama, Katibu Mkuu wangu pia na pale iliyobakia ni idara moja.

Sasa tukahamia wapi, Mhe. Mwenyekiti mtakumbuka kwamba kuna ghala na zamani ilikuwa ni *Government Stores*, sisi tumo mle na lile ni ghala liko wazi, hivyo ikabidi tufanye ukarabati kwa sababu vyenginevyo tungekwenda wapi? Hatuna pa kwenda.

Kwa hiyo, katika shilingi milioni 49/=, shilingi milioni 15/= zimetumika hapo na shilingi milioni 34/= tumefanyia ukarabati na unaendelea lakini tumo humo humo, wakati wanapokuja mafundi basi unatoka na wanapotoka unaingia angalau tupate mahala, haya ndio maelezo sahihi ambayo naweza kuyatoa mbele ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya barabara ya Mahonda Kinyasini Mkokotoni. Hoja hii imechangiwa zaidi na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Kwa kweli barabara hii inawezekana Mhe. Mjumbe kitabu chetu hakukisoma vizuri, kwa sababu tunayo *Project* inayoitwa *Town Entry Roads* na moja katika barabara hizo ni hii.

Kwa hivyo, barabara zote hizo hivi sasa hatuzijengi upya, isipokuwa tunaweka viraka. Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mtu atakwenda hivi sasa kutoka Mahonda basi tayari wameshafika Chaani, tume-*out source*, yaani tumewapa kazi watu wanaziba viraka. Kwa maana hiyo, barabara hii imo katika mpango wa Mradi wa *World Bank* ambao hivi sasa unafanyiwa *study* na ya *study* tutajua ni kiasi gani ambacho kinatakiwa kwa ajili ya barabara hizi na ndipo barabara hizi zitakapojengwa baada ya kupata fedha.

Mhe. Mwenyekiti, barabara hii imo katika kitabu chetu kwenye ukurasa wa 20 *paragraph* ya 47 ya kitabu cha bajeti. Vile vile barabara ya Amani – Mtoni nayo imo ndani ya bajeti na imeelezwa namna ya utekelezaji kwa kutumia fedha kutoka SMT shilingi bilioni 1 zimetajwa ambazo ni ruzuku na kiambatisho Nam. 4 ukurasa wa 55 *Item* Nam. 11.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu matengenezo ya Uwanja wa Mpira siku ile haikutajwa jina, lakini leo nalitaja jina ni Manyamulenge. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitamke mbeye yako pamoja na Baraza hili, kwamba mara tutakapomaliza bajeti yetu, basi yale yote yaliahidiwa na bado haya hayajatekelezwa basi tutayatekeleza. *(Makofi)*

Hoja za barabara za majimboni. Mhe. Mwenyekiti, waliochangia hoja hii ni Waheshimiwa Wajumbe wako 25 na naomba niwataje, ili hao wapiga kura wenu wajue kwamba kweli barabara zao umezitaja na ningenyamaza kimya au nisiwataje. Kwa hivyo, naomba kuwataja kwa sababu na wewe umo.

1. Mhe. Rashid Seif Suleiman;
2. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa;
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu;
4. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa;
5. Mhe. Raya Suleiman Hamada;
6. Mhe. Rufai Said Rufai;
7. Mhe. Saleh Nassor Juma;
8. Mhe. Hamza Hassan Juma;
9. Mhe. Omar Ali Shehe;
10. Mhe. Asaa Othman Hamad;
11. Mhe. Abdi Mosi Kombo;
12. Mhe. Mohammed Haji Khalid;
13. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak;
14. Mhe. Hassan Hamad Omar;
15. Mhe. Ali Salum Haji;
16. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi;
17. Mhe. Viwe Khamis Abdalla;
18. Mhe. Suleiman Hemed Khamis;
19. Mhe. Salim Abdalla Hamad;
20. Mhe. Bikame Yussuf Hamad;
21. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo;
22. Mhe. Amina Iddi Mabrouk;
23. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko;
24. Mhe. Mussa Ali Hassan na
25. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma.

Mhe. Mwenyekiti, nimewataja makusudi kwa dhamira hiyo na ninaomba radhi sana, kwa sababu kama nilivyokwambieni mpaka nipo hapa naletewa vikaratasi vya kufanya majumuisho na wala sina muda huo. Kwa hivyo, kama vilivyoletwa hapa amechangia barabara hiyo basi naomba nay eye awe ametajwa.

Sasa haya ninayo maelezo ya jumla kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kila mmoja ningemjibu kivyake basi tungekesha na tunalo tatizo la *time* na nimeheshimu hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waridhike na hivi ambavyo nitatoa maelezo yafuatayo.

Kwa kweli barabara nyingi za ndani ambazo zinalalamikiwa na Waheshimiwa Wajumbe ziko chini ya usimamizi ama wa Mabaraza ya Miji, Manispaa au Tawala za Mikoa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwatoa wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe, kwamba wizara yangu kwa kulitambua hilo imeanza juhudi za makusudi kwa kuwashirikisha wenzetu hao kusaidiana nasi, ili kuweza kutatua matatizo ya usafiri katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Katika kutimiza azma hiyo, tayari wizara yangu ikishirikiana na Bodi ya Mfuko wa Barabara umefanya kikao na Mabaraza ya Miji pamoja na Tawala za Mikoa kwa upande wa Pemba. Lengo la kikao hicho ni kwamba kwanza kuzitambua barabara hizo kuzikagua, ili kuona hali halisi, kuangalia vikwazo vilivyomo katika barabara hizo na pia kujua ufumbuzi wa vikwazo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wizara yangu kupitia Mfuko wa Barabara haina fedha za kutosha za kuweza kuzitengeneza barabara hizo zote kwa wakati mmoja, basi tunalazimika kukubaliana kulingana na hali ya barabara ipi ipewe kipaumbele cha mwanzo kuliko nyengine. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti wizara kwa utaratibu huo itazifanyia matengenezo barabara hizo. Aidha utaratibu huo ndio pia utakaotumika kwa upande wa Unguja.

Kwa hivyo, tutawahusisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge, Madiwani pamoja na viongozi wengine, kwa ajili ya kushughulikia barabara hizo ambazo mumezitaja na zile ambazo hazikutaja ziko majimboni na zinaleta kero.

Aidha tayari wizara imeshaanza kuzishughulikia baadhi ya barabara za ndani za Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa barabara hizo ni Koba – Kajengwa, Koba – Kinandi, Chukwani – Buyu, Tungu – Nyambiza. Kwa upande wa Pemba Wawi – Vikunguni, M/Mboko na Mhe. Saleh Nassor Juma kama utachukua gari yako, basi hakuna sehemu utakayokwama au kuingia shimoni na watu watakulani sana, kwa sababu utekwenda *speed* kubwa ya

kuhatarisha maisha wa watu, inaonekana hujenda siku nyingi, Finya – Kicha, Wesha – Mkumbuu, na hizo ni baadhi ya barabara kwa bajeti na tutaendelea kutatua kero moja baada ya jengine.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwajuulishe rasmi kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina kawaida ya kushirikiana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge, Madiwani katika kufanikisha utengenezaji wa barabara zao. Kwa hivyo, mara nyingi sisi huwa tunavyo vifaa, lakini hatuna fedha za kununulia mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependa sasa kwamba Mwakilishi, Mbunge, Diwani au hata Halmashauri zisitoe hata *single cent*, isipokuwa watuoneshe tu kuwa hii na ile, lakini tatizo ni kwamba huwa sina fedha za mafuta. Kwa mfano, vyombo vile Waheshimiwa Wajumbe kama vile *bulldozer* mafuta yanayohitajika ni mengi na huwaambia Waheshimiwa kwamba watusaidie mafuta na Mhe. Salim Abdalla Hamad na Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasisi mashahidi, kwamba wanatoa fedha.

Vile vile juzi tu hapa katika Jimbo la Kiembesamaki kutoka Chuo cha Afya imezungu *ring road* kule mpaka *Mbweni Ruins Hotel*, yaani waheshimiwa wamechanga shilingi milioni 2 na tumeiweka barabara utafikiri iwemekwa lami, sasa ni misaada hiyo. Mhe. Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe kuwa tushirikiane katika hilo. *(Makofi)*

Usalama wa watumiaji wa barabara katika sehemu mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, kwa jibu la mkato ni kwamba wizara imeshafanya ukaguzi wa sehemu nyingi sana zinazotaka kujengwa matuta na tayari mpango huu tayari umeshapelekwa katika Mfuko wa Barabara kwa kwa ajili ya kuombewa fedha na kazi hiyo itaanza karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, tumeangalia maeneo ya skuli, kwenye masoko, sehemu zenye mipindo hatari na vijiji ambavyo viko *congested*. Vile vile tumekwenda sehemu nyengine kwa sababu ya maombi ya Masheha na kwengine kutokana na hali halisi ilivyo. Kwa hivyo, utaratibu ni kwamba panakaguliwa, yaani kuna kamati ya Usalama Barabarani inakaa na mimi ndiye ninayotoa *authority* kwamba pawekwe matuta au pasiwekwe, baada ya ushauri wa kamati hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, tokea niwekwe pale nimeshasaini ruhusa tisa na hakuna ruhusa hata moja iliyokataliwa. Kwa maana hiyo, njia iko wazi na tutashirikiana katika hali hiyo. Kwa kweli mlisema mtukosoe na mmetukosoa na hii ndio faida yenyewe hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Mji Mkongwe na hii naomba niseme ni hoja na wala si hoja pekee, lakini ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Hivi sasa tayari kwa mpango wa Usalama Barabarani, hivyo tutazingatia sehemu hiyo wakati wa bajeti na matengenezo kupitia Mfuko wa Barabara. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe Mfuko wa Barabara ndio unaohuwisha au unahami, kwa sababu Mji Mkongwe ni *International Heritage* na *Inshaallah* fedha za kwanza za Mfuko wa Barabara, basi macho yetu yatakuwa kwako. *(Makofi)*

Hoja kuhusu Usalama wa Barabara, Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia. Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Mhe. Kazija Khamis Kona na wengineo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu hoja hii kama ifuatavyo.

Kwa kweli kila barabara inapojengwa huzingatia masuala yote ya usalama ikiwemo kuweka matuta na alama zote kila sehemu inapohitajika. Mhe. Mwenyekiti pamoja na Baraza tukufu, tukubali kwamba *we have problem*, kwa sababu unaweka alama za barabarani kama vile *pipe* ya *inches* tatu na halafu kuna kibati cha *round about eighteen diameter* na kukiandika vizuri na kwenda kukiweka ikifika asubuhi hakipo. Kwa hivyo, mtu tayari ameshachukua na kwenda kuwekea umeme au amekwenda kufanyia mambo yake mengine.

Kutokana na hali hiyo, hivi sasa tumeamua kwamba hatuweki tena alama za namna kama ile na tunajenga *block work* na muhimu kuonesha basi tutafanya hivyo, sasa kama mtu atakwenda kung'oa na lile ah! Tena hiyo itakuwa sijui tuseme vipi. Lakini hizi alama za mabati, vyuma, *pipes* hazikai.

Kwa mfano, tumejengewa barabara nzuri tu na *COGEFAR* tukawekewa mpaka taa za kumweta mweta na wala haijachukua hata miezi miwili vyote havipo na watu wawechukua wakwenda kutia kwenye baskeli zao. Kwa maana hiyo, *we have problem* na lazima tubadilike, vyengine tutajenga barabara kila siku ni hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kila barabara tukiweka matuta basi hiyo si barabara tena, kwa sababu kila anapogongwa mtu ukasema uweke tuta na hivi sasa umeshakuwa utaratibu sasa. Kwa mfano, Kinyasini pale tunajua yaliyotokea, yaani siku hizi utaratibu wa wananchi anapogongwa mtu gari popote pale hata kama dereva kaleva, basi siku ya pili kuna kikundi cha watu na kusema gari haipiti kama hatujaekewa matuta.

Sasa kama ni hivyo, kwa sababu matuta ni kurahisisha gari iende, nadhani sasa tutachimba mashimo ndio rahisi, kwa sababu tuta moja ambalo lina upana wa

futi nne na urefu wa futi sita ni *hundred and twenty three thousand shillings*. Kwa hivyo, kama ni ku-*slow down speed* ya gari basi tutachimba shimo ndio maana yake, sasa lazima tubadilike vyenginevyo hatufiki. *(Makofi)*

Hoja ya kwamba serikali haina nia ya kujenga barabara ya Kiwani, suala hili tunalikataa katakata. Mhe. Mwenyekiti, nimesema kwa *style* au *fashion* yoyote Mjumbe aliyochangia sisi tunaichukua na tutaifanyia kazi. Lakini serikali ingekuwa haina nia ya kujenga barabara hii, nyote mnajua kwamba uvumilivu nayo ni ibada. *(Makofi)*

Vile vile barabara ya Ole Kianga ina miaka 26 inataja na siku nyengine haitajwi na mpaka leo hii bado haijajengwa na watu wa Jimbo la Ole, Wawi, Chonga, Chambani na Mtambile hawajasema kwamba serikali haina nia ya kujenga, kwa sababu serikali yetu tunaijua hali yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika haya serikali inataka kila mahala kuwe na barabara nzuri ya mgongo wa ngisi. Lakini kwa vyovyote wema usizidi uwezo, kwa sababu wewe unafanya wema hata kama huwezi, mt amekuomba fedha huna na huwezi kumwambia sina, unakwenda kuiba si utafungwa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Baraza lako tukufu sisi ndio serikali. Kwa hivyo, serikali ni *Executive, Legislature and Judiciary*, sisi ni serikali, sasa ukisema serikali haina nia, maana yake na wewe pia huna nia. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija, tumetenga shilingi milioni 300/- tukiwa hai na mimi nikidumu katika nafasi hii, basi tutahakikisha zinapatikana na zote zitakwenda Kiwani. Kwa kweli suala hili nitalisimamia mwenyewe pamoja na kushirikiana na wewe pia. *(Makofi)*

Hoja ya maendeleo ya ujenzi wa barabara tatu Pemba hayaridhishi bado hatua zinakwenda taratibu. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwa sababu ujenzi wa barabara una tatizo lake. Mhe. Rufai Said Rufai barabara zile za Wete – Konde, Wete – Gando imesimama kwa 45 *days*, kwa sababu unakata mlima na kuuweka mvua kubwa inakuja na mlima wote unachukuliwa. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili ni shahidi katika Bonde la Mangwena mpunga wote umefukiwa, basi baada ya wale wakulima kulia, amelia yeye Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tulifanya kwa kujua kwamba hapa hakuna tatizo na *bulldozers* zinaondoka saa 12 na saa 6 za usiku liliteremka wingu na yote ikachukuliwa. Sasa huwezi siku ya pili ukenda na *grader* pamoja *bulldozer* kwanza litatoka. Kwa hivyuo, utaratibu au mwendo ambao si wa kasi wa ujenzi

wa barabara kuna mambo mengi na wala si *contrantor* peke yake hata mjengewa, kwa sababu anatudai yule isipokuwa tunaficha ficha tu. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) ameseme wakati mwengine naona fedha hawana, lakini nikizidi kuwasubiri hapa nitachelewa wacha niwahi, basi anatoa fedha zake mfukoni na sisi tukipata tunamlipa zile za kwake na zile ambazo ametukopesha. *If you are not friend*

Mhe. Mwenyekiti, Ununuzi wa Kifusi. Kuna hoja hapa kwamba *UUB* ina machimbo ya kifusi na mawe tunaziita kware, lakini pia ina magari, ina ma*grader* ina vyombo vyote inakuwaje leo *UUB* inunue kifusi kwa mtu binafsi Mhe. Mwenyekiti, hili tunalifanya kweli na tuna sababu za msingi, kuna wakati kuna kazi nyingi lakini na hiyo inayotakiwa ifanywe ni muhimu vile vile, barabara hii ya Amani/Mtoni ya Kilomita nne mnajua historia yake, imejengwa upande mmoja tu upande wa pili fedha zimetolewa tangu Mhe. Mkapa ni Rais kama nimekosea ni miaka mingi, kama kuna barabara yenye ajali nyingi ni barabara ile. Sisi hatujafanya study ya muda mrefu lakini zaidi ya watoto 17 tangu mwezi Januari mpaka sasa hivi kama si mlemavu ameshafukiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo zikatolewa pesa kwa ajili ya barabara ile kwa muda wote huo mpaka limekwamuka mwezi huu wa Machi mwaka huu. Tukasema ina umuhimu wake, kazi kuna nyingi, vifaa havitoshi na tulipofanya *calculations* sisi tunanunua gari moja ya kifusi popote atakapokipata alimradi ni kifusi ambacho kinafaa sio kwa maana ya kifusi tu, ni milioni elfu 90. Kwa sababu kazi ile kapewa na serikali kuna *VAT* asiilmia 18 inarudi serikalini. Amekuja akasema jamani naomba hii *contract* tui-*terminate* mna hasara. Kama tunafanya mambo ya *scales of economic* sisi tukichukua gari letu lile tukachukua kifusi mpaka pale ni shilingi 92,000, mafuta, vipuri, dereva na kila kitu.

Hivyo kwamba nyengine utoe serikali ukishatoa ndo umetoa sababu tumeshakubaliana hili ukasema hapana utumalizie kazi yetu, kwa hivyo hapa hakuna chochote cha varange sisi tunaomba huyu asije kukataa aendelee kutupa hiki kifusi kwa sababu sisi hatuna magari ya kutosha na kifusi chetu sisi tunachukua mbali zaidi tukisema tuchukue pale kwake itabidi atuuzie kile kifusi iwe sisi kazi yetu ni kukipeleka pale. Mheshimiwa hakubahatisha katika haya na ndio maana ile barabara ile inakwenda haraka.

Kwa hivyo hili jawabu lake ni la kifundi tu na la mahisabu na hatufanyi hivi kwa hili tu, Mhe. Mwenyekiti nivumilieni leo ni darasa hili ukimwajiri mfyeka majani wa barabara kuna mambo matatu hayo ukitaka usitake, kwanza mshahara kila mwezi akifyeka asifyeke. Kuna siku atakayostaafu kuna kiinua

mgongo na mambo mengine chungu nzima. Sasa ukifanya hisabu mfanyakazi mmoja tu ni laki moja kwa mwezi ni kima cha chini hicho, lakini unapoikata makataa na tunazipa jumuia ambazo sio za serikali hata jumuiya za vijiji barabara hii kilomita ngapi kumi na nane inakaguliwa huku na huku mtatufyekea kiasi gani milioni moja na nusu, kwa mwaka sisi tumefyeka mara nyingi basi mara tatu. Kwa hivyo barabara ya kilomita kumi na nane kwa mwaka haitugharimu zaidi ya milioni nne, lakini wachukue wafanyakazi wa serikali wa kufyeka barabara ile anakwenda anakaa kitako tu akiona gari inakuja ananyanyuka mahali pa mita tatu anafyeka siku sita.

Kwa hivyo mimi nasema ni vitu ambavyo inabidi tubadilike kama serikali haina pesa basi hizo pesa kidogo ilizokuwa nazo lazima tujue namna ya kutumia vizuri, kila siku nahimizwa hapa ni kweli tunanunua kifusi na siri iliyopo ni hiyo, mmetuuliza mmetuhoji majawabu yetu ni haya tunaomba yule bwana Khalifa na wala sio kwamba kapewa tu hapa na kumeitishwa tenda. Wiki mbili watu wamepewa jamani ee kuna kazi hii aliyekuja ni peke yake au atwambie mtu mwengine kaleta tenda yake akakataliwa, ni mtu mmoja tu kaleta mimi nikawambia ni huyo huyo kaeni kitako mkubaliane na sisi tungeona bei kubwa tungesema basi tuaache tungeieleza serikali kwamba hatuwezi kujenga tupeni muda tumalize kazi hii halafu serikali ijenge.

Mhe. Mwenyekiti, kuna barabara ya majumba mawili mpaka kwa mchina hii iliahidiwa kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami mwaka jana, lakini mara hii haikutajwa bahati mbaya aliyeleta hoja hii hayupo lakini mtamwambia Mhe. Amina Iddi Mabrouk nafikiri hajaenda kwenye hiyo barabara, Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda ameeleza vizuri tunaweka lami *over lay* ya uhakika kutoka Mwanakwerekwe *junction* mpaka nyumba mbili, tunatoka pale kuna barabara ile ambayo mwaka jana tuliweka kifusi mara hii tuna *over lay* mpaka kwa mchina ukenda sasa hivi kuna msongamano wa magari lakini tutafanyaje.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo tunakwenda kwa Mchina Shimoni sokoni mpaka Mbuyu Mnene tumeshaitengeneza vizuri *formation* iko tayari inasubiri lami, kwa hivyo barabara hizi waheshimiwa jawabu laki ni hili tumeahidi na tunatekeleza.

Hoja ya ndege za *Costal* kuwa na abiria mmoja hizi ni *concern* lakini katika ghali ni *pilot* kwa hivyo aidha ndege isiende kama lazima ipate *pilot* wawili ama isende kwa sababu huyo mwenye ndege hatompata wa pili au turisk, iwe na *pilot* mmoja aende mungu na hiyari yake. Sasa tukasema haiwezekani kama wewe mwenye *air line* huwezi kupata *pilot* wawili kwenda Pemba au Dar es Salaam au kwengine. Kwa sababu tuseme hiyo *condition* lakini ni *condition*

ambayo ni sawa sawa na kutunga sheria ambayo haitekelezeki itakuwa sio sheria hiyo mwanasheria Mkuu yupo pale. Ukinambia natunga sheria kwamba uruke mpaka pale uliguse kwa mkono utanifunga, Kwa hivyo kwa nini ndege inakwenda na abiria *pilot* mmoja ni kwasababu ya upungufu wa watu hawa na ughali wao.

Vyombo kutolewa spea na kupewa kampuni ya *MECCO* suala hili lilijitokeza katika hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Idara ni kweli ilivifungua vifaa vya gari la *Grade* SMZ 5616 na kuvitumia kwa ajili ya matengenezo ya *Grade* SMZ 3369 na SMZ 5614 baada ya kutoa dharura ya kuharibika magari hayo yakiwa katika kazi ya matengenezo ya barabara zetu. Mhe. Mwenyekiti sio kweli kwamba vifaa vya magari yetu vimefunguliwa na kuazimwa kwa kampuni ya MECCO, naomba Baraza lako tukufu liamini kwamba kitendo kama hicho hakijawahi kufanyika na uvumi tu sio kweli.

Mhe. Mwenyekiti na hili tunafanya sio kwa hili tu tuna kazi inakwenda kuna kifaa kimeharibika kama kuna kingine tukitoa kule magari yetu yatakwenda, ni sawa sawa na kutoa mfuko huu ukatia mfuko huu ni suruali hiyo hiyo moja hatuwezi kusema kazi isiende kwa sababu tu tukitoa kifaa cha gari hii ambayo haiendi itakuwa tena ni kosa hivyo tunaendelea kufanya kutokana na ule utendaji wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, janareta la UUB ni kweli janareta la UUB liliazimwa na Wizara kutokana na matatizo ya umeme, UUB walikuwa na janareta limezungumzwa hapa lakini limezungumzwa sivyo Wizara waliliazima hiii Wizara yetu, baada ya kurudi umeme liliazimwa Shirika la Meli na kwa hivi sasa janareta hilo liko Kibele kwenye stoo yetu mtu akitaka kuona tukitoka hapa tupande gari tukalione.

Mhe. Mwenyekiti suala la ujenzi wa barabara za Kusini Pemba ambazo wajumbe wamekuwa wakali kidogo, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Mwajuma Faki Mdachi, Mhe. Abdalla Juma kidogo, Mhe. Moh'd Haji Khalid, wao wanasema viwango vya barabara ile havijafikiwa barabara ni mbovu hujamaliza huku huku ulikoanza juzi kumeshachimbuka. Waheshimiwa naomba na hapa nitoe darasa teknolojia tunayoitumia kwa barabara zile ambazo zinafadhiliwa na *NORAD* ni ngeni na mpya, kwa afrika hii Zanzibar na Pemba yenyewe ambako huo mradi upo ni mara ya kwanza watu wengi hawajazoea kwa sababu hawajaiona.

Mimi naijua kwa sababu nimesoma kuna lami za ina chungu nzima hizi zinatumia lami inaitwa *coldmix* kama uji tu au togwa, linatoka kwenye mapipa kama vile lami za kupika unachanganya na kokoto tena sio yale makubwa

kokoto maalum na mchanga kidogo na pengine na saruji inategemea unafanya shughuli katika ardhi gani, na hii huwa inawekwa juu tena ubambazu mwembamba tu *ten milimitar*. Lakini wamehoji sura ile barabara ukiikata kwanza unakuta ardhi kwa sababu ile ardhi imewekwa *formation* lakini *formation* hiyo hiyo unaweza kuifanya *grade* kama iko madhubuti, lakini kama *formation* ardhi *natural* haipo madhubuti unaweka *layer* inaitwa *sub grade* juu yake hapo unaweka *sub base,* juu ya *sub base* unaweka *base* ukimaliza *base* unaweka *surface course* barabara zote tulizojenga zina utaratibu huo na kwa unene wa tabaka hivyo hivyo ambavyo zimefanikiwa.

Mimi nakubali kwamba katika ujenzi kuna mapungufu kuna kasoro na kuna uzembe, lakini kuniambia kwamba barabara hizo hazina umadhubuti ziko chini ya kiwango nakataa, nakataa kwa sababu tu *design* iliyofanywa ndio inayotekelezwa, kuna barabara iliyojengwa na *SS MEHTA* pita barabara moja inaitwa Gana hata ile *guarantee period* haijesha yote nyang'anyang'a.

Mimi nasema kuna mapungufu lakini tusiiponde hii mpaka wale wanaotufadhili hii wakaona maana yake nini, kweli kuna mambo mengine nishengesha tu kejeli ya hali ya juu. Sasa hao ambao wamekuja kujenga ujenzi huu wa barabara unazingatia kweli kweli MKUZA, katika barabara ambazo tumejenga tumeajiti *for thousand two hundred people* kila mmoja miezi mitatu na kila siku anapata shilingi elfu tano na kama ana nguvu kidogo mpaka kumi katika miezi mitatu ni shilingi ngapi hizo.

Halafu barabara hizi sio kama hizi ambazo tumezoea wenyewe wale ndio tutakaowapa yale *material* ikibomoka tunawaambia jamani hapa mpaka pale pamebomoka, kwa sababu wao wamezoea wataifanya vile mimi nasema kasoro nakubali zipo lakini suala kwama sio madhubuti hilo sikubali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri ukiona kimya ujue watu wamefahamu hao tukidhi muda zaidi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mimi nasema tusikejeli kasoro zitolewe, wakili ukimpa *force information* akimwambia jaji *force information* kafungwa, wakili ukimpa uhakika wa mambo yenyewe atapanga namna ya kukunusuru, umeua mwambie nimeua. Mimi nasema tena barabara hizi na Mwenyezi Mungu akitujaalia sisi tumeshapiga tembo kwa ubua, bara bara nyingi sasa mimi mtu aniambie kutoka Mtambile mpaka Kangani kabla ya barabara ile kujengwa gari ilikuwa inachukua *spare will* tatu anajua kwa moja tu harudi. Leo unakwenda kwa *speed* mpaka unaambiwa tuweke matuta usiposhukuru kwa kidogo na kikubwa hushukuru, mimi nasema tuwapeni moyo kuna kasoro tuwaeleze kwa sababu na wale ni wenzetu na hawa anaozungumza

humu wamo wale pale anafikiri hawajui Kiswahili wote nimewaambia waje, si wizara yao hii.

Sisi ni viongozi na nilisema zamani hapa ni vizuri tuwafurahishe watu wetu vizuri tu lakini kwa taarifa ambazo ni sahihi watanuna lakini watajua huu ndio ukweli, kuliko kuwaambia taarifa sizo wakafurahi halafu tukakosana. Mimi nafurahi sana ten asana ukimueleza matatizo ambayo yapo lakini ajue kwamba haya ni matatizo anayozungumza kiongozi aliyepevuka kisiasa kibusara na mambo mengine na sote humu tusingeletwa na watu kama hatukupevuka hivi.

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Kenya/Chambani kupitia halali panapoitwa kwa Mtora Mhe. Mwakilishi wa Mtambile barabara ya Kenya/Chambani inafikia kwa Mtora kweli, lakini barabara ya Ole/Kengeja inatoka Ole inaingia Vitongoji, inakwenda zake mpaka Pujini, inakwenda zake mpaka Chambani, sasa Chambani inaungana na Kwamtora sasa, ukitoka kwa Mtora inaelekea Ukutini moja kwa moja haisimami mpaka Kengeja. Kwa hivyo barabara ile chini ya *PRRP* itamalizikia kwa Mtora, lakini barabara ya Ole/Kengeja itaunga kwa Mtora kutoka Ole, itaunga kwa Mtora kutoka Kengeja, kwa hivyo watu wa Chambani ambako haijafika, watu wa Ukutini wote ishaalla watanufaika na si muda mrefu mazungumzo yetu sisi na *OPEC* katika barabara ile yamebaki ujuzi mmoja tu.

Mhe. Menyekiti, barabara ya Ole/Kengeja itaanza lini na wapi mazungumzo yamechukua muda mrefu lakini kawia ufike, siri iliyopo ni kwamba barabara ile ni ya kilomita 35 inataka kujengwa kwa kontrakta bei ya chini walioyoleta ni 19 milioni dola, tulizonazo ni 11 millioni dola tufanyeje, tujenge nusu kwa hivyo tumekaa nae muda chungu nzima tumesema tutakwenda hivi na hivi mpaka tumefika pahali sasa Makamo wa Pili wa Rais analifuatilia kweli kweli hili. Ingekuwa watu wa Ole wanajua anavyolifuatilia tukishindana kwenye kura watampa yeye. *(Makofi)*

Kwa hivyo waheshimiwa hilo linakwenda vizuri na tumefika pazuri na ishaalla kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu si muda mrefu na hii tutaitangaza hapa kwamba hii barabara tumeshapa *contractor*.

Mhe. Hassan Hamad Omar Kojani kuhusu baadhi ya wananchi wengine bado hawajalipwa fidia kwenye barabara za *MCC* ni kweli kuna baadhi ya waathirika sio wa ukimwi hawajalipwa fidia, kazi hiyo inaendelea ya kuwalipa kabla ya mradi huo kuanza na watu wenye matatizo watalipwa mara tu watakaposawazishiwa matatizo yao kwani fedha zao zote zipo. MCC wana *system* tofauti na yetu sisi tunaiambia Wizara ya Kilimo nendeni kafanyeni

tathmini ya vipango wanatuletea inabidi tuheshimu, tunawaambia wizara inayohusika na nyumba nendeni mkatuletee tathmini ya nyumba wanatuletea.

Sio Wizara ya Miundombinu inayofanya tathmini ya jambo lolote kwa hivyo sisi lazima tuheshimu MCC wamekwenda wenyewe na hata baada ya kufanya tathmini wanawauliza uko tayari kulipwa hichi au huko tayari kuna fomu, ukisema niko tayari wanakulipa ukisema hupo tayari hawakulipi mpaka mtakapo kubaliana. Kwa hivyo ni kweli sasa hivi barabara za MCC fidia ya majumba na mambo yote ardhi, vipando, miti vimeshafikia 4.3. 29 bilion wako wengine hawajakubali tunawabembeleza kwa sababu ni tofauti kama nilivyokwambia na miradi mingine tunayotekeleza na kama hataki lazima tumbembeleze ndio masharti yenyewe na bila ya shaka kuna mahali atapenda, wapo wengine tumekwenda tukazungumza nao wakasema mimi sijaelewa basi akapokea pesa.

Nataka nichukue nafasi hii katika kikao hiki cha baraza na hutuba hii kusema yafuatayo, kuna barabara nyingi tumejenga ambapo tayari tumeshalipa fidia ya majengo, nyumba mabanda na viwanda lakini mpaka tunamaliza kujenga hatujazivunja na watu wanakaa, waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nyie ndio mnapisha watu mimi na wenzangu tumekaa tukasema utaratibu huo ni mbaya sana.

Kwa hivyo kila nyumba ambayo tumeshainunua na tumeshailipia na iko kwenye koridoo ya barabara tutaivunja, hatwendi na *bulldozer* tutamuita Sheha tumwambie hii tumelipa vilelezo hivi hapa tunavunja nyumba yetu na tutahakikisha hapo hapajengwi kwa sababu kuanzia sasa *contractor* watakaojenga barabara zetu moja ya kazi zao ni kuhakikisha kwamba wanalinda koridoo yetu kwa kuweka vigingi, unamaliza barabara unatuonyesha na vigingi ulivyoweka na hayo tumesema tufanye mapema na zile barabara ambazo tumejenga sisi wenyewe kidogo kidogo tutakuwa tunaweka kigingi kuhakikisha kwamba hakuna mtu atakayejenga mle.

Leo tusipoivinja ile nyumba baada ya miaka kumi yule anakaa njia tunataka kuiongeza itabidi tumlipe hatuwezi kulipa mara mbili, bora eneo lile apande mchicha na mambo mengine lakini nyumba tutaivunjwa kwa sababu tusipoivunja ni hasara ya huko mbele, leo tupo sisi kesho wanaokuja sijui itakuwaje. Kwa hivyo hili ni vizuri waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mlijue na tunasema hivi kwa sababu nyinyi ndio wawakilishi wa watu mtu akijakulalamika mjue ameshalipwa. *(Makofi)*

Kuhusu kokoto za barabara za Pemba kuchukuliwa Mombasa Je, hizi za kutoka Muwambe hazifai mnanikumbusha mbali, mimi nilikuwa nafundisha *Civic*

Engineering hapo Mbweni sasa mnanirudisha huko lakini sina budi, *cold mix* ile tabia yake ni tofauti na *hot mix*, *hot mix* ni zile unazozipika ka kuni barabarani huko. Hizi kokoto kuna namna chungu nzima hizi zetu sisi za Vitongoni na Mwambe ni jiwe la chokaa ni jepesi lina matundu chungu nzima japo huyaoni ni laini ukilichukua jiwe lile kokoto moja ukaipima kabla hujaitia maji ukapata *gram* kumi, ukaichukua ile ukaitia kwenye maji masa 12 ichukue uifute fute halafu ipime tena inakuwa na uzito karibu mara mbili badala ya *gram 10* zinakuwa 20 zile kumi zilizoongezeka ni maji yaliyokuwa *absorbed*.

Hii kwenye *cold mix* lami yote utaimaliza na hutakuwa na lami iliyobakia kuunganisha kokoto na kokoto, mwanifahamu kwa hivyo utajenga kokoto zako zile pale gari inapita zinaparuza hizo zinakwenda zake, hizi kokoto kutoka Mombasa sio *line stone ni* hizi chukua *grem* zako kumi zipime wakati kavu zitie kwenye maji sikwambii zinaweza kuongezeka 0.8 kwa sababu ya yale maji ambayo hukuyafuta vizuri. Kwa hivyo lami ile inayotiwa kwenye *cold mix* inabaki kuunganisha kokoto na kokoto kwa ukosefu kwa sababu inawezekana na huko Mombasa hazipatikani, lakini vile vile ukiangalia mahisabu yake kokoto unayoichukua kule na sidhani kama na MCC hawatotumia utaratibu huo wewe ukibanja kokoto kwanza una *blast* upate zile baruti halavu uyavunje vunje, uyachukue kwa gari uyapeleke kwenye *grasha* kuna umeme na mambo chungu nzima.

Ukichukua tani moja ya kokoto hizi hapa bei yake na zile unazochukua Mombasa zina tofauti ya alimia kumi na tano kwa hivyo saa nyengine na mahesabu lazima yafanywe, ingekuwa hatuna chochote hatuwezi kutoa vile tungeelekea huko huko lakini tungeelekea huko tukijua kwamba barabara zetu zitakuwa katika hali sio nzuri. Kwa hivyo suala la kokoto za Mwambe hazifai hapana zinaweza kufaa lakini kwa masharti hayo, ule mradi jamani wenzetu ni wazungu wanataka kuona kwamba kile kilichofanyika ni bora, sisi kweli tungefyatua tu lakini wao hapana, ni pesa wanazitumia na wao wanakuja kukagua kila baada ya miezi mitatua wanakuja kukagua barabara zile.

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa **a**esema asilimia 97 za *feeder road* zimeshughulikiwa na Mabaraza ya Mji, *feeder road* zote zilizopo Pemba hazihusiani na Mabaraza ya Mji zimechukuliwa kutoka vijijini ambako kulikuwa na matatizo ya usafiri, mimi nafikiri hapa mngefanya hivyo hivyo.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Kuhusu barabara Ole/Kengeja, Kipangani, Kangagani na Chwale Kojani, mradi huu unagharamiwa na *OPEC* kama nilivyoeleza katika ukurasa wa 17 katika kitabu hiki, barabara ya Kipangani/Kangani/Chwale hizi ziko katika mradi wa *MCC* kama ilivyoelezwa katika bajeti hii ukurasa wa 15, barabara ya Mchanga Mdogo/Hindi wizara kwa

kushirikiana na wana kijiji kupitia msaada wa *UNDP* walifanya matengenezo na sasa hivi inapitika vizuri. Hizi vipo katika barabara za jimboni. Zingatio la mafuta katika barabara ya Ole/ Kengeja. Ushauri wako Wizara itauchukua.

Mhe. Hija tena jimbo la Kiwani kuhusu barabara ya Mgagadu/Kiwani, barabara hii inatengewa shilingi milioni mia tatu. Hii sina haja ya kurudia nimeshamuahidi shilingi milioni 300 zote pakiwa na uhai na tukidumu katika nafasi hizi. Tutazitumia zote na mimi na wewe tutakuwa mashahidi.

Mhe. Rufai anaseme fidia ya vipando hazijatolewa. Ni kweli mwahali mwingi fidia ya vipando hatujalipa. Mimi nina ushahidi kwamba tutalipa, kwa sababu kuna muhali mwingi tumejenga barabara na tumeshalipa na hili ni deni la Serikali kwa watu. Tuvumilieni.

Hoja ya kununua vifa vya kuhudumia mizigo bandarini. Wizara kupitia Shirika la Bandari linajua suala hilo na tayari limeanza kufanya kazi. Lakini kutokana na ukubwa wa gharama hizo utekelezaji wake unafanywa kwa awamu. Awamu ya kwanza tumenunua *terminal* trekta mbili kwa ajili ya kuhusumia makontena kwa mwaka 2008 na kwa thamani ya *Euro* milioni moja lakini tatu na ishirini na moja na thamanini na nane.

Ununuzi wa wa *mobile crane* mbili ambazo zinatarajiwa kuwasili mwisho wa mwaka huu na vifaa vyengine vitaagiwa kwa mujibu wa hali ya fedha ya Shirika kwa thamani ya dola za Kimarekani milioni moja laki mbili sitini na moja elfu mia nne na ishiri na mbili.

Gharama za LCT Jitihada, wajumbe wengi wamechangia. Kwa bahati nina *break down* ya gharama zote hata pini. Hizi *accounts* zinakuwa *accounted* halafu zinakuwa *audited* kwa hivyo si suala ya kuwa unaandika tu unavyotaka mwenyewe. Lakini gharama kamili ya matengenezo ya meli hii ni shilingi bilioni mbili, milioni mia sita na hamsini na mbili, laki tisa na thalathini na saba elfu, mia mbili na hamsini na tatu, nukta hamsini na tano.

Gharama hizo zimejumuisha ununuzi wa mashine mbili mpya, majenereta. Majenereta mawili mapya mtambo wa chumba cha mashine pamoja na chumba cha usukani. Aidha gharama hizo zinajumuisha *marine plate* zilizotumika kutengenezea umbo la nje la meli hiyo yaani *hurl* pamoja na malipo ya wafanyakazi na vifaa vyengine vyote vya matengenezo. Vilivyonunuliwa na fedha ni hizo mashine lakini *plates* Shirika la Bandari lina Kampuni inaidai *charges* Shirika lile likawa halina fedha lakini lina vifaa tunavyovihitaji. Kwa hivyo *it was a butter systerm*. Tupeni *plates* hizi tunafuta, kwa hivyo sio kama hizi zote zilitoka katika mfuko. Aa hivyo ndivyo ilivyokuwa. Ili mahesabu

yakae sawa lazima tuseme kwamba gharama ni hii na mashine hizo la katapila mtu anasema mashine hii ni mtumba. Unaweza ukenda pale mlandege ukanunua jinzi mbichi Shs. 3,000, haya kachukue kitambaa sasa pale Darajani kitafika Sh. 40/-.

Sisi ile tumeikuta ipo hali hiyo na sasa hivi ndio inapunguza angalau Sh. 60/- za mchele kule Pemba. Sasa hivi Jitihada ndiyo inachukua makontena. Zamani meli ya mchele ikifika pale mchele unachukuliwa unekwenda kuwekwa kwenye ghala. Mchele wa Pemba huo, halafu unatolewa kwenye ghala unarudi tena bandarini. *Charge* ya kutoka kwenda na kwenda kurudi wafanyabiashara wanaziingiza. Sasa hivi unatoka kwenye meli unaingia kwenye Jitihada, hauwendi tena ghalani. Jitihada inachukua mpaka Mkoani pale ndio unatolewa. Kwa hivyo *blessing disguise* na hizo ndizo gharama za matengenezo ya hii na ni meli ambayo ni ya serikali.

Kuhusu gharama ya tishali dogo la abiria. Gharama ya tishali hilo limenunuliwa kwa Euro laki sita na ishirini na tano elfu, kutoka Kampuni ya *Damens Shipyard* na limetengenezwa Afrika ya Kusini. Tishali hilo ndilo linatumika hivi sasa kwa kupanda na kuteremkia abiria badala ya tishali kubwa kuondoshwa kwa matengenezo. Tuna matishali mawili kubwa na dogo, kubwa ndio lile mlilolizowea. Meli tatu tilikuwa zikijipanga kwa wakati mmoja. Kaskazini, Kusini, Magharibi, hili ni dogo, lile likuwa 40 kwa 20, hili ni 10 kwa 20. Sasa hivi kwa sababu ya udogo wake hatuwezi kufunga meli mbili meli moja. Pengine cha pili kidogo, tumesema hivyo kwa sababu lile lilokuwepo kubwa lazima liende matengenezo vyenginevyo lingezama. Lipo kwenye matengenezo kwenye chelezo chetu, matengenezo tunafanya wenyewe.

Lile dogo ambalo tumelinunua ni *multipurpose* ni dogo lakini mle kuna *fuel pumps* tutalitumia kwa kutia mafuta na kuzipelekea meli hata kama zipo *work shop*. Kwa hivyo waheshimiwa *justification* ya kununua lile na gharama zake ni hizo. Limeundwa Afrika ya Kusini. Aidha tishali hili limetengenezwa ili liweze kutumika kubebea mafuta kama nilivyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kutokidhi haja ya jengo la abiria lililokuwepo sasa katika Bandari ya Malindi. Wizara yangu inakubaliana na hoja hiyo. Lakini naomba Baraza lako tukufu lielewe kuwa huduma zinazotolewa sasa ni za muda tu. Wizara yangu kupitia Shirika la bandari linalengo la kujenga jengo la abiria la kisasa katika bndari ya Malindi Unguja ambalo litakuwa na huduma zote za kisasa ikiwemo *VIP*, mikahawa na vyoo. Ramani ninayo ofisini kwangu. Watu wengi walisema ni kwanini hatumpi mzalendo mwenzetu Baharesa. Yote hayo tunayafahamu. Lakini kwa nini? Zipo sababu na baadhi yao nitazitaja.

Kwa mara ya kwanza Mhe. Baharesa alikuja ili ajenga kama iliyokuwepo Dar-es-Salaam lakini iwe yake peke yake. Kwa hivyo abiria wengine wote ambao sio wa meli ile wasingeruhusiwa kuingia mle, kama Dar-es-Salaam. Kule kwenye lile jengo lake labda ukaibie, lakini wenyewe huwa hawataki. Kwa Zanzibar hiyo itakuwa ngumu. Wote tu wanyonge, wengine wanakaa chini ya mwamvuli wengine anapigwa na mvua. Tukamwambia kama unataka jenga tukubaliane ujenge kwa wote. Akasema basi ngojeni. Kwa hivyo hapo ndio tulipokwama kwanza.

Lakini uwezekano wa kujengwa bila ya kumtumia yeye kwa watu wote kama hivi ninavyoeleza upo e*stimate* haizidi milioni mia tatu. *Capacity* ya bandari yetu abiria ni 1.2 *million per year* kila tiketi au ukiweka *service charge* ya bandari ambayo kwa mujibu wa *act* ya bandari wanaruhusiwa *service charge* ya bandari ya Shs. 100/- tu kwa kila abiria, 1.2 milion mara mia ni ngapi. Kwa hivyo wewe unaweza ukaijenga ile bandari kwa kutumia cervice charge.

Sasa hivi tuna mazungumzo na *Zanzibar Social Security Fund* ramani tunazo na tutafika mahali ZSSF ni serikali. Tutafika pahali bila ya kutumia mzalendo, bila ya kutumia *investor,* bila ya kutumia nani. *Investor* itakuwa na ni serikali yenyewe, *they have got money those people.* Tuna mazungumzo mazuri na hawa, tukifika mahali tutaiarifu Serikali. Tunahangaika jamani, tunajitahidi sana lakini ni lazima tutafute kitu ambacho watu wote wakisikia kimefanyika hata ukilaumu ukielezwa unageuka unasifu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, maana ya makofi hayo mimi najua, lakini kama nilivyosema watu 45 wamechangia tunapunguza buti. Kwa sababu wengine hapa wasipotajwa tutasemaje siye. Kwa hivyo nivumilieni. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri haya makofi yanaashiria kukubalika kwako kutokana na hoja ulizokwisha kuzitolea ufafanuzi. Inaonekana wajumbe wameridhika.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Msongamano wa eneo la gati la abiria, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Bandarini tayari limeweka mpango maalum wa kudhibiti msongamano wa magari hasa wakati wa kuwasili vyombo nyakati za jioni ndani ya eneo hilo. Kwa upande wa nje ya ukuta wa eneo hilo kwenye barabara kuu ya Mizingani ni eneo linalosimamiwa na Baraza la Manispaa.

Aidha kwa upande wa baharini mipango iliyopangwa ni kuviingiza vyombo kimoja kimoja chini ya usimamizi wa Shirika la Bandari, jambo ambalo ni

moja ya majukumu yao. Huu ni msongamano wa pale ambapo tunahama Forodha Mchanga tunakwenda bandarini.

Mhe. Ismail Jussa anaendelea kuhusiana na wafanyakazi wa kubwa *group C.* Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba wafanyakazi wa *group C* ni vibarua wa kubwa ambao huajiriwa kwa mujibu wa kazi za ziada za msimu. Wanalipwa mara tu baada ya kumaliza kazi zao. Kwa wafanyakazi walioshiriki katika kazi ya matengenezo ya LCT. Jitihada Shirila la Bandari linawatambua na ndio linalowatumia katika kazi nyengine zote na mbali mbali za matengenezo ya vyombo vinavyohudumiwa kwenye chelezo hicho.

Kwa upande wa kupatiwa ajira za kudumu wafanyakazi hao ukweli ni kwamba Shirika la bandari lina zaidi ya wafanyakazi 600 wanaolipwa mishahara yao kwa mwezi. Hivyo kwa sasa Shirika linao wafanyakazi wengi kuliko mahitaji halisi ya wafanyakazi 400. Kwa utaratibu huo ni vigumu kuongeza ajira za kudumu kwa wafanyakazi wapya hadi pale zitakapotokea nafasi tupu kutokana na walioajiriwa sasa kustaafu au kuondoka kwa sababu nyenginezo.

Kujua maboya ambayo yanafanya kazi na yasiyofanya kazi. Bandari za Zanzibar zina maboya saba ya taa. Maboya 14 ambayo hayana taa ni maboya bubu kwa Unguja na Pemba. Maboya yote hayo yanafanyakazi wakati wa mchana. Kwa yale maboya yenye taa hivi sasa lipo boya moja tu Unguja, ambalo taa yake haiwaki. Shirika linampango wa kuitengeneza taa hiyo kama ilivyokawaida yake.

Msongamano wa abiria katika bandari ya Mkaoni Pemba. Shirika limeweka utaratibu wa kusimamia udhibiti katika bandari hiyo kwa kutumia mpango wa kuwazuia abira wanaotaka kusafiri hadi pale abiria wanaowasili wanapomaliza kuteremka katika chombo husika. Katika hali hiyo abiria ambao wanakuwemo katika jengo la abiria hutakiwa kusubiri na kutangaziwa wakati wa kuanza kuelekea kwenye meli ili kupunguza msongamano gatini. Hata hivyo baadhi ya abira wamekuwa na kawaida ya kuondoka katika mlango wa ndani wa kuendea getini mara tu chombo kinapotokeza na kuwasilia bandarini. Shirika la Bandari litazidisha usimamizi wake ili kudhibiti hali hiyo na kuleta usalama wa kutosha.

Mhe. Asha Bakari kuhusu ujenzi wa jengo la abiria bandari nimeshalieleza. Mhe. Omar Sheha kuhusu uimarishaji wa gati ya Wete na Wesha. Wizara kupitia shirika la Bandari limeshaingiza matengenezo ya bandari hizo katika mpango wake wa maendeleo kwa muda mfupi, ambapo imekusudiwa kurefushwa gati hizo hadi kufikia urefu wa maji. Itarefushwa mpaka mahali ambapo hata maji yakiwa katika *low tide* majahazi na meli ziweze kufika ndio

maana yake hapo. Hata hivyo kwa mwaka huu fedha kwa mwaka 2011/2012 haikutengewa fedha katika bajeti ya utekelezaji wake kutokana na majukumu makubwa yanayoikabili shirika kwa mwaka huu.

Mhe. Asaa Othmani Bandari ya Mkoani kutotumika ipasavyo. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Shirila la Bandari imekusudia kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa awamu ili iweze kutumika kama inavyokusudiwa. Mipango hiyo ni kurekebisha miundominu ya gati kwa kurekebisha sehemu iliyodidimia kazi ambayo inategemea kuanza katika mezi huu ya Julai 2011. Baada ya hapo mpango utakaofuata ni ununuzi wa vifaa, *crane complete* kwa matumizi ya bandari hiyo pamoja na ya Wete.

Mhe. Mwenyekiti, tumezungumza na Kampuni ya meli na imekubali kama tutakubaliana basi kutakuwa na meli.
Mhe. Mwenyekiti: Kwa vile Mhe. Waziri anaendelea kutoa majawabu kwa kina zaidi tumuombe basi kutokana na muda ulivyo Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ili tuweze kuweka Kanuni kando na tuweze kuongeza muda tuweze kumaliza hili suala linalazimika kumalizika sasa hivi na jioni tuendelee na bajeti ya Wizara ya Elimu. Mhe. Waziri tafadhali.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi wa Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda uliobaki hautoshi Mhe. Waziri kukamilisha kujibu hoja mbali mbali za wajumbe wa Baraza hili tukufu. Na kwa kuwa tutakuwa na Kamati ya Matumizi kwa hivyo naomba Baraza lako tukufu tutengue muda ili tuweze kumaliza shughuli iliyokuwepo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na wajumbe nawashukuru sana. Hoja ya mnara wa Kibomasha kuwa hauwaki. Mnara wa Kigomasha ulifungwa taa za *solar* mwaka 2001 kutoka *Farous Marine* hata hivyo taa hiyo na ile ya Mnara wa Matumbini ambazo zimenunuliwa kutoka Uingereza hazifanyi kazi ipasavyo. Shirika limeandaa mapango wa kuzibadilisha taa za minara yote saba kwa Unguja na Pemba kwa kufunga taa za *solar* kupitia mradi utakaouharimu shirika zaidi ya dola za Kimarekani laki saba.

Mhe. Abdi Mosi Kombo bandari ya Mkokotoni kuimarishwa kuwa ya kimataifa. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano haina mapango wa kuifanya bandari hiyo kuwa ya Kimataifa isipokuwa tunao mpango wa kujenga gati ndogo jeti katika bandari hiyo. Hata hivyo kabla ya kuanza kwa mradi huo kumejitokeza haja ya kutathmini upya ujenzi huo wa msingi wa kuekeza katika eneo la Mkokotoni au Fukuchani ambalo lina kina kikubwa cha maji karibu na nchi kavu kuliko eneo la Mkokotoni.

Mhe. Wanu alitaka kujua kwa nini meli za *Car carres* hazifiki Zanzibar. Kampuni iliyokuwa ikileta meli za kubebea magari imefuta safari zake kuja moja kwa moja Zanzibar. Hadi muda huu serikali haijapata sababu za msingi kuhusiana na sababu hizo. Kutokana na kukosekana meli hizo bandari ya malindi Zanzibar inakosa kiasi cha Dola za Kimarekani 15,000 hadi 20,000 kwa kila meli moja.

Mhe. Jaku, bandari kukosa taa, maji yakunywa na matumizi ya vifaa ya GMDSS, bandari ya Malindi inazo taa za kutosha isipokuwa taa hizo huzidiwa na makontena yanapopagwa bandari humu hasa yanapokuwa mengi ambayo hupangwa kwenda juu hadi gorofa 5. Hali hiyo imetokana na minara ya mwanzo iliyokuwa mirefu zaidi kuharibika na mengine kuanguka. Shirika la Bandari tayari linao mpango wa kununua minara mengine mipya na ya kisasa kwa madhumuni ya kurekebisha kasoro hizo. Kuhusu maji bandarini yanapatikana isipokuwa huhadimika pale yanapokosekana katika eneo lote la Malindi.

Hata hivyo Shirika la Bandari huweka maji kiasi cha tani 400 kwenye tishali lao maalum ambayo huuzwa kwa meli zinazohitaji maji hayo. Kwa upande wa gati ya Kaskazini *North dock Nam. 3,* mipango ipo mbioni ya kuungwa bomba yaani paipu mpya ya maji ili yaweze kupatikana kwa upande huo. Kuhusu matatizo ya GBDSS ni kwamba tayari vifaa hivyo vimeshanunuliwa na Shirika na vitafungwa hivi karibuni katika bandari za Malindi na Mkoani Pemba. Hivi sasa wafanyakazi wa Shirika wanaandaliwa mafunzo maalum ya matumizi ya vifaa hivyo. Ni muhimu kwa wenye meli vile vile hasa hapa nchini na wao wakafunga mitambo itakayokubaliana na vifaa hivyo kwenye meli zao ili waweze kutumia huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, wanaolalamika wanalalamikia suala hili la maji ni wale wanaotaka maji ya bure. Tishali letu lina uwezo wa tani 400, yapo yanapatikana na kila mtu mwenye kuhitaji atapewa.

Mhe. Mwenyekiti, safari za Nje za Mhe. Waziri, Mhe. Hamza alitaka maelezo ya kina. Akataja *Swiss Port,* Switzaland. Mhe. Mwenyekiti, mimi tangu niwe

Waziri katika kipindi hichi nimefanya safari za nje tano, zote kwa ruhusa ya Raisi. Ya kwanza ni ya Dubei mimi na Mhe. Waziri wa Fedha. Waziri wa Fedha ndiye *share holder* wa Zantel mimi ndiye mtumizi na mratib. Zantel ilikuwa na mabadiliko ya uongozi na sisi ni viongozi wapya katika serikali hii. Sisi ndio tunaohusiana na Zantel, kwa hiyo tulikwenda Abudhabi, makao makuu ya Zantel kwa mualiko wa Zantel yenyewe. Tukakutana na *management,* faida ya safari hii tutaieleza wakati ninapozungumza Zantel, kulikuwa kuna watu wanne, wakati nitakapozungumza Zantel ndio mtajua faida ya safari hii.

Safari ya pili ni kuhudhuria Semina maalum ya kimataifa iliyoandaliwa na IFC *International Finance Cooperation* ya *World Bank*, tulialikwa na ilikuwa inazungumzia *Global, AirPort* PPP ni *Public Private Pattnership*, semina hii ya kimataifa iliyoandaliwa na *World Bank.* Mimi na Waziri wa Fedha tulialikwa kwa hivyo tulikwenda na gharama za *IFC*. Tulialikwa kwa sababu inatuhusu na ilikuwa *of high level* mawaziri, makatibu wakuu ndio tuliokutana nao kule. Sasa na sisi kama mawaziri wa nchi kama hii hatuwezi kukaa nyuma katika mambo haya.

Safari ya tatu ni ya Uturuki. Suala la Uturuki litaelezwa kinaga ubaga si leo, lakini ndio hayo mnayoyasikia. Pemba kutakuwa na *extension*, *terminal* mpya itajengwa, *investment* yao ni *about forty millions* kuna mambo mengi. Lakini ni *result* ya safari yetu hii. Na hii vile vile ilidhaminiwa na hao ambao walitaka tukaone wanachofanya kabla ya kukubali wao kufanya.

Safari ya nne ni ya Ujerumani katika mwezi wa tano. Ujerumani kulikuwa na *International Conference and Exhibition* kuhusu *new technology* ya *vehicles*, lakini *for high level administrators*, Mawaziri, Mkatibu wakuu, wakuu wa makampuni. Nilikwenda kwa gharama zao baada ya kunialika kama Waziri.

Safari yangu ya tano ni ya Switzerland, hiyo S*wissport*. Mhe. Mwenyekiti, tangu Mhe. Karume ni Rais *Swissport* walitakiwa wa-*operate* mambo ya *ground handling* pale *Airport*. Kwa hivyo sisi hili sio kama tumelianzisha, tumelikuta na tunaliendeleza. *Airport* yetu ya Kimataifa wanaofanya *ground handling*, uchukuzi wa mizigo na mambo mengine ni *ZAT*. Nyote mnalalamika hapa, *ZAT* wana mkataba na serikali wa miaka 30 wana *monopoly* peke yao. Kwa hivyo wakifanya, wasifanye *so what*? Hawana mshindani, wana mkataba wa miaka 30. *Airport* yetu ile tuna i–*develop*, mtalii anakuja pale, mizigo inabebwa kwa kichwa, kuna mambo mengine yanatokea.

Hii ni serikali ambayo inajua inafanya nini. Tukasema hapana, kwa nini tusiendeleze hii hii Mhe. Karume ambayo katuachia. *Swissport* wakatualika,

tumekwenda kule kwa gharama zao, nimekwenda mimi, amekwenda *DG Director General* wa *Airport* na *Chief Security officer,* tumekweda kule, wakatuonesha wanavyo *operate* kwenye *Zurich Air Port na Bassel,* ili sio tukubali kwa kusikia. Kwa hivyo huku kote tulipokwenda Waheshimiwa serikali inajua. Safari hizi za serikali lakini zimedhaminiwa na waliotualika. Serikali ilichofanya ni kukamilisha Kanuni, Afisa yoyote anakwenda nje kama safari inagharamiwa anapewa nusu posho. Huo ni utekelezaji hata kama ungezikataa lakini zipo na hata kama ungetaka zaidi usingepewa kwa sababu ya kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, safari nyengine ya Waziri mimi ilikuwa ya binafsi ya UK. Niliondoka hapa tarehe 2 Mhe. Spika, anajua, Mhe. Rais anajua, Mhe. Makamo wa Kwanza anajua, Mhe. Makamo wa Pili anajua. Uingereza nilikwenda kufanya nini. Nakuombeni dakika mbili.

Mimi digirii yangu ya pili nilifanyia chuo kimoja kinaitwa *Lafra University* tangu ianzishwe wahitimu wa chuo kile ni zaidi ya laki moja na arubaini elfu katika nchi zaidi ya 170. Miongini mwao ni mimi mmoja hao wahitimu. Sasa wahitimu wote wa chuo kile kuna jina wanaitwa **Alumni** ni jina maarufu. Mimi ilikwenda kwenda vipi, ilikuwaje, lakini wanajua habari zangu.

Nikapata barua kutoka kwa *Vice Chancellor* na *president of University* kwamba nimetunukiwa tunzo maalum. Tunzo hii ni mara ya kwanza kwa Chuo Kikuu hichi kutoa na katika wahitimo hao 140 katika nchi 170 tulipewa tunzo hii watu watano (5) tu. Mmoja ni miye Mzanzibari, mwengine mu-Ireland, mwengine Mpakistan, mmoja wa Uingereza na mwengine wa Uganda. Kwa Afrika nzima na Hamad Masoud na *Master* Lon wa Uganda.

Hii inaitwa *University Distinguish Alumni Award* na imetolewa kwa sababu O*ut Standing Commitment and Achievement in Engineering and Infrastructure.* Sikuchukua sikuchukua *a single cent* ya serikali, nimekwenda kwa gharama zangu mwenyewe, nilichopewa serikalini ni ruhusa ya Mhe. Rais. Kwa hivyo, hizi ndio safari ambazo nimefanya na nimefanya hivi kwa sababu kama waziri makini siwezi tu mimi nikakaa kitako hivi nasubiri, mambo mengine lazima uyafuate huko. *ZAT* hatuna mpango wa kuinyang'anya kazi. Serikali tumeshapeleka taarifa, serikali wanasema *ZAT* ni wazalendo, *ZAT* wame-*invest* na wametusaidia ni wa hapa hapa petu. Lakini bado tunahitaji *competition.*

Kwa hivyo, *ZAT* haondolewi kama ni kuondoka *ZAT* ataondoka mwenyewe kama atashindwa na *competition,* tumeelewa jamani na tumesema hatuitishi *tender* kwa sababu ukiitisha *tender* na *International* hawa *Handlers* inawezekana kwamba *ZAT* wakashindwa, na wakishindwa itakuwa ni huo

mpango ulo sema kwama *ZAT* tumefanyia mkakati wa kuinyang'anya kazi. Mhe. Mwenyekiti, hatufanyi hivyo hata wakiwa wawili mmoja atakuwa ni *ZAT*, tunatoa *licence* mbili za ku-operate pale sisi, lakini kwa hali ilivyo na *Act* inayokuja kesho kutwa ya *Zanzibar Airport Authority* na *Air Drown Act* ni mbili hizo. Sheria hizi zinaletwa makusudi ili ku-*strengthen* na hawa *investors* wapate *protection* ya kisheria. Lakini si suala la kwamba tunataka kuinyanganya *ZAT* kazi, hapana *ZAT* wameajiri watu wengi, *ZAT* wametusaidia Waheshimiwa na kwa hivyo serikali inajua hilo, na ndio maana nikasema serikali pamoja na yote *ZAT* itabaki, labda isijibakishe wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwambia kwa sababu ya wakati sitaki niendelee sana, lakini nimalize hili la mwisho mengine nitajibu kama kutakuwa na buti, maana yake majawabu ninayo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, mapato kutoka taasisi za Muungano, hili angekuwepo Waziri wa Fedha basi tungesaidiana, lakini mimi niseme haya ambayo nayajua. Mashirika ya Muungano tuliyonayo sisi hapa ni *TTCL*, hili ni Shirika la Simu, *TCAA*, Shirika la Anga, *TMA*, Mamlaka ya Hali ya Hewa, kuna *TPC* na kuna *TCRA*. Katika mashirika haya ninachoweza kuthibitisha mimi ni kwamba bodi zote tuna *member* kutoka Zanzibar angalau mmoja. Lakini ni kiasi gani kinapatikana kipi hakipatikani, kuna mambo haya ya mapato ya Muungano na mgawanyo kuna kamati inaitwa *JFC (Joint Finance Commission)*, hawa ndio wanaojua mambo yote. Lakini mimi ninachofahamu ni kwamba katika mashirika haya *TCRA the reaches* na sijui kama sisi tunapata chochote.

Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kwamba yote hii ina-*reflect* mwenendo mbaya wa huu Muungano wetu, kama shirika ni la Muungano kama *TCRA* Katibu Mkuu wangu mimi ni Makamo Mwenyekiti. Lakini hiyo kuhudhuria yeye ndio tumeshanufaika, tunataka ahadhurie lakini utajiri wote huu alionao *TCRA* na *raw material* yao ni *space*. Mhe. Mwenyekiti, kuna mtu kanambia hivyo nyinyi Zanzibar hamuwezi kuanzisha *Zanzibar Regulatory Authority*. Anasema katika shirika au kampuni au taasisi ambayo ni *very rlch licence* tu kuna *licence* mpaka milioni 2 kwa mwaka. Kwa hivyo, mimi nasema katika haya mimi ndio ninayojua mashirika yako haya nayalea mimi naya-*coordinate* mimi lakini hicho ndicho ninachokijua. Zaidi watu wa fedha wanajua zaidi na wale waliomo kwenye kamati ya *JFC* wao watajua zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kuchangia kidogo tu. Waheshimiwa Wajumbe mjadala wa Muungano unakuja mimi nakuombeni moja ya suala ambalo lipigiwe debe ni Urais wa Muungano uwe kwa zamu. Mhe. Mwenyekiti, wameshachukua miaka 20 mfululizo ndio, kwani si Muungano wa nchi mbili basi mara hii iwe zamu yetu tena miaka 10. Wagombea wa Urais wa Jamhuri

ya Muungano wawe Wazanzibari peke yao, CUF waweke mgombea wao, CCM wao, CHADEMA wao lakini wawe wote ni Wazanzibari. Mimi nasema niko makini katika hili, Mwalimu Nyerere Marehemu kutoka Bara, Shekhe Ali Hassan Mwinyi ndio tumeonjeshwa, Mhe. Mkapa kutoka Bara, Mhe. Kikwete miaka 50 tuambieni wenzetu *if you are serious and if the like this Muungano* mara hii iwe zamu yetu, miaka 10 halafu baada ya miaka 10 mengine watagombea wao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa vile hoja imetolewa sasa labda tuwahoji wale ambao wanakubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wasiokubali, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 26 – WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	98,980,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru katika mchango wangu nimezungumzia suala katika sehemu ya mapato lile suala ambalo Mhe. Waziri amelimazia kulitolea ufafanuzi. Kwanza naomba kumshukuru kalitolea ufafanuzi mzuri, lakini nilikuwa bado nataka maelezo kutoka kwake kwamba kuna mashirika kadhaa haya ya Muungano ambayo yanazalisha mapato. Nilitaka kujua mchango wake kwa Zanzibar ni upi, na ametuambia hapa kwamba kutokana na maelezo yake inaonekana kuwa mchango wake haueleweki na niliwahi hata kutoa mfano.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe kifungu tunachokijadili kina sifuri sasa sijui wewe unaelezea sehemu gani?

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mmekitaja nyinyi eti.

Mhe. Mwenyekiti: Ni bahati mbaya Mhe. Mjumbe.

Kifungu 0501	Mamlaka ya Usafiri Baharini	163,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Anga	1,210,410,000
Kifungu 0701	Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara	500,000,000
Kifungu 0801	Idara ya Usafiri na Leseni	280,600,000
	Jumla ya Fungu	**1,757,990,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamatiya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 26 – WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	1,065,000,000
Kifungu 0401		

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili niweze kupata ufafanuzi wa kutosha kuhusu majibu ya Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana kwa majibu yake mazuri, lakini Mhe. Mwenyekiti, vile vile jana nilipokuwa nikichangia nilieleza kasoro za mawaziri. Na hili sio kama kwa kuwafurahisha wananchi kama alivyosema Mhe. Waziri, hili nimelizungumza tangu tuko Kikwajuni katika Baraza lile la Wawakilishi lilopita, mara nyingi katika bajeti za mawaziri nilikuwa namsifu sana Mwalimu Haroun Ali Suleiman aliyekuwa Waziri wa Elimu. Nilikuwa namsifu sana kwa sababu gani? Kwa sababu anaelezea safari zake zote za nje na anatueleza katika kitabu chake nimekwenda hapa, nitafanya hivi nitafanikiwa hata kama hajafanikiwa lakini anatueleza.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nilipokuwa najaribu kukosowa kitabu cha Mhe. Waziri ndio nikasema kwamba Mhe. Waziri hiki kitabu chako mbona hakijatimia, kwa sababu tunaamini kuna mambo mengi mnayafanya. Mhe. Mwenyekiti, mimi huwa sipendi kila wakati labda kuwasifu tu mawaziri, mawaziri wanatakiwa wajisifu wenyewe katika vitabu kwa mujibu wa kazi walizofanya. Mhe. Mwenyekiti, hata Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anaelezea kuwa viongozi wa serikali mnatakiwa mnayoyafanya muyaeleze vyenginevyo wanannchi wataeleza wanayoyajua wao au wanayoyasikia wao. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri asinione labda Mhe. Hamza kama mkorofi, mimi sio mkorofi wala sipendi kuwafurahisha watu kwenye televisheni, maana yake siku hizi ndio lugha tunayoambiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika hoja nikwamba nimepata maelezo mengi kutokana na hoja zangu, nashukuru mawaziri watatu wote wamejibu hoja zangu, na hii ndio inavyotakiwa. Sio Mhe. Mwakilishi unasema halafu waziri hana chakukujibu, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri amenijibu lakini sikuridhika, namshukuru sana Mhe. Machano amejibu lakini sikuridhika na pia namshukuru kidogo Mhe. Waziri kuna baadhi ya hoja zangu kidogo amezipunguza kasi, na hii ndio inavyotakiwa. Sasa nakuja na moja baada ya moja.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia barabara ya Kwamtipura unaweza ukaniuliza kwa nini usisubiri kifungu cha ujenzi na utunzaji wa barabara kwenye mipango hapa ndio mambo yote yanapopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, barabara hii nimeizungumza tokea mwaka 2000 naingia hapa Barazani, nimepigwa danadana sana nikamuomba Mhe. Rais mwaka 2006 Rais Amani Abeid Karume tulipokuwa tunafungua Skuli ya Chekechea ya Kwamtipura kama nilivyoeleza. Mheshimiwa akaniambia kwamba basi wacha wataalamu nitawatuma tutaitengeneza tena katika kiwango cha lami, tulishukuru na wananchi wakapiga makofi pale alizungumza Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka tumekwenda katika uchaguzi, tumemaliza uchaguzi wa Rais mpya pia nimemueleza kilio changu na amekikubali. Lakini vile vile Waziri wa Mawasiliano aliyepita Mhe. Machano kweli kazungumza yeye alikuwa rafiki yangu lakini alikuwa, siku hizi inaonesha sio rafiki yangu kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mimi niliandika barua alipokuwa Waziri wa Mawasiliano. Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Saateni, Mboriborini mpaka Darajabovu kuna ahadi ya Mhe. Rais na nakla nikampelekea. Nadhani Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais ambaye ahadi za Mhe. Rais pia nikampelekea nakla, Mkurugenzi wa Ujenzi na Utunzaji wa Barabara nakla pia nimempelekea. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunapoambiwa tunawafurahisha wananchi sio tunawafurahisha wananchi tunatetea haki zao, na sisi wametuleta hapa kwa ajili hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hoja yangu mimi iko hapa Mhe. Machano hoja zake mimi sizikubali kwa sababu kwanza ananidanganya. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kipindi kilichopita na ndio maana nikasema hata kitabu cha Mhe. Waziri hakikutimia kulikuwa kuna ujenzi wa barabara nyingi ikiwemo barabara ya Karakana, na mimi kipindi kile nikamkumbusha akaniahidi tukimaliza barabara hii tunakuja barabara ya kwako. Mhe. Mwenyekiti, walipomaliza nikamwambia vipi umeshamaliza akaniambia tunajenga barabara ya Baraza la Wawakilishi, nikapata taarifa hapa wamepewa ile kampuni ya *SOGEA*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nikaona mbona napigwa danadana, najua mnanong'onezana mnasema napoteza muda lakini sipotezi muda, natoa maelezo ili nijenge hii hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema mpaka katika ilani ya uchaguzi ambayo Mhe. Machano kaijibu, hii Mhe. Machano katika ilani ya uchaguzi kama utaangalia huo ukurasa aliosema imetajwa barabara hii. Kwa hivyo, ndio nikajiuliza kuna barabara zimejingizwa katika kitabu, hata katika ilani ya uchaguzi na ndio nilipochangia nikasema Makatibu na Mawaziri wamepewa ilani ya uchaguzi. Kwa sababu serikali ya sasa hivi tunaongoza ni ya CCM bado ilani yake. Kwa hivyo, ilani imefumbiwa macho zimeandikwa katika kitabu barabara nyengine, ndio maana hapa Mhe. Mwenyekiti, nakuwa mkali katika barabara hii, ndio nikataka nipate maelezo yakutosha katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, tunayozungumza hapa tusionekane kama tunazungumza masihara Mhe. Machano alizungumza kwamba kuna barabara ambazo zilizoshinda kampuni, Kampuni ya *PRISMO* Mhe. Mwenyekiti, tulipiga kelele pale Kikwajuni Baraza la Wawakilishi tukasema kampuni hii haifai wamepewa barabara Pemba imewashinda hawajamaliza kujenga inatiwa viraka. Kampuni ile tukaja tukasikia inapewa barabara ya Fumba tukasema kampuni ni mbovu isipewe, basi ikapewe kazi kampuni hiyo. Mhe. Mwenyekiti, matokeo yake kampuni imeshindwa kazi ni hasara kwa serikali, leo tunapozungumza umasikini haiwezekani ikawa tunapitisha mambo tunajua makampuni hayana uwezo yakapewa zile kazi, matokeo yake serikali inabeba mzigo mwengine. Ndio maana nikasema hizi hoja alizojibu Mhe. Machano pamoja na urafiki wetu hajaniridhisha. Naomba maelezo ya Mhe. Waziri katika barabara ya Saateni, Darajabovu na Kwamtipura.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye sana Mhe. Hamza kwamba kuna ahadi, kuna ilani na hayo lazima tuyaheshimu. Mimi katika uwezo wangu kama Waziri nataka nimuahidi mbele ya Baraza hili kwamba kabla ya 2015 barabara hiyo tutaijenga.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anazidi kuniudhi, Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikazuia kifungu cha mipango, inaonesha mipango anayoipanga siyo anayoitekeleza. Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa kama sikosei mwaka 2003-2004 kuna mradi huu ambao juzi jina lake nimelisahu lakini rafiki yangu Mhe. Omar Ali Shehe amelikumbusha, kuna mradi huu wa Lami ya *Ro-mix* katika miradi ambayo barabara zilokuwa za majaribio, na hiyo barabara hiyo imo. Mhe. Mwenyekiti, leo inakuwaje barabara mpaka ilitiwa ile lami ya majaribio, halafu leo katika kazi haishughulikiwi zinakuja kushughulikiwa nyengine. Leo Mhe. Waziri ananiambia mpaka 2015 Mhe.

Mwenyekiti, mimi nitazidi kuwa mgumu na hapa ndio maana nikasema bajeti hii mimi sitoi *percent* yangu mpaka nipate maelezo yakutosha. Ahsante sana

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nimesema hapa tuzungumze kitu ambacho kinawezekana, kwa mwaka huu hata huo Mfuko wa Barabara kwenye programu zetu hiyo barabara haimo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe Hamza amechaguliwa kwa kipindi cha miaka 5 na hata hizo ahadi za Rais ni katika kipindi ambacho yeye atakuwa Rais ni mpaka 2015 penye uhai. Kwa hivyo, kuna tatizo gani kuahidi kwamba kabla mimi nimesema kabla ya mwaka 2015, kwani mwakani si tunaweza tukapanga hii mipango, kwamba katika mipango ya mwaka 2012 au 2013 basi barabara hii ina *priority* lakini kusema mwaka huu sitaki nimdanganye.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikawa mkali kidogo kuhusu barabara yangu kwa sababu katika mwaka huu hakuingiza kwenye bajeti kwa hiyo hana pesa, lakini bado pesa anazo kwa sababu kuna mfuko wa barabara unakuja tunayo Wizara ya Fedha. Kwa sababu mimi Mhe. Mwenyekiti, hapa Barazani sijaja leo najua ninachokifanya na ninajua mipango ya serikali. Kwa hiyo ndio maana ninapoona ninapuuzwa katika mipango hii mimi inakuwa sikubali. Lakini sasa mimi nadhani Mhe. Waziri angelinitosheleza kwa sababu barabara ile sasa hivi haipitiki, na ile barabara inapita daladala, wajawazito mambo chungunzima. Mimi nadhani angeliniahidi kwanza kuna lile eneo ambalo walilolifanyia lami ya majaribio, sasa hivi limevurugika kwa maji halipitiki basi angalau aje atengeneze kuanzia pale Kwaabasi Hussein mpaka kule juu angalau papitike, mimi nitasubiri bajeti ya mwakani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kwa kuwa katika bajeti ya mwaka huu halikuingizwa aniahidi hicho kipande kitakachobakia baada ya kurekebishiwa hicho kipande kidogo, basi katika bajeti ya mwaka 2012-2013 angalau aniahidi nije nimkamate tena katika kikao kinachokuja. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tulipokuwa tunazungumza kwenye sehemu ya mapato nimeambiwa kuna sifuri sasa nimeamua nizungumze hapa kwa sababu hapa ndio kwenye mipango na sera yote ya wizara. Katika mchango angu Mhe.

Mwenyekiti, nilizungumzia suala mapato ya SMZ ambayo inapaswa kuyapata kutokana na haya mashirika ya Muungano yaliyopo chini ya Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Haya ni pamoja kama alivyoyataja Mhe. Waziri mwenyewe *TCRA*, *TTCL*, *TPC* na hata lile la *TCCL*. Sasa nilikuwa naomba pamoja na maelezo yake kwamba amekiri kama alivyosema Mhe.

Mwanasheria Mkuu juzi kwamba hatupati kitu kwa sababu ni sehemu tu ya uendeshaji mbovu wa Muungano huu ambao umeanza tangu 1964.

Kwa hivyo, wakati tunasubiri Katiba maana yake sisi inaonekana Katiba ndio itakapokuwa kila mmoja tunapotegemea kumaliza matatizo yote haya katika kipindi hiki mpaka 2014 tulivyoambiwa Katiba mpya itakuja. Mhe. Waziri aniambie ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba anadai sehemu ya mapato haya kwa upande wa Zanzibar.

Nasema hili mheshimiwa kwa sababu katika mchango wangu nilisema chukua kampuni moja tu ya *ZANTEL* tunaambiwa kila mwaka hii inalipa leseni kwa *TCRA* dola milioni tatu, kwa sasa hivi takriban shilingi bilioni 4.5 za Tanzania. Sasa tunataka kuambiwa sehemu yetu ya mgao katika fedha hizi waziri ana mpango gani na katika ile ya *TCCA* madeni yetu na kuna fedha nyingi za Zanzibar katika mashirika haya ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aniambie ana mpango gani wa kudai fedha hizi wakati tunasubiri mchakato wa katiba mpya wa mwaka 2014.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa fursa hii kwa sababu Mhe. Jussa aligusa nilichokizungumza naomba kuweka rikodi sawa. Nilisema kuna matatizo katika usimamizi wa suala la mapato baina ya serikali zetu mbili, lakini linasimamiwa na linashughulikiwa na *JFC*. Lakini sikusema nikutokana na uendeshaji mbovu wa Muungano. Naomba tuweke rikodi hiyo sawa.

La pili nadhani kuhusu suala la kudai mapato kumwambia Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano yeye ndiye adai nadhani itakuwa ni kumpa kazi ambayo siyo ya kwake. Kazi hiyo ni ya Wizara ya Fedha kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, na nadhani kazi hiyo inaendelea majadiliano baina ya serikali mbili. Tunachoweza kumwambia Mhe. Jussa ni kwamba serikali hilo inalisimamia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba hii serikali inawajibika vizuri hapa Barazani kwa hivyo nadhani ni wajibu wetu kumuuliza Mhe. Waziri kwa ile sekta yake ambayo ana haki ya kujibia serikali nzima. Lakini pamoja na maelezo hayo nardhika na maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu tunaomba tukija mwakani tuje tuelezwe kwamba hatua hizi zimefikia wapi, sio kama nilivyosema kwa maneno kwa sababu wananchi wa Zanzibar wameshachoshwa na maneno hasa katika maeneo haya ambayo yamegusa Muungano. Baada ya hayo nasema tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii, Mhe. Mwenyekiti, hii ni Idara ya Mipango na Sera ambayo ndiyo inayosimamia mipango mizima ya wizara hii. Mimi nimesimama hapa kwa sababu maandalizi ya sera na mipango ya wizara hii hapa ndipo pahala pake. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikihoji habari ya barabara ya Mgagadu Kiwani nataka niungane na Mhe. Hamza kwamba sisi hatuzungumzi hapa kufurahisha watu kwenye televisheni. Ibara ya 35 ya Kanuni inatueleza majukumu yetu kama wawakilishi ni kutetea maslahi ya watu ndani ya Baraza hili na nje ya Baraza. Kwa hivyo, mimi kama televisheni ningemualika kwangu akaja akanimurika lakini nazungumza kwa hoja ya kanuni. Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti, mipango ya serikali ya bajeti ya barabara hii ipo zaidi ya miaka kumi nyuma, tofauti na hoja ya Mhe. Waziri ametoa mfano kwamba iko barabara ya miaka 20, hizo hazijapangiwa fedha, yangu mimi imepangiwa fedha mfululizo miaka 10 nyuma. Mwaka jana nilipokwenda mwezi wa nne wizarani Pemba niliambiwa fedha zimepangwa lakini zimeondoshwa zimepelekwa Unguja ni mipango tu na usimamizi sio suala la fedha, fedha zipo lakini usimamizi wake ni mbovu.

Pia nikasema kwamba hata *CAG* anaonesha kwamba kuna matatizo. Kwa hivyo Mhe. Waziri atofautishe baina ya fedha kupatikana na usimamizi wa mpango, hapa fedha zipo na zinapangwa. Kwa hivyo, na hizi amenambia kuwa zitakuwepo na mwaka jana zilikuwepo. Sasa naomba anambie meli 300 za mara hii vipi watu wa Kiwani watazithibitisha kwamba zitapelekwa na zitasimamiwa. Kwa sababu hofu yetu ni kuwa fedha zipo zimeshaidhinishwa lakini ni mipango mibovu baadae zitahamishwa kama ilivyokuwa nyuma. Kwa hivyo, si suala la fedha ni mipango ya wizara hii ni mibovu hasa Pemba. Kwa hivyo, naomba maelezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti yangu ya maendeleo ninazo shilingi bilioni tisa na ushei na bahati nzuri utaratibu wa siku hizi ni kwamba mnapewa, naamini katika bilioni tisa hata kama sikupewa zote lakini japo nudu nitapewa, chochote nitakachopewa nitahakikisha shilingi milioni mia tatu zinakwenda Kiwani. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. WAziri anazungumza kwenye Baraza, Mhe. Machano Othman Waziri aliyepita wa wizara hii alizungumza hapa baadae tukenda *field* Kiwani. Kwa hivyo, aliongeza zaidi *step* ya pili kwamba alizunguzma hapa mwaka jana baadae akanichukua mpaka Kiwani akenda akasema haya haya, lakini mwisho wa siku maamuzi ya serikali wakasema ah, Kiwani si muhimu tupeleke Unguja. Sasa Mhe. Waziri anambie hii kauli yake anaweza akenda na barua nikaikamata kwamba maamuzi ya

serikali yatafanya hivyo mara hii, vyenginevyo itakuwa nachukua yale ya Mhe. Machano kwamba kauli haina usimamizi. Sasa labda Mhe. Waziri anambie kwamba mara hii nitakupa na *document* ya barua nikawape watu wa Kiwani kwamba hii ndio kauli ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Kiutaratibu Mhe. Mjumbe waziri akishakusema inakuwa ni kauli ya serikali, nakuomba ukubaliane na maelezo hayo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakubali kauli ya serikali ni sawa sawa na ile kauli ya Mhe. Machano ya serikali vile vile. Kwa hivyo, naomba ufafanuzi zaidi.

Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba serikali mwaka jana iliahidi barabara ile kuijenga, lakini hazikuchukuliwa fedha kwa sababu tu, tulikuwa tukijenga Makombeni/Mkoani, tumalize huko ndio wende Kiwani, ukimaliza Kiwani uende Kangani kujenga barabara. Sasakama Makombeni hujamaliza huwezi kwenda Kiwani, kama kuna fedha za barabara unaweza kusimamisha ukapeleka katika barabara nyengine zikaendelea na kazi. Sasa hivi Makombeni imemaliza, waziri hana barabara nyengine Pemba ni ya Kiwani. Kwa hivyo, amuamini Mhe. Waziri fedha zake haziwezi kuhamishwa.

Mhe. Mwenyekiti: Anachotaka Mhe. Mjumbe ajibiwe kwamba barabara yake uhakika itajengwa isije ikawa hadithi tena kwa mara nyengine. Nilifikiri utatoa maelekezo hayo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tunayosema hapa hayana utani. Mimi Mhe. Mwakilishi kutia wasi wasi kwamba itakuwa hivi au hivi sioni kwamba kuna haja hiyo. Nimesema nina zaidi ya shilingi bilioni tisa, pamoja na umasikini wote wa serikali, lakini lazima japo nusu hizi zitapatikana, kitakachopatikana naahidi kwamba shilingi milioni mia tatu zitakwenda Kiwani na haziendi Kiwani kule kwa sababu yoyote ya kununuliwa samaki ni kwa ajili ya ujenzi ndio tunaozungumzia hapa na tutajenga kwa kiwango hicho cha shilingi mia tatu, kama ni nusu, robo, kama zitabaki tutampa yeye.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu waziri ametoa kauli mara tatu mfululizo na sote ni waungwana basi tuendelee tutakuwa mashahidi mwakani tukijaaliwa.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Sera 150,000,000
Kifungu 0501 Mamlaka ya Usafiri

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ndio mitambo yetu tustahamiliano. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa mara nyengine tena na katika mchango wangu nilizungumzia suala la *chaos* ambayo iko bandarini pale. Nilitaka maelezo hasa kwa sababu ile mipango mipya inayoandaliwa katika suala zima la usafiri wa baharini pale lime-*destruct* utaratibu wa matumizi ya barabara huku juu kutokea Forodhani kuelekea Malindi. Sasa nimeyasikiliza maelezo ya Mhe. Naibu Waziri juu ya suala hili ambaye ndiye aliyenijibu, lakini sikuridhika.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hivi sasa kwa kuwekwa pale boti tu zinazotoka Dar es Salaam na Pemba hali tunaiona namna ile, sasa panakwenda kuongezwa na Land craft ambayo tunaambiwa inajengwa eneo la pale pale tunategemea barabara ile. Sasa huku ni kuongeza msongamano sana Mhe. Mwenyekiti, hivyo nilikuwa nataka maelezo.

Huko nyuma msongamano wa abiria ulikuwa haupo kwa sababu abiria walipokuwa wakitumia lango kuu la bandari ilikuwa ni rahisi wakitoka pale wanaelekea barabara ya Malindi moja kwa moja wanaingia katika maeneo ya mji, lakini hapa pamesababisha *traffic* kubwa sana na mara nyengine unaweza kukaa zaidi ya nusu saa gari hazendi wakati boti zinashusha abiria, mimi mwenyewe nimeshashuhudia hilo. Sasa naomba maelezo, boti za abiria zimekwamisha namna ile tunakwenda kuongeza na *land craft*, hebu waziri atusaidie kuna mpango gani mwengine ili kuondosha msongamano huo angalau kwa hiyo *land craft.*

Kuna maeneo kama vile Mtoni kule Mhe. Mwenyekiti, ingeweza kujengwa kwa hizi meli ambazo zinakuja na mizigo kwa nini tunaongeza msongamano pale ambapo tayari panaleta usumbufu mkubwa kwa raia sio wa Mji Mkongwe tu, lakini raia wote wa Zanzibar wanatumia eneo la Mji Mkonwe. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza suala la kufunga barabara ndogo ile pale ambayo watu wengi wanafikiria kwamba ni chanzo cha msongamano wa magari masuala haya yalijadiliwa na taasisi tisa mbali mbali. Kwa hivyo, hayakuwa maamuzi ya Wizara ya Miundombinu kwamba ifungwe ni maamuzi ya Serikali Kuu yenyewe. Lakini sasa hapa ambapo tunazungumzia kwenye *Ram, ram* ilioko Forodhamchanga ni *one way*, ukishaingia hivi huna kwa kutokea, gari imeshapakia kule na nyengine ziko nyuma huna pakutokea, ya huku ina *entry* na *exit.*

Kwa hivyo, si dhani kwamba kama kutakuwa na utaratibu mzuri ambao umeelezwa na *control* hata polisi si dhani kama kutakuwa na tatizo hilo. Sio hilo tu ni kwamba ile *ramp* imeshajengwa, sio kama tunapanga sasa hivi

ijengwe au isijengwe, imeshajengwa kwa matumizi hayo. Kama ikitokea hivyo ambavyo inazungumzwa sisi hatuamini, basi sisi ni binadamu tuna akili na maarifa tutatafuta namna nyengine ya kusawazisha hilo tatizo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nataka sana nimuelewe Mhe. Waziri, lakini nasema na sisi haya maeneo jamani tunayatumia kwa hivyo tunaposema kitu huwa tunakielewa tunachokizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, hahitaji mtu yeyote mtaalamu kuona hali inavyokuwepo pale *chaos* bandarini hivi sasa. Nadhani hata Mhe. Waziri anatumia boti siku nyengine anaiona hali inavyokuwa pale. Sasa anatwambia kwamba pamejengwa, lakini nasema kama tulikosea tusiendelee kukosea, suala la meli hizi zinazoteremsha mizigo mimi nakubali Forodha mchanga panasababisha matatizo makubwa, hilo nalikubali wala sina matatizo nalo kabisa.

Lakini hapa palipohamishiwa napo hapana hizo njia mbili anazozizungumzia Mhe. Waziri ndio maana nikasema liko eneo ambalo linatumiwa kwa mfano, Mtoni kule ambako mara nyengine huegeshwa meli kwa dharura. Kwa nini kule kusijengwehiyo *ramp* ili hizi meli za mizigo zikapelekwa kule tukapunguza huu msongamano, huu wa boti za abiria tayari unaleta usumbufu mkubwa halafu tena kuongeza na mwengine wa meli za mizigo na tunajua meli za mizigo zikiteremsha pale hali inakuwaje, mfano hai ni ule wa pale Forodha Mchanga hivi sasa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nasema haya mengine watukubalie kwamba sisi tunaokaa pale tunawakilisha wananchi na wananchi wanalalamika. Kwa hivyo, anasema suala la boti halijapatiwa ufumbuzi tunakubali kwamba kwa sasa hivi hakuna ufumbuzi wa mkato, lakini hili la *ramp* litafutiwe sehemu nyengine angalau kuondoa usumbufu, vyenginevyo itakuwa ni *total kiosk* kama tunasema kwamba Mji Mkongwe tunataka kuwaondolea usumbufu kwa sababu ni *Heritage site* tutakwenda kuwaongezea usumbufu kwa mambo kama hayo ambayo watu hawakai wakafikiria kwa upana wake kwamba nini athari zake wanakuwa wanafikiria pale pale tu solution ya jambo moja hawaangalii *Social impact* ya lile jambo linalokwenda kufanywa. Mhe. Mwenyekiti naomba katika hili wanikubalie watafute pahala pengine ili eneo la Mji Mkongwe lisiendelee kuleta usumbufu hasa katiak eneo la kutoka Forodhani hadi Malindi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa ya Wajumbe na Mhe. Ismail Jussa kabla ya maamuzi ya kufanya *ramp* pale mwahala munne tofauti mliangaliwa, paliangaliwa Kizingo, paliangaliwa pale Bandarini ambapo kuna chelezo watu wananunua samaki, huko Mtoni anakozungumza, lakini *the feasibility* ya *project* yenyewe ikawa ni pale. Kwa

hivyo, sio kwamba hatukuangalia mahali pengine hapana, ni baada ya kuona kwamba mote mwengiine si *feasible* ama kwa gharama au hata kwa ile mandhari yenyewe. Kwa hivyo, tumefikia maamuzi yakfuanaya pale si kwa sababu hatukuangalia mahala pengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kweli nasikitika na kwamba siridhiki kabisa. Kwa sababu kama alivyosema kwamba labda atwambie kuwa serikali sasa Mji Mkongwe ufanywe kwamba ni eneo litakalokuwa kila kilichokuwa hakifanyiki kuna vyengine vinakuja kufanywa palepale kuongeza msongamano kwamba wananchi wawe hawana haki nyengine. Kwa sababu suala la kutumia njia zile Mhe. Mwenyekiti, ni haki yao wananchi na kama ninavyosema eneo hili halihudumii tu wananchi wa Mji Mkonwe lakini linahudumia wananchi wote wa Zanzibar kwa ujumla wake. Sasa nasema sijui tunahitaji maelezo gani mtu kuona kwamba pale tukipita hivi sasa ile *chaos* ambayo ipo nasema tufikirie tu, kwamba unakwenda kuongezea meli za mizigo.

Mhe. Mwenyekiti, tuichukue ile hali ilivyo sasa hivi halafu uchukue hali inayoshuhudiwa pale Forodha Mchanga unakwenda kuiongezea pale halafu tujaalie hali ya eneo lile litakuwaje Mhe. Mwenyekiti, halafu anasema pana *in and out*, labda Mhe. Waziri anisaidi hii *in and out* iko wapi. Kwa sababu njia imefungwa, njia ni *one way* tu zote, Mji Mkongwe wote sasa hivi umefanywa kwamba una njia za *one way. Chaos* tunayoiona sasa hivi inatutosheleza Mhe. Mwenyekiti halafu tunakwenda kuongezwa nyengine bado naomba maelezo katika suala hili Mhe. Mwenyekiti, sitaki tufikishane pahala nikasema nazuia fungu lakini naomba maelezo vipi serikali itaweza kusaidia kupata ufumbuzi wa suala hili si kwa wananchi wa Mji Mkongwe tu lakini ni kwa wananchi wote wa Zanzibar ambao wanatumia eneo hili.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sijui kama nina maelezo zaidi ya hayo, lakini nasema maamuzi ya pale ni baada ya hayo ambayo tumefanya kuangalia sehemu nne tofauti na kwamba maamuzi ya kufunga ile njia yalifanywa na taasisi tisa. Serikali za Mitaa, watu wa Mazingira, Mji Mkongwe ambao ndio wamiliki wa ule mji. Kwa hivyo, sisi hatungeweza kupingana na taasisi nyengine nane, ni maamuzi thabiti ambayo tumeyakubali.

Kama nilivyosema mimi siamini hivyo ambavyo anasema, kila mtu ana muongo wake na anavyoamini, nimesema kama ikitokea kwamba hayo yanayozungumzwa kwa sababu *ramp* imeshajengwa sio kwamba tujenge au tusijenge, raimp ishejengwa na sisi tumejenga kwa kuamini kwamba hatutakuwa na tatizo hilo, sasa ni namna mbili ya kuona, huyu anaona nyeuzi

huyu anaona nyeupe na kwa sababu imeshajengwa acha tu-*practice* ikitokea vyenginevyo nasema sisi ni binadamu tuna maarifa tutaangalia vya kufanya.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika hili sipati jawabu imekuwa ile hadithi ya nyimbo 'nafanya hesabu sipati jawabu'. Lakini nadhani nikubaliane na Mhe. Waziri kwa hiyo kauli yake ya mwisho kwamba tuendelee lakini hoja ya kwamba, kama alivyosema yeye tuone hali itakavyokuwa na nadhani yeye swahibu wangu sana Mhe. Waziri itafika wakati nitakwenda kumchukua nikamuoneshe hiyo hali ninayoizungumza mimi ya *chaos* ili kama kunahitajika ku-*review* tu, lakini anipe *commitment* kwamba hali hii ikiwa hairidhishi basi ndani ya mwaka huu wa fedha kwa hatua za kiutawala watachukua hatua wao kuona wanafanya marekebisho katika suala hili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia eneo hili nilizungumzia mikataba ya *Seagull,* nikasema kwamba Wazanzibari wanafanya kazi bila ya mikataba wanapewa barua za kujitolea. Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri amenijibu, lakini ameelekeza tu kwamba Wazanziibari wenyewe ndio waende kule wakadai mikataba. Ninachotaka mimi sasa serikali itoe tamko chini ya Mamlaka hii kwamba *Seagull* waandae mikataba ionekane na serikali na baadae wawakilishi pengine Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wakaiona kuwa mikataba ipo sio kwamba Wazanzibari wenyewe ndio wakadai mikataba kwa sababu Wazanzibari wana shida wanafanya kazi hata bila ya mkataba.

Sasa serikali itoe tamko kwamba *Seagull* na kampuni nyengine waandae mikataba ya mabaharia wetu ili haki itendeke na usalama wa Wazanzibari upatikane, vyenginevyo kwa kuwambia Wazanzibari wao ndio wahakikishe wanapata mkatana hawatasubiri mkataba, shida haisubiri mkataba Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba tamko la wizara.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, *Act* iliyounda *Zanzibar Maritime Authority* inaelekeza hivyo, kwanza mabaharia na wamiliki wa vyombo lazima kuwe na mkataba. Tatizo lililopo kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, mtu anatafuta kazi anakubali kw amasharti yoyote wanakwenda taratibu hakuna tatizo, lakini likitokea tatizo ndipo Mamlaka inapoambiwa kwamba mbona hamjafanya hili?

Yanafanywa kinyume nyume, tutahakikisha kwamba wamiliki wa vyombo wote iwe *Seagull, Zamarine,* wana mikataba na wafanyakazi wao katika meli. Hivi ninavyokwambia sisi tuna *standard format* ya *contract* na tutapenda waichukue hiyo, ama kama wana yao ni nzuri zaidi kuliko yetu sisi basi tutai-

adopt. Lakini tutahakikisha kwamba wamiliki wa vyombo wana mikataba na wafanyakazi wao katika meli zao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0501 Mamlaka ya Usafiri Baharini	128,000,000
Kifungu 0601 Idara ya Anga	806,000,000
Kifungu 0701 Idara ya Ujenzi	

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi. Kwa kweli wakati nachangia hapa nilizungumzia juu ya Idara ya Utunzaji na Ujenzi wa Barabara unavyoathiri mazingira hasa katika maeneo ya Makaani kule kwa kuchimba mashimo mazito. Nilieleza kwamba kuna asilimia kumi ya kila mradi inachangiwa kwa ajili ya utunzaji wa mazingira, nikamuomba Mhe. Waziri anieleze fedha zile zinakwenda wapi kwa sababu mashimo yamekuwa makubwa sehemu za liko la Vumba, Makoba, liko la Mjini, mashimo yamekuwa makubwa sana. Sasa je, ile asilimia kumi ya kila mradi inapelekwa wapi kwa ajili ya kufukia yale mashimo.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, nikamueleza kuna kijipande kidogo Dodeani mpaka sehemu ya mgodi wa uchimbaji wa matofali, pale pana kipande ambacho hakipitiki kiasi ambacho wapiga kura wa Jimbo la Ole analotoka Mhe. Waziri na majimbo mengine ya Pemba wanapata shida sana kuchukua matofali yao. Je, ni lini atakijenga katika kiwango cha lami ili matofali yapatikane kirahisi kutoka Makaani uwandani mpaka Majimbo mengine likiwemo la Mhe. Waziri.

Halafu nilizungumzia barabara ya Vikunguni kuwa imo katika ahadi ya rais, itajengwa lini katika kiwango cha lami?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi anazungumzia asilimia kumi kama fiee ya uharibifu wa mazingira kwa kuchimba kifusi. Mhe. Mwenyekiti, masuala ya mazingira yako katika wizara inayozungumzia mazingira, Wizara ya Miundombinu hawashughuliki na kutoza *fee* yoyote au hata kutozwa na kupeleka mahali pengine. Sasa kama kuna watu wengine wanachukua kifusi sio serikali hiyo mimi siitambui, lakini kama serikali hatuna *fund* ambazo zimewekwa kwamba ukienda ukichimba kifusi mahali utoe. Tunachofanya sisi ni haya yafuatayo:-

Kwanza tunachukua kifusi katika mahali ambapo ni ardhi ya serikali, lakini vile vile tukishafanya hilo shimo na sasa hivi tunashirikiana vizuri sana na Idara ya Mazingira, tunafukia kama ilivyokuwa na tunapanda miti. Hiyo imejidhihirisha wakati wa ziara ya Mhe. Rais katika sehemu hiyo hiyo ya Vitongoji

tumekwenda na Mhe. Rais amesifu sana, mahali pamechimbwa huamini kama pamechimbwa na mashahidi ni mawaziri waliokuwepo. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Mhe. Waziri wa NChi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kitabu hiki kinaonesha yale mazingira hasa tuliyokwenda kutembelea. Miti imenawiri *ever green* hilo ni moja.

Lakini la pili ni kuhusu barabara ya matofalini. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli barabara hii ni muhimu sana katika maisha ya watu, lakini ninachoelewa mimi ni kwamba, Wilaya ya Wete na Wilaya ya Chake-Chake wanagombea pale mahali, kila mtu anataka kukusanya ada na wameweka ada zao kabisa ***cubit*** mita moja ambayo inatoa matofali si zaidi ya 70 utoe shilingi karibu laki mbili ambayo ni hesabu iliyokuwa haifanyiki.

Kwa sababu hayo matofali yote ukiyatoa kwenye *cubit* mita moja ya lile pande la ardhi huwezi ukauza ukapata hizo shilingi laki mbili, ama makosa yawe yamefanyika katika mahesabu. Lakini ninachofahamu mimi ni kwamba, barabara zile zimetenga pesa kwa ajili ya kuzitengeneza na sisi Wilaya ya Wete katika Jimbo la Ole wamepewa shilingi milioni nne, kwa nini basi pesa kama hizo kwa utaratibu ambao nimeueleza wasinunue mafuta halafu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ikawasaidia. Kwa hivyo, mimi nasema ni utaratibu tu na kama kweli.

Mambo si hayo tu Mhe. Mwenyekiti, wanaochukua matofali yale wana magari makubwa na mazito lakini wanaweza wakakuta shimo kubwa la kuweka kifusi kidogo tu hawafanyi hivyo. Magari wanayo hawawezi wakachukua kifusi wakafukia shimo wanakwenda hivyo hivyo maana yake ni kwmaba hata wao wenyewe hawajionei huruma na magari yao. Kwa hivyo suala hili la kujenga barabara zote mimi nasema tunaweza tukatengeneza lakini kwa mashirikiano hasa kama hili ambalo pale kuna *income* inakwenda wilayani.

La tatu Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu barabara ya Vikunguni hebu anikumbushe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Mhe. Rais alitoa ahadi ya kuijenga barabara inayotoka Vikunguni mpaka Mjengo wa Banda Matrekta pale katika kiwango cha lami wakati anatoa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri kwa Skuli ya Vikunguni, rais mstaafu. Je, ahadi ile ya rais mbona mpaka sasa hivi haijatekelezwa?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa barabara una hatua mbali mbali, lakini huwezi ukaweka lami kabla hujaweka kifusi. Sasa hivi barabara ile tumeitengeneza ina kifusi hatua

iliyobakia ni lami hiyo inahitaji fedha. Sio kwamba rais ahadi zake anazotoa hazitekelezwi, lakini kama nilivyosema ahadi za Mhe. Rais ziko nyingi na inategemea hali ya fedha ilivyo sio kwamba hazitekelezwi na kipindi ni cha miaka mitano. Mimi naamini kabisa kwa ari ya Mhe. Rais na anavyopenda kuwa ahadi zote ambazo ameto zitekelezwe basi ahadi hizo kabla kipindi chake kumalizika kama alitoa ahadi ya kuwekwa lami itakuwa imewekwa lami. Lakini sasa hivi hatua kubwa ya kuweka kifusi na njia kupitika tayari hiyo ipo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe kwa mujibu wa Kanuni kifungu cha 96(3) hoja ziwe tatu sio watu wawe watatu na hoja tatu zimetimia kwa hivyo tunaendelea.

Kifungu 0701 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara 1,004,000,000
Kifungu 0801 - Idara ya Usafiri na Leseni

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuheshimu kiti chako lakini nadhani hata ile iliyopita hoja ilikuwa ni moja tu ya Mhe. Saleh hazikuwa hoja tatu. Lakini naomba niendelee hapa kwenye Idara ya Usafiri na Leseni.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia mbali ya lile pendekezo nililotaka wanipe kauli ya kuwa na mradi wa uhakika wa kuleta *public transport* ya kisasa katika mji wetu, lakini sema katika kipindi hiki tuelezwe utaratibu gain utachukuliwa ili kudhibiti hii vurugu ambayo tunaiona katika suala zima la *public transport* iliyoko sasa hivi mjini ya daladala. Tumepewa maelezo hapa lakini nilikuwa nahitaji maelezo ya ziada, kuna utaratibu gain wa kuona kwamba hawa watu wanaokiuka sheria za usalama barabarani na idara hii ndio inayohusika na mambo ya utoaji wa leseni na madereva na mambo mengine, kuona kwamba wale madereva wazembe ambao wote wameishia katika daladala kwamba wanapofanya makosa wananyang'anywa leseni au kudhibiti katika hatua nyengine ili haya mambo ya kupoteza roho za watu kila siku yanayoendelea katika barabara zetu yaweze kusita. Naomba maelezo zaidi katika suala hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri Idara ya Leseni na Usafiri ina Kamati ya Usalama Barabarani na ni kamati hii ambayo inatekeleza kanuni na sheria. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inadhamiria kama kanuni zenyewe hazitoshi kwanza kuzi *reinforce*, lakini kuna vitu vyengine ambavyo ni *direct.* Kwa mfano, gari imepewa *rout* kutoka Bububu/Hospitali au kutoka Darajabovu/Hospitali, lakini ikafika Darajani au Michenzani kwa Khamis Machungwa pale anakwambia mtu mimi siendi huko, kwa hivyo ama uteremke hapa au wende Darajani, hizo

nimeshamwambia mimi Mkurugenzi. Kam akuna ushahidi na uhakika hhuyo ni moja kwa moja ku-*panelize,* anyang'anywe leseni japo kwa kipindi fulani.

Mhe. Mwenyekiti, au suala la mtu kuteremshwa Michenzani akambiwa apande gari nyengine watu wameshaachwa na kupondwa na gari kabisa na kuvunjika miguu. Sasa kama kanuni hazitoshi tutazi-*reinforce* lakini tuhakikishe kwamba usalama barabarani unazingatiwa vya kutosha, hatuwezi kila siku madaladala haya na makondakta na madereva wasiozingatia maisha ya watu ikawa kila siku tunakuwa na vilema tu.

Mhe. Mwenyekiti, namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba suala hili na mimi kamati hii itapokutana mara hii nitakutana nayo kuwapa maelekezo namna ya kufanya na kama wanataka msaada wengine wote, basi tuutafute ili sheria na kanuni za usalama barabarani ziweze kutunzwa na kutiiwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa ufafanuzi wake naomba tuendelee.

Kifungu 0801 Idara ya Usafiri na Leseni 370,000,000
Kifungu 0901 Idara ya Uendeshaji

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwenye Idara Utunzaji na Ujenzi wa Barabara nilipiga buti lakini hoja yangu imeelekeza katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika michango niliomba tuunde Kamati Teule ya Baraza. Hoja nilizozungumza katika muundo wa tume ile ili kuchunguza na kupata ukweli. Kama Mhe. Waziri alivyosema kutoa maoni, kushauri, kuuliza, sio kumkomoa mtu au kumchukia mtu, lakini tunajenga serikali yetu, tunajenga usalama na haki za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika suala la Idara ya Uendeshaji na Utumishi nilizungumzia suala la mfanyakazi wa Idara ya Anga. Katika kifungu 06 huku waheshimiwa walikuwa wanapiga zogo ukakipitisha mimi sijawahi kupiga buti, kwa hiyo ndio maana nikaamua nije nikizuie kwa huku mbele, nimetumia uzoefu.

Mhe. Mwenyekiti, pale kuna mfanyakazi ambaye nilileta hoja kwamba wale waliamua kufungua Kampuni ya *Zanzibar Emission Porters Service*
yaani kampuni ya ubebaji wa mizigo. Nilisema kwamba mama yule alishirikiana na mumewe, mumewe alikuwa ni Afisa wa Jeshi la Usalama ambaye amestaafu ameletwa pale Uwanja wa Ndege kwa ajili ya *security*.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupeleka yale maombi ya wakakubaliwa wakaambiwa fanyeni hivi, tafuteni sare, tutakufanyia *registration* zote ninazo hapa. Mhe. Mwenyekiti, tatizo lililojitokeza kwamba wale walikuja kupigwa pute na sitaki kusema na wakubwa, lakini walikuja kupigwa pute na viongozi wa Idara ya Anga. Matokeo yake yule aliyebuni mradi akaja akaonekana kwamba yeye atafaidika matokeo yake wakubwa ndio wakauchukua mradi ule.

Mhe. Mwenyekiti, huyu mzee ambaye alianzisha hii kampuni ndio maana nikasema kwamba yeye kaajiriwa pale kama *security officer* akaondolewa kabisa sasa hivi kapelekwa UUB kwenda kukaa getini Afisa Usalama huyo. Lakini jengine na huyu mkewe anaendelea kusulubiwa baada ya kuona muda mrefu pale anasumbuliwa akaamua kwenda kusoma, kasoma mambo ya uhasibu, kasoma mara ya kwanza, kasoma mara ya pili, sasa hivi anasoma mara ya tatu. Ndio maana nikatoa mfano kwamba sasa hivi ukimuangalia hata uso wake umegeuka kama wa mwanamme kutokana na ile adha ya maisha anayoipata kukaa pale kazini anakuwa anaona tabu. Matokeo yake kawekwa kama Afisa wa Mazingira pale Uwanja wa Ndege na hakupewa nyenzo yoyote ya kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema hapa kuna jambo la kuunda tume. Kwanza hii kampuni iliyokuwepo Uwanja wa Ndege inayobeba mizigo haiko kihalali na tukenda mpaka kwa Mrajis tukakuta *document* ambazo kampuni iliyoomba mwanzo na wao wakaja wakawapiga pute wale.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema tuunde tume ili twende tukachunguze hili suala. Mhe. Mwenyekiti, kama kweli tunataka tutumie Serikali ya Umoja wa Kitaifa iwe mawaziri na *backbenchers* tusaidiane hii kazi, tupeni hii kazi tukaifanye mnaona tabu ya nini. Kwani kukubali kuunda tume sisi tunamsulubu nani. Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaposema tunataka tuunde tume kuna jambo tumeshaliona. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nimejenga hoja yangu wakati wa kuchangia nilizungumzia na huyu mwekezaji ambaye wizara inanunua kifusi kutoka kwake. Huyu kauziwa kware mbili na wizara au idara lakini iko chini ya wizara hii, lakini vile vile anatumia kifusi hichi sasa hivi kwa kuiuzia serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi pamoja na mahesabu aliyonipa Mhe. Waziri sitegemei kama huyu atakuwa anakula hasara kuliko serikali ingelitumia kware zake. Ndio maana tukasema Mhe. Waziri ameshatupa maelezo lakini hajaturidhisha, twende tukajiridhishe na mahesabu, kama kifusi tutachimba wenyewe serikali gharama yake itakuwaje. Kama sasa hivi tunanunua kwa mtu gharama itakuwaje.

Lakini ukiangalia hata huu mradi kama tulikuwa tunauharakisha, mradi umeanza tokea mwezi Februari, leo tuna Julai mradi haujesha barabara sijui kilomita 4 pale. Ndio Mhe. Mwenyekiti, tukasema tuna hofu. Lakini huyu huyu katumia kifusi hichi kwa kwenda kufukia bahari bila ya kibali chochote cha serikali. Ndio maana tukasema huku kauziwa mashimo ya kifusi, huku kifusi kile kile tumekinunua, huku katumia kifusi kile kile kwenda kufukia bahari, kaharibu mazingira, kachukua eneo la hoteli ya utalii. Mhe. Mwenyekiti, tunakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hii kama sijakubaliwa kuunda tume nitakuja kuzuia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa sababu yule ni mwekezaji wa utalii. Kama sikuruhusiwa hapo nitakuja kutaka iundwe tume katika Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa sababu kule ndio kwenye uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, ili tusipate tabu huko niruhusuni tuunde tume tukayachunguze haya yote, tutailetea serikali taarifa nzuri hatutomchafua mtu. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa maelezo ya Mhe. Mwakilishi amezungumzia kuhusu kuundwa tume teule. Lakini kwa kuwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ipo na ni kamati ambayo inatoa taarifa zake kwa Baraza hili tukufu, basi kwa nini tusiiachie Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi ikafanya uhakiki wa kina na ripoti yake ikaja hapa Barazani tukaijadili.

Kwa hiyo, naona ni vyema kwa wakati huu kabla ya kuunda tume teule ambayo itaongeza gharama na shughuli nyengine na kamati ya kisekta ipo na ina uwezo wa kufanya shughuli hii, kwa nini tusiiachie kamati sekta ikafanya tathmini ya kina na baadae ilete ripoti yake kwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namstahi sana mrithi wangu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa ufafanuzi wake.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama tunataka kusikiliza maelezo ya viongozi wetu wa kitaifa naanza Rais wa Zanzibar uwajibikaji, ikisha pia maelezo ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais uwajibikaji, Makamo wa Kwanza wa Rais uwajibikaji. Mhe. Mwenyekiti, inaonesha lugha zinagongana, sisi wasemaji wa wananchi tuna hofu, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi siiamini. Mhe. Mwenyekiti, siiamini kwa sababu kwanza katika ripoti yake hakuandika lakini kachukue *hansard* ya Mwenyekiti wa Kamati kasifu tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ndio maana nikakosoa hichi kitabu. Humu katika kitabu hichi maelezo yaliyonitosheleza ya Shirika la Bandari peke yake, wote waliobakia hapa wameona sisi hatuoni mbumbumbu wametuletea kitabu hichi. Tunataka tumsaidie Mhe. Waziri. Hapa Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi hii kazi hawaiwezi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitika kidogo kwa sababu Mhe. Mjumbe anasema Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi haiamini. Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote hamna hata mtu mmoja wa nje. Yeye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa hivyo naomba aseme hapa kwamba yeye kama ni mwakilishi hawaamini wawakilishi wenzake wanaofanya kazi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hii ndio raha ya kuwa na wanasheria ndani ya Baraza. Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi nimesema siiamini kwa sababu moja tu kwa suala hili. Ripoti yao wameshaleta hamna kitu. Mwenyekiti kachangia mwenyewe, maana yake labda ingekuwa imekosewa, lakini Mwenyekiti kachangia mwenyewe kasifu kila kitu, tutawapa kazi hii wataifanya vipi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi narejesha kauli yangu Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naiamini lakini kwa hili kamati hii haiwezi kututendea haki kwa sababu maelezo yao tumeshayapata, ripoti ya kamati ipo na maelezo ya Mwenyekiti yapo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, suala hili limekuja hapa katika kikao hichi, kwa wakati huo Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi haijafanya hii shughuli. Sasa kwa sababu hili suala limekuja hivi sasa huwezi kusema kwamba Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi huiamini mpaka wewe mwenyewe iwe huwaamini wawakilishi wenzako.

Kwa maana hiyo ninayosema kwa sababu Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ndio yenye shughuli hii na kwa sababu baada ya Baraza hili kiutaratibu kamati zinakwenda katika kazi wapewe Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ili iende katika kazi. *Specifically* moja katika kazi zao itakuwa ni hii ambapo hapo nyuma walikuwa hawana kazi hii.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nataka nifanye hiyo kazi ya kamati. Mhe. Mwenyekiti, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukikwambieni kuna kitu tunataka kukifanyia kazi mna mambo ambayo nyinyi hamuyajui. Mimi nataka nikwambieni kwamba hapa ndio maana nimeunganisha hizi hoja zangu. Ukiangalia mimi nazungumza huyu mama

ambaye amesomea fani ya uhasibu lakini amepelekwa kwenye maeneo ya mazingira ambayo si fani yake. Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, ina maana huu ni unyanyasaji. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, inaonesha na ndio hofu yangu ilipo kwamba labda kuna mbinu za hawa kutolewa kuingizwa wengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mtataka niseme kitu ambacho pengine kitakuwa si kizuri. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hichi kuna matatizo mengi hayakuandikwa katika eneo hili ninalolizungumza na ndio hii hofu yangu ninayotaka sasa tuunde hii kamati teule tukaangalie.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika kitabu hichi tumekwenda bajeti ya mwaka 2010/2011 hawakuonesha humu masuala ya uajiri. Ndio maana tukaona hawa wengine wanataka kuondolewa kazini ili waajiriwe wengine. Mhe. Mwenyekiti, naomba unisikilize.

Mhe. Mwenyekiti, humu kwa sababu nina hofu unajua nimefanya hivi ili haya mambo tuyafanye baadae tulete ripoti, lakini inaonesha mnataka tutoe hofu yetu hapa.

Mhe. Mwenyekiti, humu huyu mama inaonesha kwamba pale sehemu aliyosomea anataka kuletwa mtu mwengine na kwa sababu Mhe. Waziri humu hakutueleza masuala ya uajiri.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika bajeti hii kuna uajiri umefanyika kinyume cha taratibu. Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wameajiriwa sasa hivi wapo skuli wanasoma. Hili Mhe. Mwenyekiti, ni halali. Kuna wafanyakazi wameajiriwa mara mbili humu humu ndani ya serikali hii. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mkitaka mambo haya tusiyaseme tukayaseme wapi, tukiunda kamati mambo haya tutayaleta.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nataka niseme, najua kwa kura nitashindwa, najua kwa sheria mtanishinda. Lakini Mhe. Mwenyekiti, maneno yote ya viongozi wetu hapa tutakuwa hatuyatendei haki, uwajibikaji hapa haupo.

Mimi nataka maelezo kuna sheria gani inayomruhusu mwanafunzi aajiriwe wakati bado anasoma, kuna sheria gani inayomruhusu mtu aajiriwe mara mbili serikalini. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikataka tuunde tume tuna mambo mengi tunayajua.

UTARATIBU

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma na ile ya Mhe. Waziri hazina utata iwapo Mhe. Waziri angekubali kwamba Kanuni ya 117 inasema "Mtoa hoja wa kamati teule atakuwa ni miongoni mwa wajumbe wa kamati hiyo."

Kwa hivyo, tunaweza tukairuhusu Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi lakini mtoa hoja na yeye akawa ni mjumbe wa kamati hiyo kwa mujibu wa kanuni.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachotaka kusema kwamba kamati teule inaweza kuteua Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao Mhe. Mjumbe hawaamini kwa alivyoeleza. Lakini kwa sababu kamati teule inawateua Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi aliyetoa hoja si lazima awe Mwenyekiti, anaweza akawa Mjumbe.

Sasa ninachopendekeza mimi ni kwamba Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ipewe dhamana hiyo na kwa mujibu wa kanuni zetu mjumbe anaweza akaalikwa wakati wowote. Kwa hivyo, yeye awekewe *option* ya maagizo, hayo maelezo yake yote atayatoa huko.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na msaada mkubwa wa Mhe. Hija Hassan Hija nakubaliana na maoni aliyoyatoa sio mtu mwengine. Kitu nitakachokiomba katika hadudi rejea yale yote niliyokuwa nina hofu nayo yaingizwe nisije nikapewa suala moja. Kaangalieni *hansard* maeneo yote niliyokuwa na wasi wasi nayo yaingizwe ili kuweka mstari sawa, vyenginevyo bado nitaomba kamati teule.

Kwa sababu Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ina maeneo yake machache. Sasa kitu ninachokiomba yale maoni yangu kwa sababu mimi ndio niliyeleta hoja yaingizwe na nitajitahidi kuyasimamia ili sasa ionekane kwamba kweli tuko katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi nilete hoja yangu hapa. Katika mchangio wangu mimi nilizungumzia kwamba naazimia kulizuia hili fungu la Idara ya Utumishi na Uendeshaji kwa sababu ya fedha ambazo waliwahi kuomba za ujenzi wa jengo la Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wakati huo katika eneo la Mtoni. Waliomba shilingi milioni 100 wakaingiziwa milioni 49.1 Mhe. Waziri kazitolea ufafanuzi hapa kwa namna walivyozitumia. Lakini nikawa na shaka na lile eneo.

Nilimwambia kwamba nilitaka kujua kile kiwanja alichokiombea pesa ujenzi wake ulifikia wapi, hakuzungumza Mhe. Waziri kwenye hilo hapo. Sasa nataka kujua kile kiwanja cha Mtoni ambacho walikiombea pesa alisema kimefanyiwa uhaulishwaji. Nilikuwa nataka kujua ule utaratibu uliotumika katika kukihaulisha kile kiwanja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kiwanja cha Mtoni kinachozungumzwa kilikuwa ni kiwanja cha Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ambayo sasa ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, lakini pale kilipo ilionekana kabisa kwamba wizara haiwezi kujenga makao makuu yake kuna sababu za msingi. Moja ni mbali mno sana na mjini, lakini kama hilo halitoshi pale ni karibu sana na *Depot* ya mafuta.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ili kutafuta mahala pengine pazuri zaidi tukaona kwamba kwa nini tusiwaambie watu wa ardhi ambao wanamiliki ardhi wakatupa eneo jengine. Kwa hivyo, eneo jengine likapatikana la Mazizini lakini kwa masharti kwamba yule atakayepewa pale basi asaidie ujenzi wa huko atakakopewa.

Kwa hivyo, *process* zote za kisheria Mhe. Mansoor Yussuf Himid ni shahidi, wizara ikahaulishiwa kutoka pale kwenda pale. Hivi sasa ninavyokwambia kwamba tuna waraka kabisa wa kumiliki kiwanja kilichoko Mazizini mita 60 kwa mita 60 na hapa ndipo ambapo tutakapojenga wizara yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kiwanja kile sasa ni cha serikali lakini kwa utaratibu ambao umependekeza serikali jengo hilo moja litakuwa na wizara mbili hatujajua ni wizara gani gani, lakini moja itakuwa ni miundombinu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, fedha ambazo zilitakiwa zitumike kujenga pale na huyu ambaye amepewa pale pahala si suala kwamba atupe fedha mkononi na hakuna fedha mkononi iliyotolewa hadi sasa. Ni kwamba tukiwa tayari atujengee mpaka *level* fulani ya nyumba yetu na hatua hiyo bado hatujafika. Hatuna michoro, kiwanja tunacho na hatuwezi kuwa na michoro mpaka tupate fedha za kutosha kwa sababu hiyo michoro yenyewe nayo ina gharama zake.

Kwa hivyo, si suala la kwamba kuna pesa zimetolewa pajengwe ofisi lakini ofisi haijajengwa, hakuna fedha iliyotolewa. Makubaliano ni kwamba tukiwa tayari kujengewa basi tujengewe na huyu ambaye ametoa pahala pale badala yetu atujengee mpaka *level* fulani ya nyumba, kama ni *foundation* au kama ni ghorofa moja. Lakini nasema kuna masharti na makubaliano, hayo makubaliano bado hayajatekelezwa, hatujawa tayari sisi kujenga hatuna fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu kama nilivyosema kwamba sasa hivi ujenzi wa kila kiwanja kimoja ni kwa ajili ya ofisi mbili za serikali. Kwa hivyo mpaka serikali itakapoona kwamba sasa hivi wizara hii na hii na utaratibu ukawekwa hapo ndio tutatumia hiyo fedha ambayo tumekubaliana kwamba huyo aliyepewa kiwanja cha Mtoni atujengee hapo. Haya ndio maelezo ambayo naweza kuyatoa na ndio sahihi na ndio ninayoyajua.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Mwenyekiti, mimi naona Mhe. Waziri anajikanganya. Katika majibu yake hapa alitwambia kuna shilingi milioni 200 zipo tena zikiwa salama za uuzwaji wa kiwanja kile, sasa hivi anajibu kwamba hakuna pesa iliyotolewa. Kuna maelekezo ya kwamba huyo mtu waliyempa watakapokuwa wao tayari ndio wakajengewe kwa utaratibu maalum. Mimi nilikuwa nataka kujua uhaulishwaji wa mali za serikali kutoka taasisi moja kwenda nyengine au kutoka kwenye taasisi kwenda kwa mtu binafsi kuna taratibu zinazofuatwa. Nilitaka kujua ule utaratibu ulifuatwa, hakuwa amenijibu Mhe. Waziri vizuri.

Lakini hii mali ni ya serikali, huyu mtu unayesema mnakubaliana aje akujengeeni jengo ndio utaratibu wa kiserikali huu kwamba wizara inahitaji jengo basi inatoa mali yake kwanza, bwana eee njoo utujengee huku. Mimi nahisi pana tatizo hapa. Kwa hiyo, nirudi kwa Mhe. Hamza Hassan Juma kama alivyozungumza na mimi nataka kwenye hili ni vyema tupeleke kamati kwa sababu pana utata hapa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, wakati nafanya majumuisho kwa niaba ya Mhe. Waziri nilieleza namna ya uhaulishwaji wa kiwanja hichi. Napenda nikiri maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri wangu.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo tuliyoyatoa ni kwamba kiwanja hichi namba 181 kilikuwepo Mtoni kilikuwa ni milki na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, hivi sasa ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo yetu ni kwamba kiwanja hichi kipo na sisi wenyewe Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano baada ya kutafakari kwa kina tukaona eneo lile sio muafaka kwa kujenga ofisi ya makao makuu. Tuliiomba serikali kuu azma na nia yetu hiyo ya kukiondoka kiwanja kile, serikali kuu ilitukubalia maombi yetu ikaielekeza wizara husika ya Ardhi itupatie kiwanja chengine. Maelekezo tuliyopatiwa ni kwamba hapo mnapoondoka atakayepewa hiyo ardhi lazima alipie, malipo hayo ndio hizo shilingi milioni 200 na fedha hizo nimeeleza kwamba ziko salama kulingana na mkataba tuliokubaliana sawa sawa na maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri wangu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nikariri baadhi ya barua zilizohusika katika uhaulishwaji huo. Mhe. Mwenyekiti, siku ya Jumanne tarehe 5 Oktoba, 2010 Waziri wa wakati huo alimuandikia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi azma ya uhaulishwaji wa hakimiliki ya kiwanja namba 181 kiliopo eneo la Maruhubi. Mhe. Rais alikubaliana na ombi hilo na siku ya tarehe 11 Oktoba, 2010 tulipata majibu.

Baada ya majibu hayo na maelekezo yaliyoelekezwa kwa wizara husika, siku ya tarehe 20 Oktoba, 2010 tuliingia mkataba kwa mujibu wa maelekezo na makubaliano na huyu mwekezaji aliyepewa kiwanja hichi.
Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huu umekamilisha taratibu zote kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1992 ya sheria ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hakuna hofu wala sioni haja ya kuunda kamati.

Mhe. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, hoja yangu nimeanza kuuliza utaratibu uliotumika kumpa mtu huyu. Kwa sababu kiwanja hichi ni mali ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa wakati huo. Kama utakumbuka walikuwa wanakaa UUB pale kuweka magari yao, ma-*caterpillar* yao. Kama wao wizara walikuwa wameshindwa kile kiwanja kwamba hapafai kwa mujibu wa kujenga, ingawa kabla ya kufanya hivyo mimi najua kulifanyika uchambuzi yakinifu ili kuweza kujua wataweza kujenga lile jengo au hawatoweza kujenga. Ndio maana wakaja wakatuomba pesa hapa Barazani ili waidhinishiwe kwa ajili ya ujenzi wa jengo lile pale. Wamefikia pahala wameghairi kwa nini wasiwarejeshee wale wale watu wa Idara ya Barabara wakaendelea kutumia pale.

Lakini huyu ambaye wamempa utaratibu hawakuufuata. Kwa sababu sisi kama Kamati ya *PAC* tumeshakwenda pale lakini haya ambayo yanaelezwa hapa leo hatukupewa. Tumekwenda pale hakuna mkataba zaidi ya kuambiwa waziri ndio aliamua kwamba kiwanja hichi sasa anampa. Hata huyo mtu wenyewe hakuna barua yake ya maombi kwamba anaomba lile eneo pale. Kwa hivyo, sijui ilikuwaje wizara ikafikiria tu kwenda kumpa zawadi mtu huyu. Kwa sababu hivi naona umemtunukia zawadi mtu ambaye alikuwa hataki kitu.

Mhe. Mwenyekiti, ukitazama maelezo ya Mhe. Naibu Waziri hizo barua ukizitazama ni za waziri kaomba, anasema kapewa ruhusa sina uhakika Waziri wa Ardhi kahaulisha. Waziri wa Ardhi umemuandikia barua ahaulishe kama waziri kahaulisha, lakini taratibu za kisheria za uhaulishwaji ndio ninazozitaka mimi zilifuatwa. Tukizitazama hizi taratibu kitabu tunacho hichi *procurement* yake ipo zilifuatwa? Hapakufuatwa kitu. Sasa hiyo ndio hoja yangu utaratibu haukufuatwa wa uhaulishwaji. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo katika hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tunalolizungumzia hapa ni suala linalohusiana na umiliki wa ardhi ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria za Ardhi, Sheria ya Mwaka 1992 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndie mmiliki wa ardhi yote ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mamlaka aliyopewa kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi hii yeye ana uwezo, haki na fursa ya kutoa maelekezo chochote anachokifanya katika utawala wa haki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndiye mmiliki halisi wa ardhi ya Zanzibar. Baada ya kwamba yeye ni mmiliki ameridhia, jamani tunataka utaratibu gani. Tunachokiongelea hapa ni suala la sheria, huu ndio utaratibu. Utaratibu umemuomba mwenye mali amekubali tunahitaji utaratibu gani jamani zaidi ya hilo.

Kwa mujibu wa sheria ya Zanzibar imeeleza ardhi yote ya Zanzibar mwenyewe ni Mhe. Rais na yeye Mhe. Rais tumemuomba ametukubalia tunahitaji utaratibu gani jamani. Mhe. Mwenyekiti, naomba kukaa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi anasisitiza kwa mujibu wa sheria, hatuambii ni sheria ipi na ya mwaka gani.

Mhe. Mwenyekiti: *Procurement* ndio aliyotumia pale kwamba ndio aliyoizungumzia yeye.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, haihusiani na hiyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakuhsukuru Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachokisema utaratibu wa kuhauliswa haukufuatwa, kwa sababu Rais kaandikiwa kuombwa na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kama kaombwa wao wanajua wameshakaa huko wameshamaliza utaratibu ndio maana wakamuomba yeye, katoa idhini. Lakini hawa ambao wameanzia hili zoezi la kuanza mpaka kufika huko kuombwa ndio ninakosema mimi haukufanyika kwa utaratibu. Hata sasa hivi akimuomba waziri yeyote kule atampa ruhusa, kwa sababu yeye anajua taratibu mmezifuata. Lakini huku taratibu hazikufuatwa, naomba utaratibu uliofuatwa mpaka ikafikia hatua ya kumuomba huyo Rais.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kuna jambo dogo ambalo tunavutana. Mhe. Mwenyekiti, hakuna utaratibu maalum wa kwenda kumuomba Mhe. Rais wa Zanzibar kitu ambacho nahisi yeye atusaidie. Hichi ndicho tulichokisema hapa kwamba kwa mujibu wa sheria Mhe. Rais yeye ndiye mmiliki wa ardhi na taratibu tumefuata. Kuanza na barua na mikataba hii hapa ipo. Ni utaratibu upi mwengine tunaouhitaji jamani.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni zetu kifungu 96(f) kuhusu jambo lisilo na uzito wowote, jambo hilo halihusu kujadiliwa. Kwa hivyo, kama hoja ya kisheria imetolewa na Mhe. Naibu Waziri, sasa kama hakuna hoja ya kisheria ya utaratibu mwengine, basi hatuwezi kujadili jambo ambalo tayari limeshatolewa utaratibu wake na sheria gani, mmiliki Rais mwenye uwezo huo akatoa ruhusa sasa uzito ukuwapi tena mwengine wa hoja. Kwa hivyo, naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 58(3) inayozungumza,

kanuni ya 58(3)

> "Mtu yeyote anayesimama hapa hutakiwa azungumze neno ambalo ni la ukweli".

Mhe. Mwenyekiti, tulipata jawabu la Mhe. Waziri katika hoja hii juu ya uhaulishaji wa kiwanja kutoka kwenye wizara na kupewa mfanyabiashara. Nahesabu kwamba maneno aliyozungumza Mhe. Waziri hapa ni ya kweli. Lakini kwa mnasaba huo natetea mamlaka ya kamati. Kamati ya PAC ilipokwenda katika wizara na kuliuliza suala hili. Nathubutu kusema hapa kwamba yale maelezo kamati iliyoyapata kutoka wizarani ni maelezo ya uongo. Kwa sababu kamati tulidai mkataba, kwa sababu huwezi ukahaulisha jambo lolote lile pasi na kuwa na mkataba. Hilo ni jambo ambalo lazima kamati huwa tunasimamia.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya Baraza 115(3) inasema,

Kanuni ya Baraza 115(3)

> "Kazi moja ya kamati ni kuhakikisha kwamba matumizi na idhini iliyopitishwa katika Baraza yanatumika kama ilivyoidhinishwa na Baraza."

Mhe. Mwenyekiti, wizara iliidhinishiwa milioni 100 na zikatolewa milioni 49. Hizo milioni 49 ilikuwa zitumike kama zilivyoidhinishwa kwa ajili ya kujengea. Mhe. Waziri katoa maelezo mazuri kuwa kutokana na haja kwa kweli fedha zile zilifanyiwa marekebisho.

Hoja ya kwanza ni kwamba hiyo ni kukiuka kanuni kwa mujibu wa fedha zinavyoidhinishwa hapa lazima zitumike kwa mujibu tunavyoziidhinisha katika Baraza hili.

Hoja ya msingi Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tulipodai mkataba kamati haikupewa mkataba. Sasa tunarudia kusema kwamba hilo ni kosa la kudanganya kamati. Ikiwa kosa hilo linakwenda kinyume na sheria ya *The House of Representative Unity Power and Privilege* ya sheria nambari 4 ya mwaka 2007, kifungu cha 22, kwamba mtu yeyote anayetoa maelezo ambayo sio mbele ya kamati basi huyo ni mkosa.

Kwa hivyo, hoja ya kamati na kwa sababu tunatetea mamlaka ya kamati na kamati ilitoa agizo, kwanza ujenzi wa kiwanja kile usitishwe hadi maelezo yatakapotolewa, lakini Katibu Mkuu akaijibu kamati yako Mhe. Mwenyekiti, maelezo ambayo ni kinyume na utaratibu. Kwa hivyo, aliidharau kamati na sijui kama leo yupo na hata tulipokwenda kwenye kamati Katibu Mkuu hakuwepo ni kudharau.

Mhe. Mwenyekiti, leo tunaidhinisha fedha hapa tunamuidhinishia Katibu Mkuu, Katibu Mkuu yuko wapi wa wizara. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninasema ama nakubaliana na maelezo ya waziri, mimi sina tatizo na maelezo ya waziri ni maelezo sahihi. Lakini wizara ikubali kwa sababu kamati ilidhalilishwa kwa kupewa maelezo ya uongo. Nadhani Mhe. Mwenyekiti, tutumie kifungu cha 22 katika sheria nambari 4 ya mwaka 2007, kuitaka wizara iombe kamati ya PAC, ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, napenda niheshimu maelezo ya Mhe. Omar Ali Shehe. Lakini napenda niseme kwamba hapa tunachanganya mambo mawili. Jambo la kwanza tunalolizungumza ni kuhusu utaratibu ambao kuna kiwanja kilichokuwa cha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na baadae kikapewa mtu mwengine na wao wakapewa nyengine. Hilo ni suala moja.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine la pili, ni suala la Katibu Mkuu au viongozi wa wizara kuidanganya kamati, hilo ni suala jengine. Sasa tunalolizungumza na hili huku, hilo jengine kuna utaratibu wake mwengine. Mimi nakubaliana sana kuwa wachukuwe hatua kwa mujibu wa sheria inavyosema. Kule katika sheria

kuna utaratibu wake. Mimi naomba watakapokutana Kamati ya PAC wana utaratibu wa kumwita mtu huyo, kuwaita mashahidi na hata kumpeleka mahakamani hiyo wachukuwe kwa upande mwengine lakini sio hapa ambapo tunazungumzia suala jengine.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunazungumzia suala la kiwanja na kiwanja, utaratibu umetolewa, aliyeombwa na Mhe. Rais na ndiye mmiliki wa kila kitu katika Zanzibar hii ametoa kibali na kibali hicho kimefanywa. Sasa utaratibu tushughulikie suala hili. Kuhusu suala la wizara kama kuna mtu aliyesema uongo au aliyedanganya, mimi nakubali lakini tuchukuwe kwa mujibu wa sheria nambari 4 ya mwaka 1998 nafikiri ya *privileges and immunity,* huo ni utaratibu mwengine. Mhe. Mwenyekiti, naomba twende kwenye mada hii.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo yote hayo ambayo nimeyapata, mimi nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwamba kamati irudi tena pale ikaendelee kufanya uchunguzi kule chini kabisa, tuachana na hilo jambo. Mimi nakubaliana tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0901	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	632,000,000
Kifungu 1001	Idara ya Mawasiliano	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala la Kampuni ya Zantel ambayo kwa mujibu wa hotuba ya waziri, katika ukurasa wa 40 chini ya Idara ya Mawasiliano, alituarifu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa ya asilimia 18.

Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya Mhe. Waziri kutokana na muda mrefu aliotumia kujibu hoja zetu za awali, nadhani hakulifikia suala hili. Kwa hivyo, nilikuwa naomba maelezo kwa sababu nilihoji hapa kwamba Kampuni ya Zantel ambayo Serikali ya Zanzibar inahisa imeonekana imehama katika Makao Makuu yake na Makao Makuu iliyobaki Zanzibar imebakia jina tu. Lakini Makao Makuu hasa yako Msasani Dar es Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hata ukilinganisha yale majengo yalivyo haiitaji jicho lenye nuru kali kuliko langu mimi kuweza kuona kwamba Makao Makuu yamehamia Dar es Salaam na nikasema adhari zake ni pamoja na Wazanzibari kupoteza ajira, sio tu kwa kutumia Makao Makuu ambayo hivi sasa yamehamia kule, lakini nilisema hata uendeshaji wake umepelekea katika nafasi za msingi hapa Zanzibar ukiondoa zile za *customer care* zimeshikiliwa na ndugu zetu wa damu.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti, ambayo bahati mbaya Mhe. Waziri hakunielewesha. Anipe maelezo ya kwamba wizara yake ina mpango gani kuweza kusimamia kwamba haki za Zanzibar katika kampuni hii zinarudi na kwamba kampuni hii tutaachiwa kurudisha Makao Makuu yake, kwa maana halisi ya Makao Makuu hapa Zanzibar sio kama lile jengo lililobakia pale Amani, na kwamba italinda ajira kwa nafasi za msingi katika zile nafasi za *managerial* kuona kwamba vijana wetu wa Kizanzibari ambao wamesoma wanapata ajira badala ya kuwanufaisha watu ambao hawakuingiza chochote katika kampuni hii. Naomba maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tutakumbuka kwamba wakati nawasilisha ufafanuzi kwa ajili ya kuwajibu Waheshimiwa Wajumbe nilisema kwamba mimi na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tulikwenda Dubai kwa ajili ya Zantel. Nikasema kwamba nitakapoizungumzia Zantel, ndio nitazungumza haya. Kwa bahati mbaya kwamba kwa sababu ya wakati kama nilivyosema mambo mengi nimeyafupisha.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, unipe fursa ili nitowe maelezo ambayo Mhe. Mjumbe ameyaomba.

Mhe. Mwenyekiti: Jibu kwa mkato lakini.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Makao Makuu ya Zantel jina ni Zanzibar, Dar es Salaam ni Ofisi Kuu ya Zantel. Nimesema jina kwa sababu sivyo ilivyokuwa awali. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ziara yetu ya mimi na Mhe. Waziri na Katibu Mkuu wa fedha, tulifanya kazi kubwa na nawaambieni sasa hivi Makao Makuu ya *ZANTEL practical* yanarudi kidogo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, *ZANTEL* iko njiani kurudi na ufuatao ni ushahidi. Kwanza kuna mabadiliko makubwa yaliyofanyika katika *ZANTEL*, (*CEO)* aliopo yaani *Chief Executive Officer* sio wale ambao walishiriki sana kuihamisha Makao Makuu kiholela. Amekuja mpya na hata *Chairman* wa *Board* ya *ZANTEL* amebadilika ni mwengine kabisa. Katika kujijenga vizuri *ZANTEL* Bara walishafanya mipango na mipango ilikuwa robo njia ya kujenga *cole center* ambayo itaajiri watu zaidi ya 100. Tumefanya kwa hoja maalum. Sasa *cole center* ile haijengwi tena Bara inajengwa Zanzibar na karibu itakuwa tayari na zaidi ya Wazanzibari 100 watapata kazi katika *cole center* hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sheria ilikuwa hairuhusu kampuni yoyote ya kigeni kuwa na *share*. Zantel ilikuwa na *shareholders* wanne, Zanzibar nafikiri vyake 18.

Lakini njiani *shareholder* mmoja akatoka akanunuliwa, wakabaki *shareholders* watatu hadi sasa. Sasa hivi *shareholder* mwengine baada ya kanuni kubadilika za makampuni ya mawasiliano, *ZANTEL* sasa hivi itakuwa na *shareholders* wawili ambao ni **At Salat** na Zanzibar. Nikutokana na kanuni hizo kubadilika kwa sababu haikubadilika hivi hivi ni *pressure* ambayo tumeiweka. Itakapofikia hali hii At Salat itakuwa na asilimia 72 na hapo ndipo furaha yao itakapokamilika kwa sababu wataweza ku- *invest heavily* kwa kuisaidia Zanzibar. Moja ni kujenga jengo maalum litakalojengwa Fumba ambako tayari kuna kiwanja.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Zantel ilikuwa haina nafasi kubwa za juu. Lakini sasa hivi Zantel Wazanzibari walioko kuna nafasi kubwa tatu za u-*director* ambao ni Wazanzibari hapa. Mhe. Mwenyekiti, Zantel imeajiri watu wengi, ina zaidi ya walinzi 200 wameajiriwa na Zantel. Waliokuwepo kabla ya *Chief Executive* huyu ilikuwa walinzi wale wanaondolewa inakuja kampuni, tukasema hapana serikali hii haiwezi kuvumilia. Kwa hivyo, Zantel wakasema sawa. Kwa hivyo, bado walinzi wa Zantel ni wale wale Wazanzibari na wataendelea kuwa pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, katika watu walioajiriwa wa kada mbali mbali wasiokuwa walinzi. Kuna wafanyakazi 350 kati ya hao 30 tu sio Wazanzibari, maana yake ni kwamba 320 ni Wazanzibari. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Zantel ina mpango wa kuanzisha *site* 75, ambao itasaidia kukuza uajiri hapa Zanzibar na kuongeza mawasiliano. Pia inampango wa kujenga (*BSC)* yaani *Belt Station Controller* katika kiwanja chake kilichopo maeneo huru Fumba.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema pole pole ndio mwendo. Tulikuwa na Makao Makuu hapa na hata zile nembo zetu Marhaba na nyenginezo zote zimepotea. Mimi naamini kuwa (*CEO*) aliopo. Hata juzi tulikutana, akaniambia atahakikisha kwamba anakuwa na nyumba yake Zanzibar kama makaazi na Wengine wote wanaohusika kufanyakazi Makao Makuu watarudi hapa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema nashukuru sana Mhe. Ismail Jussa, kupiga buti yake hapa, kwa sababu nimepata nafasi ya kulizungumza hili suala la Zantel ambalo nilikuwa nimesema nisizungumze kwa sababu ya wakati. Kwa hivyo, Zantel inarudi kidogo kidogo na kwa imani yangu sio muda mrefu Zantel itakuwa kama asilia. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake hayo mazuri. Kwa hivyo, nimuombe tu kabla sijaruhusu kifungu hiki tuendelee. Kwamba watupie jicho pia katika hizo nafasi ulizosema za *managerial* hapa Zanzibar kwa sababu kama ulivyosema. Unapokwenda pale Majestic kwenye ofisi yao ya *customer care*, unawakuta ndugu zetu wa

Kizanzibari wako katika madesk wanaanza kuhudumia. Lakini ukiambiwa pawe na mtawala basi ukiingia lugha tu inakujulisha kama umekutana na ndugu yetu wa damu. Kwa hivyo, naomba kwamba hili atusaidie na baada ya hayo nasema tuendelee ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 1001	Idara ya Mawasiliano	103,000,000
	Jumla ya Fungu	**4,258,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 26 WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	18,630,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Anga	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Nadhani Mhe. Waziri hakufikia kutujibu majibu yetu yote ya maswali tuliyouliza, nadhani mimi hakunisikia vizuri, katika mchango wangu nilihoji katika sehemu hii ya maendeleo kwamba katika hotuba yake ile iliyokuwemo ndani ya kitabu ilikuwa haina maelezo fulani ambayo aliyataja hapa kwamba *world bank* ilikuwa pia imetoa mkopo wa dola milioni 57 ambazo ni pesa za maendeleo.

Sasa nilikuwa naomba nisaidiwe kwamba fedha hizi hazikuombewa, nilitaka maelezo kwa waziri, kwa sababu fedha hizi hata zikiwa ni mkopo au ni msaada bado zinakuja kwa Zanzibar na Baraza hili kama ndio dhamana wa haki za wananchi wa Zanzibar inapaswa kuombwa idhini ya matumizi. Sasa hili alilisema nje ya kitabu. Kwa hivyo, naomba aje atusaidie maelezo kwamba fedha hizi kwa nini hazikuombewa matumizi yake katika Baraza hili na kama kuna maelezo ya ziada anipe ili tuendelee, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi milioni 89 zitaombwa kutoka serikalini. Kuna dola 57 milioni ambazo nilizitaja lakini haziko katika hotuba yangu. Sasa hizi ni msaada wa *world bank* ambao tunatarajia kuupata. Naomba Baraza lako tukufu likubali maombi ya ziada ya dola milioni 57.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ni jukumu la Baraza kukubali. Mimi nimekubali, ahsante sana.

Kifungu 0601 Idara ya Anga

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilipokuwa nachangia, nilitaka kujua ukweli wa wananchi ambao walikuwa hawajalipwa fidia katika ule ujenzi wa uzio, nilisema kwamba kuna wananchi ambao hawajalipwa fidia. Nilimtaka Mhe. Waziri aje atupe ukweli wa jambo lile kwamba wapo ambao hawajalipwa au wote walishalipwa, kwa sababu katika suala langu la msingi lililopita niliulizia kwamba kuna wananchi hawajalipwa fidia katika ujenzi wa uzio ule. Lakini Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anatujibu, alijibu kwamba hakuna mwananchi ambaye hajalipwa fidia.

Mhe. Mwenyekiti, leo katika majumuisho hapa, Mhe. Naibu Waziri kakiri kwamba kweli kuna wananchi bado hawajalipwa fidia. Sasa mimi nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa amelidanganya Baraza kwa kauli yake ile ya mwanzo, alikuwa atumie fursa hii kutuomba radhi yaani aliombe radhi Baraza ili tuweke kumbukumbu zetu vizuri. Kwa sababu mwanzo tulipokea kwamba wameshalipwa wote, lakini leo tunaambiwa hawajalipwa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba atumie fursa hii kuliomba radhi Baraza kwa kauli yake hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sasa tunajadili bajeti ya maendeleo, suala analozungumzia Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando halihusiani zaidi na hili.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0601	Idara ya Anga	52,540,000,000
Kifungu 0701	Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara	27,452,725,000
	Jumla ya Fungu	**98,622,725,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa kamati ya matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liyakubali makisio hayo.Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile maelekezo yameshatoka kwa Mhe. Waziri na mambo yamekuwa kama tulivyoyaona, niwahoji basi wale wajumbe wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sasa hivi ni muda ambao unaonesha saa 9:00, ningeomba mheshimiwa tuweke kando kanuni ili Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aendelee. *(Vicheko/ Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe, naomba kwanza tumalize hili ikisha tutakwenda kwenye jengine.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kazi kubwa na nzito ambayo tumekwisha kuifanya kwa umoja wetu hapa. Sasa kabla hatujaahirisha kikao naomba nitowe tangazo.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaarifiwa sote kwamba kutakuwa na Bonanza la michezo siku ya Jumamosi tarehe 16/072011 kwa kushirikiana na Wakurugenzi na *Management* wa Benki zote zilizopo hapa Zanzibar kwa kuchezo michi ya mpira wa miguu, kati ya wawakilishi wa timu ya mchanganyiko ya benki pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote. Kwa hivyo, mnaombwa kushiriki ili kuhamasisha wawekezaji hao kuchangia ili kuinua mambo ya michezo kwa hapa Zanzibar. Tamasha hilo litaanza kuanzia saa 8:00 katika uwanja wa Mao Tse Tung.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelekezo hayo, kwanza kabisa nichukuwe fursa hii kukushukuruni tena kwa mara nyengine tena kwa kuweza kuendesha shughuli zetu kwa salama na amani na kuweza kufikia hapa tulipofika. Baada ya maelekezo hayo sasa nachukua fursa hii kuahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 tutakapokuja kusikiliza hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

(Saa 9:00 jioni Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba yangu. Lakini napenda kuomba radhi kwamba nitakapokuwa ninasoma hotuba yangu Mhe. Mwenyekiti sitakisoma kitabu chote hiki, isipokuwa nitasoma na halafu nitawaelekeza Waheshimiwa Wajumbe ukusara wa kuangalia.

UTANGULIZI:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa liingie katika kamati, ili niweze kutoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kutuwezesha kukutana hapa leo, tukiwa wazima na wenye afya njema na tuko katika hali ya amani na utulivu na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukuwa fursa hii kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwapongeza wananchi wote wa Zanzibar kwa kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kwa amani, utulivu na kumchagua mgombea wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile napenda kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kutekeleza Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar kwa kuunda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa. Muundo ambao umejenga misingi imara ya mashirikiano katika kuleta maendeleo ya Zanzibar. *(Makofi)*

Tunaahidi kumuunga mkono katika juhudi zake za kuleta maelewano, umoja, amani na maendeleo ya haraka ya watu wa Visiwa vya Unguja na Pemba. Vile vile, napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru tena wananchi wote wa Zanzibar kwa kushiriki kwao kikamilifu katika Kura ya Maoni, kura ambayo imepelekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu maalum kwa Viongozi wa Vyama vya Siasa, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Tume ya Uchaguzi kwa kuwezesha mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kukamilika kwa amani, utulivu na mshikamano mkubwa. Shughuli zote mbili, yaani Kura ya Maoni na Uchaguzi Mkuu wa 2010 zimeiletea sifa kubwa nchi yetu na Zanzibar imekuwa ni mfano wa kuigwa na mataifa mengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Mhe. Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa na Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Kuteuliwa kwao na Mhe. Rais kushika nyadhifa hizo za juu umeudhihirishia umma wa watanzania juu ya uwezo wao mkubwa wa utendaji na mashirikiano chini ya Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Pongezi pia zikujie wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kuchaguliwa na Wajumbe wa Baraza hili kushika nafasi ya Uwenyekiti wa Baraza hili. Kuchaguliwa kwako kunadhihirisha uwezo mkubwa ulio nao katika kuliongoza Baraza hili tukufu kwa misingi ya uadilifu na uaminifu mkubwa. Aidha nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa ushindi walioupata katika majimbo yao, yakiwemo pia yale ya uteuzi, hata wakaweza kuingia katika Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake ya Baraza la Wawakilishi ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk kwa kutuongoza vyema na kutushauri ipasavyo. Wajumbe wa Kamati hii waliweza kuichambua na kuijadili hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kwa undani kabisa na mwishowe kuipitisha. Pia wameweza kuishauri Wizara yangu ipasavyo kila walipotembelea shughuli tunazoziendesha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kikao hiki cha bajeti ni cha kwanza tokea tulipomaliza uchaguzi mkuu wa mwaka 2010, na kwa kuwa Baraza lako tukufu lina sura nyingi mpya, naomba nianze maelezo yangu kwa kutoa angalau kwa muhtasari tu Mpango wa Maendeleo ambao Sekta ya Elimu inawajibika kuutekeleza kutokana na Dira 2020, MKUZA, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Sera ya Elimu 2006 na Mpango Mkuu wa Elimu wa Zanzibar (*ZEDP*).

MPANGO WA ELIMU KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO IJAYO 2011 - 2015

Mhe. Mwenyekiti, Elimu ya Maandalizi ni sehemu ya elimu ya lazima kama ilivyoelezwa katika Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Afya, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto na mashirika yasio ya kiserikali itaandaa Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (*Integrated Early Childhood Care and Development Policy*).

Sera hio itakuwa ndio kiongozi kwa sekta zetu kuandaa na kutekeleza mipango ya maendeleo ya malezi na elimu ya maandalizi ya watoto wadogo kwa mashirikiano ya karibu. Katika kipindi hicho, wizara, inakusudia kujenga skuli mpya 8 za maandalizi, ili kuongeza idadi ya Skuli za Serikali zinazotoa elimu ya maandalizi. *(Makofi)*

Vile vile, wizara itaendelea na utaratibu wa kuanzisha madarasa ya maandalizi katika skuli za msingi ili kuhakikisha kuwa watoto wengi zaidi wanapata elimu ya maandalizi kabla ya kujiunga na elimu ya msingi. Mbali na juhudi hizo,

juhudi za kutoa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio zitaendelezwa, ili watoto wadogo ambao hawatoweza kupata elimu hiyo kupitia skuli za msingi waweze kunufaika na elimu ya maandalizi kupitia vipindi vya redio. *(Makofi)*

Aidha, wizara itaanzisha mafunzo kwa walimu wa skuli za maandalizi yatakayotolewa kwa njia ya redio. Pia, wizara inakusudia kutayarisha, kuchapisha na kusambaza vijitabu vya wanafunzi na viongozi vya walimu kwa wanafunzi wa madarasa ya maandalizi kwa mujibu wa mihutasari mipya ya elimu ya maandalizi ya mwaka 2008.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watoto waliofikia umri wa kujiunga na skuli za msingi. Wizara yangu itaendelea na juhudi zake za kuwahamasisha wananchi kujenga madarasa na skuli mpya za msingi katika sehemu ambazo hakuna skuli au skuli zilizopo hazina nafasi za kutosha.

Ni kwa njia ya wananchi kujitolea katika ujenzi wa madarasa mapya ndio tutafanikiwa kuwapatia nafasi za kusomea watoto wetu wote waliofikia umri wa kwenda skuli kupata elimu wanayostahiki. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, wizara inakusudia kukamilisha ujenzi wa madarasa 1,000 yalioanzishwa na yatayoanzishwa kwa nguvu za wananchi pamoja na kuchonga madawati 30,000. Tatizo la vikalio linazozikumba skuli zetu nyingi hivi sasa, linatarajiwa kumalizika kabisa katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Katika kuhakikisha kwamba watoto wote waliofikia umri wa kwenda skuli wanaandikishwa na wanapatiwa nafasi ya kwenda skuli, hasa watoto wenye mahitaji maalumu, wizara itaikamilisha Sera ya Elimu Mjumuisho pamoja na kuvijengea uwezo vituo vya walimu, ili viweze kutoa mafunzo ya elimu mjumuisho kwa walimu waliomo katika kanda zao.

Aidha, Wizara itachapisha na kusambaza vitabu vya kiada, viongozi vya walimu na vifaa vyengine vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wote wa madarasa ya 1- 6 kwa mujibu wa mihutasari mipya ya elimu ya msingi ya mwaka 2009. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba ufundishaji katika elimu ya msingi unaimarika. Wizara yangu inakusudia kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika kufundishia na kujifunzia. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikishirikiana na Serikali ya Marekani na makampuni ya *Microsoft*, *CISCO*, *INTEL* na *Zantel* itatekeleza mradi mkubwa unaojulikana kwa jina la "*21st Century Basic Education*" wenye lengo la kuinua kiwango cha elimu cha wanafunzi wa madarasa ya 1- 4 katika kusoma, kuhesabu na Sayansi. *(Makofi)*

Kupitia mradi huu skuli zote za msingi za Unguja na Pemba zitapatiwa kompyuta na zitaunganishwa na mtandao wa "*Internet*". Mradi huo utatoa mafunzo kwa walimu wa madarasa ya 1-4 ya msingi juu ya mbinu za kusomesha kwa kutumia kompyuta. Mradi huu pia utahusisha matumizi na utunzaji wa takwimu mbali mbali za skuli kwa kutumia kompyuta na kuziunganisha skuli zetu zote na *"data-base"* ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi za kutoa elimu ya lazima hadi kidato cha nne kwa wanafunzi wote wa Zanzibar zitaendelezwa katika miaka mitano ijayo. Wizara inakusudia kujenga na kukamilisha ujenzi wa skuli za sekondari 21, kukarabati skuli 10, kuzipatia skuli zote vitabu vya kutosha, vifaa vya maabara na samani. Kati ya skuli 21 skuli 16 zinatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu na kuanza kutumika rasmi kuanzia mwezi Januari mwaka 2012. Skuli hizo zitakuwa na vifaa kamili kama vile madawati, vitabu, vifaa vya maabara na kompyuta. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, walimu ni muhimili mkubwa katika kutimiza lengo la kuwapatia wanafunzi elimu iliyo bora. Kwa kulitambua hili, wizara yangu katika miaka mitano ijayo itaimarisha mafunzo ya ualimu vyuoni na mafunzo ya ualimu kazini.

Wizara itahakikisha kuwa Vyuo vya Ualimu vya Kiislamu Mazizini, Micheweni na Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Wete vinaimarishwa na kupatiwa nyenzo na hatua kwa hatua vitapandishwa daraja na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Ujenzi wa Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar nao pia utakamilishwa na kuanza kutumika. *(Makofi)*

Upanuzi huu wa vyuo vinavyotoa mafunzo ya ualimu utatoa nafasi zaidi kwa walimu kuweza kujifunza na pia kuanzisha programu mpya za ualimu ikiwemo Stashahada ya Uongozi katika Elimu. Wizara pia itaendelea na juhudi za kuimarisha mafunzo ya uwalimu na kuajiri walimu waliohitimu mafunzo ya ualimu. Aidha Wizara itasomesha na kuajiri wakutubi na wasaidizi wa maabara (*laboratory Assistant*). *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara itaendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu yanayohusiana na mbinu bora za kufundishia masomo ya Kiingereza, Sayansi na Hisabati, Stadi za Maisha, VVU na UKIMWI. Katika kuhakikisha kwamba mafunzo kazini yanaleta tija kwa walimu, wizara itaandaa na kutekeleza Sera ya Mafunzo ya Ualimu Kazini.

Mhe. Mwenyekiti, Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali ina umuhimu mkubwa katika kuwajenga vijana wetu na maarifa na ujuzi utaowawezesha kujitegemea. Katika kipindi hiki, wizara yangu itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi Mtemani. Pia inakusudia kujenga Vituo vinne vya Elimu Mbadala na Vituo vinne vya Mafunzo ya Amali katika mikoa ambayo vituo hivyo havijaanzishwa.

Lengo ni kuhakikisha kuwa kila Mkoa una walau kituo kimoja cha Elimu Mbadala na Kituo kimoja cha Mafunzo ya Amali. Mafunzo katika vituo hivyo yatawawezesha vijana wetu kuwa na maarifa na ujuzi wa kazi za ufundi na taaluma ya ujasiriamali ili waweze kuajiriwa au kujiajiri wenyewe. Kwa wahitimu ambao wataamua kujiajiri wenyewe, wizara itawapatia mikopo ya kununulia zana na mali ghafi ya kuzalishia mali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya malengo ya MKUZA II ni kuongeza uandikishaji wa wanafunzi katika taasisi zinazotoa elimu ya juu kutoka 3,624 (2009) hadi kufikia 6,000 (2015). Katika kutekeleza lengo hilo kwa miaka mitano ijayo, wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika itaratibu upanuzi na uongezekaji wa fani za masomo zinazotolewa na taasisi za elimu ya juu ziliopo Zanzibar kulingana na mahitaji ya soko la ajira.

Katika kuimarisha utoaji wa mikopo ya elimu ya juu, Sheria ya Uanzishaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, imeshapitishwa na Baraza lako tukufu na inatarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni. Sheria hii mpya itahakikisha kuwa wanafunzi watakaopatiwa mikopo ya elimu ya juu, wanarejesha fedha walizokopeshwa baada ya kuhitimu na kuajiriwa, ili marejesho ya fedha hizoi ziweze kutumika kwa kuwasomeshea wanafunzi wengine.

Mhe. Mwenyekiti, muundo wa wizara yangu umebadilika kufuatia kuundwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba na mazingatio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Katika muundo huo mpya Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale imehama katika Wizara yangu. Pia, Idara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia imekufa. Idara ya Mitaala na Mitihani imebadilika sura na mahali pake imechukuliwa na vyombo viwili vinavyojitegemea; Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.

Vile vile, Idara ya Ukaguzi wa Elimu imebadilika na kuwa chombo kinachojitegemea kinachojulikana kwa jina la Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Pia wizara imeunda Idara mpya ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kutokana umuhimu wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika utoaji wa elimu. Mabadiliko hayo yatasaidia sana katika

kuimarisha utendaji na ufanisi wa kazi na kuimarisha ubora wa elimu yetu. Kwa jumla wizara inaundwa na Idara saba kama hivi ifuatavyo:-

i. Idara ya Sera, Mipango na Utafiti na
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
iii. Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi,
iv. Idara ya Elimu ya Sekondari,
v. Idara ya Mafunzo ya Ualimu,
vi. Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima,
vii. Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano,

Pia kwa upande wa Pemba shughuli za wizara zipo chini ya Ofisi ya Elimu na Mafunzo ya Amali, inayoongozwa na Ofisa Mdhamini.

Wizara pia ina mabaraza yanayosimamia Taasisi zinazojitegemea. Zipo Taasisi nane ambazo zinawajibika moja kwa moja kwa bodi za taasisi hizo. Taasisi hizo ni zifuatazo:

i. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar,
ii. Bodi ya Huduma za Maktaba,
iii. Mamlaka ya Mafunzo ya Amali,
iv. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume,
v. Taasisi ya Elimu ya Zanzibar,
vi. Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu,
vii. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na
viii. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu

Pia Wizara ina vitengo vinne viliopo chini ya Katibu Mkuu. Navyo ni:-

i) Kitengo cha Uhasibu,
ii) Kitengo cha Ununuzi na Ugavi ,
iii) Kitengo cha Ukaguzi wa ndani wa Hesabu na
iv) Kitengo cha Habari, Elimu na Uhusiano

Vitengo vyengine vinne vipo chini ya Kamishna wa Elimu ambavyo ni:-

i) Kitengo cha Urajis wa Elimu,
ii) Kitengo cha Michezo na utamaduni maskulini,
iii) Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha na
iv) Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu.

Muundo wa wizara unaonekana katika kiambatanisho B

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza kuhusu muundo wa wizara, kwa heshima naomba uniruhusu kuelezea utekelezaji wa shughuli za wizara kwa idara moja moja na taasisi zinazojitegemea kwa mwaka 2010/2011 na matarajio na malengo kwa mwaka 2011/2012.

IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Sera, Mipango na Utafiti ina majukumu ya kuandaa sera na mipango ya maendeleo na kusimamia utekelezaji wake. Pia husimamia utafutaji na uratibu wa misaada ya wahisani mbali mbali wa ndani na nje ya nchi. Aidha idara hushughulikia masuala ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na masuala ya utafiti wa elimu na uchapishaji wa majarida ya elimu pamoja na kusimamia ujenzi wa skuli, madarasa mapya na upatikanaji wa samani za skuli.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilipanga kutekeleza jumla ya miradi kumi ya maendeleo iliyotengewa shilingi 50,850,089,000/- ambapo kati ya hizo shilingi 4,475,000,000/- ni mchango wa SMZ na shilingi 46,375,089,000 za wahisani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, shilingi 3,380,000,000/= za SMZ ikiwa ni sawa na asilimia 76 ya makadirio zilikwisha tolewa. Utekelezaji halisi wa miradi ulikuwa kama ifuatavyo:-

Programu ya Uimarishaji wa Elimu ya Msingi

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 500,000,000/= za SMZ na shilingi 8,998,354,000/= kutoka Sida na UNICEF. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, Tsh. 435,000,000/= ikiwa ni sawa na asilimia 87 ya makadirio zilitolewa na SMZ na kutumika. Kwa upande wa mashirika ya Sida na *UNICEF* Tsh. 2,261,496,360/- zilizotolewa na kutumika sawa na asilimia 25 ya makadirio. Utekelezaji halisi wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya madarasa mapya 132, ukumbi wa mkutano 1, maabara 2, maktaba 2, vyumba vya mitihani 3, vyumba vya kompyuta 2 yamekamilika na kuanza kutumika na madarasa 61 tayari yameshaezekwa na yanasubiri utiaji wa sakafu, plasta na rangi. Vile vile jumla ya madarasa 280 yamefikia hatua ya kuezekwa, madarasa 116 yamo katika hatua za

ujenzi wa kuta na nguzo na madarasa 109 yamefikia hatua mbali mbali za ujenzi kuanzia ukusanyaji wa vifaa hadi kuinua kuta. Jadweli 11 (a – d) zinatoa uchambuzi zaidi.

(ii) Ukarabati wa majengo umefanyika na kukamilika katika skuli za Biashara Mombasa, Msingi Bububu, Msingi Mtopepo, Bwefum, Jongowe, Upenja, Bumbwini, Unguja Ukuu na Mtende kwa Unguja na skuli ya Ng'ombeni kwa Pemba.

(iii) Walimu wameendelea kupatiwa mafunzo mbali mbali yakiwemo ya kompyuta, mafunzo juu ya kutumia lugha ya Kiingereza kwa ajili ya kufundishia, mafunzo juu ya mtaala mpya wa ngazi ya msingi na mafunzo juu ya kufundishia katika mfumo wa elimu mjumuisho.

(iv) Jumla ya madawati 1,920, meza 947 na viti 947 yamechongwa na kusambazwa katika skuli mbali mbali za Unguja na Pemba.

(v) Walimu 686 wameendelea kupatiwa mafunzo kwa njia ya elimu masafa katika kiwango cha Daraja la IIIA.

(vi) Mfumo wa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za elimu (*data base*) ulifanyiwa mageuzi baada ya maafisa wawili wa Wizara kwenda Harare na kupata mafunzo chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Sweden (*Sida*) na wakufunzi kutoka *NESIS* Team (*UNESCO*).

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 400,000,000/= za SMZ na shilingi 314,071,000/= za *UNICEF*. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, jumla ya shilingi 330,000,000/= ikiwa ni sawa na asilimia 83 ya fedha zote za SMZ zimetolewa na kutumika. Kwa upande wa *UNICEF* fedha zilizotolewa ni shilingi 241,703,420/= Utekelezaji halisi ulikuwa kama ifuatavyo:-

i. Ujenzi wa skuli mbili mpya za Maandalizi Potoa kwa Unguja na Ungi kwa Pemba unaendelea.

ii. Mafunzo juu ya mtaala mpya wa elimu ya maandalizi yalitolewa kwa walimu 70.

iii. Mafunzo ya wakufunzi 33 ambao watasomesha walimu wa maandalizi kwa njia ya redio yalitolewa.

iv. Vifaa vya kufundishia elimu ya maandalizi vilinunuliwa na kusambazwa katika skuli za maandalizi Unguja na Pemba.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa na SMZ pekee na katika mwaka 2010/2011, ulipangiwa kutumia jumla ya shilingi 500,000,000/= kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa madarasa katika skuli ya sekondari ya Ufundi Kengeja, kuipatia vifaa vya karakana na kuendelea na ukarabati wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, jumla ya shilingi 410,000,000/= ikiwa ni sawa na asilimia 82 zimepatikana na kutumika. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i. Kazi za ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume zimefanyika.

ii. Kazi za uchongaji wa milango na madirisha kwa ajili ya madarasa manne mapya ya skuli ya sekondari ya ufundi ya Kengeja zimefanyika.

iii. Kazi za ukarabati wa dakhalia pamoja na mfumo wa maji machafu katika skuli ya sekondari ya ufundi Kengeja umefanywa.

Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Kiislam Micheweni Pemba:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 50,000,000/= za SMZ. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, jumla ya shilingi 20,000,000/= za SMZ ikiwa ni sawa na asilimia 40 ya makadirio zilitolewa. Kazi zilizofanywa ni ukarabati wa dakhalia na dari ya jengo la utawala.

Mradi wa Upanuzi na Uimarishaji wa Huduma za Maktaba:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya shilingi 150,000,000/- zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa vitabu, samani na kompyuta na kuanza kazi za ujenzi wa tawi la Maktaba Kuu huko Chake Chake Pemba. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, jumla ya shilingi 75,000,000/= sawa na

asilimia 50 zimepatikana na kutumika kwa kuongeza majengo nje ya jengo kuu ikiwemo choo, kuchimba kisima na kujenga banda la kuegesha magari.

Mradi wa Uanzishaji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na ulitengewa shilingi 1,725,000,000/- za SMZ na shilingi 5,552,664,000/- kutoka *BADEA*. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011 jumla ya shilingi 1,305,400,000/- za SMZ ikiwa ni sawa na asilimia 76 ya makadirio zilipatikana na kwa upande wa *BADEA* jumla ya shilingi 1,932,781,200/= zilipatikana. Utekelezaji halisi ni kama hivi ifuatavyo:-

i. Kazi za ujenzi wa jengo la Maktaba, jengo la Utawala, jengo la Kitivo cha Sanaa na Sayansi na jengo la Kitivo cha Uhandisi zinaendelea. Ujenzi huo umefikia asilimia 75.

ii. Hatua za ununuzi wa vifaa vya maabara na kemikali zinaendelea.

iii. Hatua za ununuzi wa samani za madarasani na ofisini, vifaa vya kompyuta ziko katika maandalizi ya zabuni.

Mradi wa Uanzishaji wa Elimu Mbadala na Amali:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ambao unatekelezwa na SMZ pekee ulitengewa jumla ya shilingi 150,000,000/- na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

iv. Kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya ushirika vya akinamama, wajasiriamali na wahitimu wa vituo vya mafunzo ya amali wenye lengo la kujiajiri wenyewe.

v. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi Mtemani Pemba.

vi. Kununua samani na vifaa vya kufundishia.

vii. Kuanza kutumika kwa Kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, jumla ya shilingi 130,000,000/- za SMZ ikiwa ni sawa na asilimia 87 ya makadirio zilipatikana.

Utekelezaji halisi wa mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Mikopo yenye thamani ya shilingi 600,000,000/- ilitolewa kwa vikundi vya ushirika 09 vyenye wanachama 554, kati yao 336 ni wanawake na 218 ni wanaume.

(ii) Jumla ya shilingi 569,744,273/- zimekusanywa ikiwa ni marejesho ya mikopo iliyotolewa siku za nyuma.

(iii) Ujenzi wa kuta za jengo zima la Kituo cha Elimu Mbadala Wingwi Mtemani zimekamilika. Mabati kwa ajili ya kazi za kuezeka yamenunuliwa. Kazi za upigaji plasta zimeanza kwa eneo la chini.

Mradi wa Ukamilishaji wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ambao unatekelezwa na SMZ pekee ulitengewa shilingi 75,000,000/- na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa eneo la maegesho ya magari.

(b) Kununua samani, kompyuta na vitendea kazi vyengine.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, jumla ya shilingi 75,000,000/- ikiwa ni sawa na asilimia 100 ya makadirio zilipatikana na zilitumika kwa kazi za ukamilishaji wa ujenzi wa eneo la maegesho ya magari na vibanda vya walinzi. Pia ujenzi wa ghala ya tatu umekamilika.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa kwa pamoja kati ya SMZ, Benki ya Dunia na *BADEA*. Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 900,000,000/- za SMZ na shilingi 31,510,000,000/- kutoka Benki ya Dunia na *BADEA*. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, jumla ya shilingi 589,600,000/= za SMZ sawa na asilimia 66 ya makadirio na shilingi 16,636,809,613/= za Benki ya Dunia na *BADEA* zilipatikana. Mradi ulikuwa na malengo yafuatayo:-

(a) Kuzipatia skuli za sekondari vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia na kujifunzia.

(b) Kuzipatia samani skuli mbali mbali za sekondari.

(c) Kuanza ujenzi wa skuli za sekondari 15 Unguja na Pemba.

(d) Kuanza ujenzi wa Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Mchanga Mdogo Pemba.

(e) Kununua vifaa vya ofisini.

(f) Kuanza matengenezo ya skuli za sekondari za Forodhani, Tumekuja, Hamamni, Fidel Castro, Utaani na Uweleni.

(g) Kuanza ujenzi wa skuli mbili za sekondari katika eneo la Kibuteni Unguja na Mkanyageni Pemba.

Utekelezaji halisi wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

i) Jumla ya vitabu vya kiada 558,104 na vya maktaba 30,260 kwa skuli za sekondari vimenunuliwa na kusambazwa. Vitabu hivyo ni vya masomo ya Kiswahili (K1-K2), *English* (K1-K6), *Geography* (K1- K6), *Civics* (K1-K4), baadhi ya vitabu vya masomo ya ufundi (K1-K4), *History* (K1-K2) na masomo ya ualimu.

ii) Jumla ya seti 738 (viti na meza) zimechongwa na kusambazwa kwa ajili ya skuli za sekondari za Unguja na seti 372 kwa ajili ya skuli za Pemba.

iii) Ujenzi wa skuli mpya 16 za sekondari unaendelea katika hatua mbali mbali. Skuli zenyewe ni Paje Mtule, Matemwe, Mwanda, Chaani, Uzini, Dole, Tunguu na Dimani kwa upande wa Unguja na Shamiani,Wawi, Ngwachani, Kiwani Mauani, Utaani, Pandani, Konde na Chwaka Tumbe kwa upande wa Pemba.

iv) Ujenzi wa Kampasi mpya ya Chuo cha Ualimu Benjamin William Mkapa unaendelea.

v) Taratibu za ununuzi wa vifaa vya ofisini kwa skuli za sekondari 25 zimekamilika. Vifaa husika ni kompyuta, printa na mashine za fotokopi.

vi) Wizara imeshatiliana sahihi mkataba na wakandarasi wa ukarabati wa skuli ya Utaani na Fidel Castro na kazi zinatarajiwa kuanza hivi karibuni. Taratibu za kuwapata wakandarasi wa kukarabati skuli za sekondari za Forodhani, Tumekuja, Hamamni na Uweleni zinaendelea.

vii) Utayarishaji wa michoro ya ujenzi wa skuli za sekondari za Kibuteni Unguja na Mkanyageni Pemba umekamilika na zabuni za ujenzi wa skuli hizo zimetangazwa hivi karibuni.

Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2011/2012:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, wizara imepanga kutekeleza jumla ya miradi tisa ya maendeleo. Kati ya miradi hiyo, miradi minne itatekelezwa kutokana na bajeti ya SMZ pekee na mitano itatekelezwa kwa mashirikiano kati ya serikali na washirika mbali mbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi. Jumla ya shilingi 4,500,000,000/- za SMZ na shilingi 52,810,054,000/- za wahisani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya miradi mbali mbali katika mwaka wa fedha 2011/2012. Malengo ya mradi mmoja mmoja yatakuwa ni kama ifuatavyo:-

Mradi wa Upanuzi wa Uimarishaji wa Huduma za Maktaba:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee na una malengo yafuatayo:-

(a) Kuanza ujenzi wa Maktaba Kuu Pemba.

(b) Kununua vitabu vya maktaba.

Jumla ya shilingi 150,000,000/- za SMZ zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mradi wa Uimarishaji wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar:
Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ambao unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu ya Afrika (*BADEA*) una malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa majengo manne ya chuo.

ii) Kununua vifaa vya maabara, samani na vipoza hewa.

iii) Kununua na kufunga vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

iv) Kuanza kutumia majengo ya chuo kikuu.

Mradi umepangiwa kutumia jumla ya shilingi 1,725,000,000/- za SMZ na shilingi 4,380,000,000/- kutoka *BADEA.*

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ, Serikali ya Watu wa China, wananchi na Mashirika mbalimbali ya maendeleo yakiwemo *USAID, UNICEF,* Shirika la Maendeleo la Sweden (*Sida*) pamoja na wahisani wengine. Mradi huu una malengo yafuatayo:-

i. Kukamilisha ujenzi wa madarasa 200 yaliyoanzishwa na Wananchi.

ii. Kujenga skuli moja ya msingi katika Wilaya ya Magharibi Unguja.

iii. Kuwapatia walimu mafunzo mbalimbali yakiwemo ya matumizi ya lugha ya Kiingereza kwa ajili ya kufundishia, mafunzo juu ya mtaala mpya wa ngazi ya msingi na mafunzo juu ya kufundisha katika mfumo wa elimu mjumuisho.

iv. Kutoa mafunzo kwa walimu juu ya matumizi ya kompyuta na uwekaji wa takwimu za skuli kwa kutumia kompyuta.

v. Kuzifanyia ukarabati skuli 15 Unguja na Pemba. Kukamilisha ujenzi wa nyumba tatu za walimu.

vi. Kuchonga madawati 5,000.

vii. Kutoa mafunzo kazini kwa walimu wasiosomea kwa njia ya elimu masafa.

viii. Kuandika, kuchapisha na kusambaza vitabu vya kiada na viongozi vya walimu wa madarasa ya I-IV.

ix. Kuandika na kuchapisha moduli za kutolea mafunzo kazini kwa walimu wa sayansi na hisabati.

Jumla ya shilingi 1,000,000,000/- za SMZ, shilingi 2, 250,000,000/= za Jamhuri ya Watu wa China na shilingi 4,969,938,000/- kutoka Sida, *USAID* na *UNICEF* zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha malengo ya mradi huu.

Mradi wa Chuo cha Kiislamu Micheweni Pemba:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee na utakuwa na malengo yafuatayo:-

(i) Kujenga uzio kuzunguuka eneo la chuo.

(ii) Kuendeleza ukarabati wa majengo yaliyopo.

Jumla ya shilingi 50,000,000/- za SMZ zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa malengo haya.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu utatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kutoa mikopo kwa vikundi vya ushirika 20 vya akinamama, wajasiriamali na kwa wahitimu wa vituo vya mafunzo ya amali wenye lengo la kujiajiri wenyewe.

ii) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala huko Wingwi Mtemani Pemba.

iii) Kununua samani na vifaa vya kufundishia.

iv) Kununua vifaa mbali mbali ikiwemo magari, kompyuta, printa kwa ajili ya ofisi ya mradi wa Elimu Mbadala na Amali awamu ya pili.

v) Kutafuta washauri ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya elimu mbadala na amali, ujenzi na ukarabati wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume na ujenzi na ukarabati wa Chuo cha Utalii Maruhubi.

vi) Kutangaza zabuni za ujenzi wa vituo vya elimu mbadala na amali, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume na Chuo cha Utalii Maruhubi.

vii) Kuandaa mitaala na mafunzo ya wakufunzi wa vituo.

Jumla ya shilingi 150,000,000/- za SMZ na shilingi 3,000,000,000/= za *ADB* zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ, Benki ya Dunia na *BADEA*. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i. Kununua baadhi ya vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa madarasa ya sekondari.

ii. Kuchonga seti 20,750 (za meza na viti) kwa ajili ya wanafunzi wa skuli za sekondari.

iii. Kukamilisha ujenzi wa skuli za sekondari 16 Unguja na Pemba.

iv. Kukamilisha ujenzi wa Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa Mchanga Mdogo Pemba.

v. Kununua vifaa vya Ofisini.

vi. Kuendelea na ukarabati wa skuli sita za sekondari za Forodhani, Tumekuja, Hamamni, Fidel Castro, Utaani na Uweleni.

vii. Kuanza ujenzi wa skuli za sekondari za ghorofa katika maeneo ya Kiembesamaki, Kwamtipura, Mpendae, Kibuteni kwa upande wa Unguja na Mkanyageni huko Pemba.

viii. Kufunguliwa kwa skuli 16 za Sekondari na Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa.

Mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 900,000,000/- za SMZ, shilingi 40,500,000,000/- kutoka Benki ya Dunia na shilingi 3,930,054,000/- za *BADEA*.

Mradi wa Ukamilishaji wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 25,000,000/- za SMZ na utakuwa na lengo la kutayarisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la pili la Wizara.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee. Malengo ya mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa madarasa manne mapya katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi, Kengeja.

(ii) Kuandaa michoro ya ujenzi wa dakhalia ya Skuli ya Sekondari ya Ufundi, Kengeja.

(ii) Kuipatia skuli ya Sekondari ya Ufundi, Kengeja vifaa vya karakana.

(iii) Kuendelea na ukarabati wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume.

Mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 400,000,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa malengo yaliyopangwa.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya SMZ na *UNICEF*. Malengo ya mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutayarisha sera ya elimu ya maandalizi.

(ii) Kuendelea kutoa mafunzo juu ya mtaala mpya kwa walimu wa skuli za maandalizi.

(iii) Kuanza kutoa mafunzo ya ualimu wa maandalizi kwa njia ya radio kwa walimu 1,000.

(iv) Kununua vifaa vya kufundishia.

Mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 200,000,000/- za SMZ na dola za kimarekani 307,000.00 za *UNICEF*.

Utafiti:

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imeweka kipaumbele katika kufanya utafiti wa masuala mbali mbali ya elimu. Hivi sasa iliyokuwa Seksheni ya Utafiti imepandishwa daraja na kuwa divisheni chini ya Idara ya Sera, Mipango na Utafiti. Shughuli za utafiti zimeendelea kufanyika katika kipindi hiki. Wizara inaendelea na uandishi wa ripoti ya utafiti wa *SACMEQ* wenye lengo la kupima ubora wa elimu itolewayo katika ngazi ya elimu ya msingi kwa kigezo cha uwezo wa wanafunzi wa darasa la sita.

Utafiti huo unajumuisha nchi 15 za Kusini mwa jangwa la Sahara zikiwemo Zanzibar na Tanzania Bara. Pia walimu mbali mbali walioko masomoni wamefanya tafiti za kielimu kama ni sehemu ya masomo yao. Tafiti hizo zitatumika katika kurekebisha makosa yaliyoonekana katika utoaji wa elimu. Katika mwaka 2011/2012, wizara yangu inakusudia kufanya utafiti juu ya uwezo wa wanafunzi wa madarasa ya awali ya msingi wa kusoma, kuandika na kuhesabu. *(Makofi)*

Ukusanyaji na Uchambuzi wa Taarifa za Elimu:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, wizara ilitoa mafunzo kwa walimu wanaoshughulikia uwekaji takwimu za elimu katika skuli baada ya marekebisho ya madodoso yanayosambazwa katika skuli kwa ajili ya kukusanyia taarifa za mwaka. Upatikanaji wa taarifa hizo unasaidia kuratibu mipango na programu za elimu kitaifa (mfano, MKUZA, utekelezaji wa sera ya elimu), na Kimataifa (mfano, *EFA*, *MDG's* n.k).

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni moja ya nchi zilizomo katika majaribio ya mfumo wa uwekaji taarifa katika skuli kwa Kanda ya Afrika. Hivyo Zanzibar ilikuwa ni mwenyeji wa warsha ya siku tatu ilyofanyika kuanzia tarehe 4-6 Mei, 2011 ilioandaliwa na Jumuia ya Kuendeleza Elimu katika Afrika (*ADEA - WGEMPS*) kwa nchi saba ikiwemo Bukina Faso, Ghana, Guinea, Senegal, Uganda, Zimbabwe na wenyeji Zanzibar.

Warsha hiyo ilikuwa na madhumuni ya kubadilishana uzoefu na utaalamu katika mfumo wa uwekaji wa taarifa katika skuli na pia maandalizi ya awamu ya pili ya uingizaji wa mfumo wa uwekaji taarifa za skuli katika mitaala ya vyuo vya ualimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, wizara itaendelea na uimarishaji wa mfumo wa kuweka taarifa katika ngazi za skuli kwa kuendelea na utoaji mafunzo kwa walimu wakuu na walimu wanaoshughulikia uwekaji taarifa za elimu katika skuli na maafisa wa elimu wilaya.

Mfumo huo wa uwekaji taarifa katika skuli unatarajiwa kuimarisha ubora wa taarifa za elimu ambazo zitasaidia kupima utekelezaji wa mipango mbali mbali ya elimu kuanzia ngazi ya skuli hadi Taifa. Pia, Wizara kwa kushirikiana na *USAID* inakusudia kuimarisha kazi za ukusanyaji wa takwimu za skuli kwa kuongeza upatikanaji wa vifaa hasa kompyuta na kuandaa mafunzo kwa watendaji na walimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 276,500,000/- kwa Unguja na shilingi 70,095,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI:

Mhe. Mwenyekiti, idara hii inahusika na masuala yote ya kiutumishi na uendeshaji. Miongoni mwa majukumu yake ni ajira za wafanyakazi, kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuwachukulia hatua za kinidhamu wanaokiuka taratibu za kisheria na maadili ya kazi. Idara hii pia inahusika na shughuli za upatikanaji wa vitendea kazi, kuratibu safari za wafanyakazi wote wa wizara za ndani na za nje ya nchi, utunzaji wa nyaraka za wafanyakazi na majengo ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, idara ilinunua vyombo vya usafiri na vitendea kazi mbali mbali ambavyo vimesaidia katika kuinua ufanisi wa kazi. Wizara ilinunua gari tano kwa matumizi ya Idara ya Nyaraka na Mambo ya Kale, Idara ya Ukaguzi wa Elimu, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Gari moja kati ya hizo imepelekwa katika Ofisi yetu ya Pemba kwa shughuli za Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi. Pia, Vespa 15 zilinunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya zote za Unguja na Pemba na 5 nyengine kwa matumizi ya Waratibu wa Elimu Mbadala na Watu Wazima na Maafisa wengine wa Idara mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, wizara iliajiri jumla ya walimu 88 wakiwemo 05 wa shahada ya pili, 81 wa shahada ya kwanza na 02 wa Stashahada. Katika jitihada za kuwaendeleza watumishi wetu kielimu, wafanyakazi 399 wamejiunga na masomo ya ngazi mbali mbali kati yao 05 wanachukua mafunzo ya cheti, 79 mafunzo ya stashahada, 288 mafunzo ya shahada ya kwanza na wafanyakazi 27 mafunzo ya shahada ya pili. Pia wafanyakazi 113 wamerudi kutoka masomoni, kati yao wanaume ni 62 na wanawake 51. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, wafanyakazi 102 walistaafu kazi kwa mujibu wa sheria, 27 walifariki dunia (Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi Amin), 03 walifukuzwa kazi kwa makosa mbali mbali na 08 waliacha kazi kwa hiari yao. Aidha wafanyakazi 24 walipewa uhamisho kwenda kuendelea na kazi katika taasisi mbali mbali za serikali na wengine 77 walichukua likizo bila ya malipo.

Hadi kufikia mwezi wa Juni 2011, wizara ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 13,893 kati yao 8,436 ni wanawake na 5,457 wanaume. Unguja wapo wafanyakazi 10,100 na Pemba wapo 3,793. Kati ya wafanyakazi wote, wafanya kazi 12,278 wako katika kada ya ualimu kati yao wanaume ni 4,397 na wanawake ni 7,881. Pia wapo wafanyakazi wasiokuwa walimu 1,615.

Mhe. Mwenyekiti, katika juhudi za kuwasaidia wafanyakazi wetu kujikwamua na baadhi ya matatizo ya kimaisha, Wizara imewadhamini wafanyakazi katika kupata mikopo ya fedha taslim, vifaa vya ujenzi, vipando na vifaa vya matumizi ya nyumbani. Kwa ujumla wafanyakazi 3,013 walifaidika na mikopo hiyo yenye thamani ya shilingi 462,000,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuushukuru uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya Posta, Benki ya *FBME*, Benki ya *CRDB*, ushirika wa kuweka na kukopa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Kampuni nyengine za watu binafsi kwa kuwapatia watumishi wa wizara yangu mikopo ya fedha taslimu na vifaa mbali mbali. Nawaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuwasaidia wafanyakazi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, idara itaandaa mpango wa mafunzo ya wafanyakazi wote ili kujua mahitaji halisi, kukamilisha upembuzi yakinifu juu ya mahitaji halisi ya walimu kwa kila skuli na kwa kila somo na kuwapatia mafunzo maalum maofisa wa uendeshaji na utumishi katika Idara na Taasisi za Wizara. Mafunzo haya yatalenga katika kuwajengea uwezo zaidi wa utendaji. Pia dara itasimamia upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya mahitaji ya ofisi zetu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 idara hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 24,192,561,000/- kwa Unguja na shilingi 8,678,064,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, ina majukumu ya kusimamia utoaji wa elimu kwa ngazi ya elimu ya maandalizi na ile ya msingi katika skuli za Serikali na za Binafsi. Pia inaratibu wa shughuli za Vyuo vya *Quraan* na Madrasa. Aidha, idara ina jukumu la kushughulikia huduma za wanafunzi maskulini.

ELIMU YA MADRASA NA VYUO VYA *QURAAN*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, kuna jumla ya Vyuo vya *Quraan*/Madrasa 2,187 Unguja na Pemba vyenye walimu 8,890 na wanafunzi 282,025. Idara iliandaa mafunzo ya walimu 800 wa Vyuo vya Quraan na madrasa wakiwemo wanaume 562 na wanawake 238 Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalilenga katika njia shirikishi za kujifunzia, matumizi ya adhabu mbadala kwa wanafunzi, matayarisho ya vifaa na visaidizi rahisi vya kufundishia na uelewano, mahusiano na mashirikiano kati ya taasisi mbali mbali zinazoshughulikia Dini ya Kiislamu za nje na ndani ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kulishukuru Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (*UNICEF*) kwa kugharamia mafunzo hayo ambayo yameleta faida kubwa kwa walimu na wanafunzi wetu. Pia, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza baadhi ya wafadhili waliojitolea kuvisaidia Vyuo vya *Quraan* na kuwalipa mishahara walimu wake.

Napenda kutoa wito kwa watu wengine wakiwemo wafanyabiashara, Wabunge na Wawakilishi kujitokeza katika kusaidia mahitaji mbali mbali ya Vyuo vya *Quraan* na Madrasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, idara itawapatia mafunzo walimu 1,000 wa vyuo vya *Quraan* na Madrasa kwa lengo la kuwajengea uwezo zaidi wa kazi zao. Pia, idara itawatafutia misaada mbali mbali ya vitabu vya kufundishia na kujifunzia (ikiwemo misahafu na juzuu) kwa kupitia wafadhili mbali mbali wa nje na ndani ya nchi yetu.

Vile vile, Idara imeazimia kuwajengea uwezo zaidi Maafisa wa Divisheni ya Madrasa na Vyuo vya *Quraan* ili kufanya kazi zao kwa uhakika, uelewa na umahiri mkubwa.

ELIMU YA MAANDALIZI

Mhe. Mwenyekiti, idara imeendelea na juhudi za kuelimisha na kuhamasisha jamii kuwapeleka watoto wenye umri wa miaka 4 na 5 katika Skuli za Maandalizi. Kumekuwa na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaohudhuria masomo katika ngazi hii katika sehemu za mjini na vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/2011, idadi ya skuli za maandalizi zilizosajiliwa ni 244, kati ya hizo 29 ni za serikali na 215 ni za binafsi. Pia zipo skuli 36 za msingi na skuli 19 za msingi na kati zenye madarasa ya elimu ya maandalizi. Skuli na madarasa ya elimu ya maandalizi ya serikali yana jumla ya wanafunzi 6,876, kati yao wanawake ni 3,500 na wanaume ni 3,376. Kwa upande wa Sekta Binafsi, wapo wanafunzi 19,524 wakiwemo wanawake 9,953 na wanaume 9,378. Jadweli Namba 13 (c) inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaendeleza mradi wa "*Radio Instruction to Strengthen Education" (RISE)* unaotoa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio kwa wanafunzi wa Wilaya ya Kaskazini (A) na Wilaya ya Magharibi kwa Unguja na Wilaya ya Micheweni kwa Pemba, licha ya kwamba ufadhili wa mradi huo umekwisha. Kwa hivi sasa vipo jumla ya vituo 179 vya elimu ya maandalizi kwa njia ya redio Unguja na Pemba vyenye jumla ya wanafunzi 7,022, kati ya hao wanawake ni 3,650 na wanaume 3,372. Jadweli Namba 13 (c) inatoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kulishukuru Shirika la Kimataifa la Misaada la Marekani (*USAID*) na jumuiya ya "*Education Development Corporation*" kwa msaada mkubwa waliotupa ukiwemo utaalamu na vifaa vya utekelezaji wa mradi. Vile vile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Wilaya za Micheweni Pemba, Kaskazini (A) na Magharibi Unguja kwa kuhamasika na kuupokea mradi huu kwa kupelekea watoto wao kwa wingi katika vituo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2010/2011, wizara kwa kushirikiana na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNICEF* na *UN-JOINT PROGRAMME* 5 ilitoa mafunzo kazini kwa walimu wanaofundisha madarasa ya elimu ya maandalizi. Mafunzo hayo yalihusisha taaluma za njia shirikishi za kufundishia watoto wadogo, utengenezaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia vitu vilivyomo katika mazingira yetu, namna ya kuwapokea na kuwaendeleza watoto wanaomaliza elimu ya maandalizi na kuanza darasa la kwanza bila ya kuathiri makuzi yao ya kielimu, kiafya na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, wizara yangu imekusudia kupanua wigo wa elimu hii kwa kuongeza vituo vya elimu ya maandalizi kwa njia ya redio katika maeneo mengine ya Unguja na Pemba ambayo hayana vituo vya elimu ya maandalizi. Wizara inaomba mashirikiano na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu katika kuwahamasisha wananchi katika majimbo yenu kuupokea utaratibu wa kutoa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio.

ELIMU YA MSINGI

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya msingi inatolewa katika Skuli 321 zikiwemo 249 za Serikali na 72 za Binafsi. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, idadi ya wanafunzi katika skuli za msingi imefikia 237,690 sawa na asilimia 118.5 ikilinganishwa na wanafunzi 226,746 sawa na asilimia 112.0 katika mwaka 2010. Pia, watoto wote 31,081 walioandikishwa kuanza darasa la kwanza mwaka 2011 wamepatiwa nafasi za kusoma licha ya kuwepo kwa msongamano mkubwa madarasani. Miongoni watoto hao 15,500 ni wanaume na 15,581 ni wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, walimu wa skuli za msingi mbali na kupatiwa mafunzo juu ya mbinu za ufundishaji kwa kuingiza dhana ya Elimu ya Mazingira kwa masomo ya Hisabati, Kiingereza na Sayansi, pia wamepatiwa mwongozo wa kuwasaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, walimu wa madarasa ya kwanza wamepatiwa mafunzo ya mbinu shirikishi za kujifunza zinazowajali wanafunzi na kuwajengea mazingira yatakayowawezesha kuwapatia watoto haki zao zote za kielimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia watoto duniani (*UNICEF*) na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inakusudia kutoa mafunzo juu ya mbinu za kukomesha utumikishwaji wa watoto kama mpango wa Kitaifa unavyoelekeza. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, tutaendelea na mpango wa kutokomeza maradhi ya kichocho kwa watoto wetu maskulini.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa uhamasisha walimu juu ya matumizi ya adhabu mbadala maskulini unaofadhiliwa na Shirika la "*Save the Children*" unaendelea vizuri. Utekelezaji wa mradi huo umeanza kwa skuli 10 za majaribio; moja kwa kila Wilaya, hivyo unajumuisha skuli sita kutoka Unguja na skuli nne kutoka Pemba.

Lengo kubwa la mradi huu ni kuwahamasisha walimu wa skuli, walimu wa Vyuo vya *Quraan*, walezi na wazazi kutumia adhabu mbadala badala ya kutoa adhabu zenye madhara kwa wanafunzi na watoto majumbani. Hii itasaidia kujenga uhusiano mzuri baina ya walimu na wanafunzi wao, wazee na watoto wao na jamii kwa ujumla.

Hadi sasa mradi umehamasisha walimu, kamati za skuli, masheha, Serikali za wanafunzi, wakaguzi, maofisa wa Elimu Wilaya na Mikoa na walimu wa madrasa na Vyuo vya *Quraan*. Skuli zilizomo katika mradi huu ni Regezamwendo, Kinyasini, Fujoni, Kisiwandui, Kitogani na Marumbi kwa Unguja na Pondeani, Ngo'mbeni, Wingwi na Minungwini kwa Pemba.

HUDUMA ZA WANAFUNZI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa 2010/2011, jumla ya skuli 218 zimefanya uchaguzi wa viongozi wapya wa serikali za wanafunzi. Viongozi hawa wamekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na walimu katika kazi mbali mbali za uendeshaji na utunzaji wa mazingira ya skuli. Viongozi wa serikali za wanafunzi wamefanya ziara mbali mbali za kutembeleana na kubadilishana mawazo juu ya utendaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, wizara yangu itaendelea kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapatiwa haki yao ya elimu iliyo bora kwa kuwajengea mazingira rafiki yanayomjali mtoto bila ya ubaguzi au vikwazo vyovyote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 idara hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 101,000,000/- kwa Unguja na shilingi 14,365,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA ELIMU YA SEKONDARI

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina jukumu la kusimamia utoaji wa elimu katika Skuli za Sekondari za Serikali na za Watu Binafsi kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita. Katika mwaka 2010/2011, Idara ilisimamia skuli 238 kati ya hizo Skuli 201 ni za Serikali na 37 ni za Watu Binafsi.

Hadi mwezi wa Machi 2011, walikuwepo jumla ya wanafunzi 49,934 wa sekondari katika ngazi ya sekondari ya awali (kidato cha I na cha II) ambao ni sawa na asilimia 85.1, kati ya hao Unguja walikuwepo wanafunzi 34,586 na Pemba ni 15,348. Jadweli Namba 16 inatoa ufafanuzi zaidi.

Pia, kwa upande wa kidato cha tatu, nne na elimu ya ufundi walikuwepo wanafunzi 27,737 kati yao Unguja ni wanafunzi 18,465 na Pemba ni 9272. Kwa upande wa skuli zenye kidato cha tano na sita ziko skuli 30 kati ya hizo Unguja ni 24 na Pemba ni 6. Kwa ujumla idadi ya wanafunzi katika ngazi ya sekondari (kidato cha 1 hadi cha 6) imefikia 81,853, kati yao 38,075 ni wanaume na 43,778 ni wanawake. Jadweli namba 21 na 22 zinatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Idara imefungua madarasa ya kidato cha tano katika skuli za Mpapa, Mkwajuni na Vikokotoni kutokana na ongezeko la wanafunzi waliopata sifa za kuendelea na masomo ya sekondari ya juu. Pia, imefungua madarasa ya kidato cha tatu katika skuli za Bwefum, Maungani na Ubago. Pia skuli za Bandamaji, Kama na Mbuzini Unguja zimefungua madarasa ya kidato cha kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Idara inakusudia kufungua skuli mpya 16 za sekondari na pia inakusudia kuongeza walimu wenye sifa hasa wa masomo ya sayansi. Mbali na kuongeza idadi ya skuli na walimu, Idara inakusudia kuongeza idadi ya vitabu vya kusomea kwa wanafunzi na walimu pamoja na vifaa vya maabara.

HUDUMA ZA DAKHALIA

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011, dakhalia zetu zilihudumia jumla ya wanafunzi 1,527 (wanaume 917 na wanawake 610) kama inavyoonekana katika jadweli Namba 24. Idadi hii imepungua kidogo ukilinganisha na wanafunzi 1,993 waliokuwepo 2009/2010. Wanafunzi wanaoishi dakhalia ni wale tu wanaojitegemea kwa chakula, kutokana na wizara kusitisha huduma za dakhalia zilizotokana na ukosefu wa fedha za kutosha za kuwahudumia wanafunzi.

Napenda kuwashukuru wazazi, na wanadakhalia wote kwa uvumilivu, utulivu na ushirikiano mkubwa wanaouonesha katika kukabiliana na hali hii. Wizara itaendelea na juhudi zake za kufungua madarasa ya sekondari katika sehemu mbali mbali za nchi yetu ikiwa ni mbinu mojawapo ya kukabiliana na tatizo la wanafunzi kufuatilia skuli maeneo ya mbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Idara inakusudia kuimarisha huduma za Afya kwa kuweka kisanduku cha huduma ya kwanza katika dahalia zetu zote na kuhakikisha kuwa mazingira ya dakhalia yanakuwa ya kuvutia kwa kupanda bustani za mauwa.

SERIKALI ZA WANAFUNZI

Mhe. Mwenyekiti, Serikali za wanafunzi zimewekwa maskulini kwa ajili ya kuwasaidia walimu katika kazi za usafi wa skuli, nidhamu za wanafunzi pamoja na kuwaandaa wanafunzi kwa kazi za uongozi baada ya kumaliza skuli. Katika kujua umuhimu wa serikali za wanafunzi, NGO iitwayo "*USEWAZA"* iliyoanzishwa mwaka 2009 imeamsha ari za wanafunzi pamoja na jamii kutokana na kurusha vipindi vya TV hewani kupitia TVZ. Vipindi hivi vimeleta mwanga mkubwa katika jamii. Miongoni mwa vipindi vilivyoamsha ari kwa wazazi ni kero za wenye daladala kwa wanafunzi, mimba za utotoni na athari zake, athari za madawa ya kulevya na wazazi kuwashirikisha wanafunzi katika biashara. Katika mwaka 2011/2012, Idara inakusudia kuendesha mafunzo kwa viongozi wa Serikali za wanafunzi katika skuli 25 za Unguja na Pemba kwa lengo la kuwawezesha viongozi wa wanafunzi kuwasimamia wanafunzi wenzao kwa ufanisi zaidi.

KAZI ZA UJASIRIAMALI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, kazi za ujasiri amali zimeendelezwa katika maskuli kwa lengo la kuwafunza wanafunzi mbinu mbali mbali za kujitegemea, kuthamini kazi na kuziwezesha skuli kupata mapato ya kuendesha shughuli zao mbali mbali. Kazi za amali zimeziwezesha skuli nyingi kupata fedha za kusaidia matatizo mbali mbali kama vile matengenezo madogo madogo na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na michezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 159,236,000/- kwa Unguja na Tsh. 19,615,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu ni Idara mpya iliyoanzishwa mwaka 2011. Idara hii ina majukumu ya kuandaa na kusimamia Sera ya teknohama katika elimu, kuratibu na kutoa mafunzo ya teknohama kwa watendaji wa Wizara, kusimamia matumizi sahihi ya teknohama tangu katika ofisi zetu zote za elimu, kuitumia teknolojia hii katika kusoma na kufundishia katika ngazi mbali mbali za elimu kuanzia skuli za Maandalizi, Msingi, Sekondari, vyuo vya amali, Vyuo vya Ualimu hadi Vyuo Vikuu vilivyopo Zanzibar. Pia inajukumu la kutayarisha na kusimamia programu mbali mbali za kompyuta ambazo zitasaidia katika kuleta ufanisi

bora wa majukumu ya Wizara kama vile programu za *EMIS*, uchambuzi wa mitihani ya taifa, "*database"* la watumishi wa wizara n.k. Sambamba na hayo, Idara hii inajukumu la kusimamia utekelezaji wa miradi ya teknohama, kufanyia matengenezo ya vifaa vya teknohama pamoja na kuishauri Wizara juu ya maendeleo ya teknohama.

Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa mashirikiano na washirika mbali mbali wa maendeleo imepanga kukamilisha Sera ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika elimu. Kukamilika kwa sera hio kutaiwezesha Wizara kuwa na dira madhubuti ya maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mhe. Mwenyekiti, Idara kwa mashirikiano na Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi inaendelea kutoa mafunzo mbali mbali ya teknohama na matumizi yake katika kusoma na kufundishia. Programu za kufundisha watoto wa maandalizi kwa njia ya Redio imeimarishwa kwa kuzipatia vifaa vya kisasa *(Solio, iPod, projekta, spika na Redio za MP*3*)* vitakavyotumika katika mafunzo hayo kwa vituo vyote vya walimu, pamoja na skuli zote za serikali za Serikali Unguja na Pemba. Lengo kuu la kusambaza vifaa hivyo ni kuwapa mafunzo walimu jinsi ya kufundisha madarasa ya maandalizi na yale ya ngazi ya msingi ya awali kwa darasa la kwanza na la pili.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha mpango wa mafunzo ya teknohama ni endelevu, Idara yangu katika mwaka 2011/2012, inakusudia kutekeleza mambo yafuatayo:

a) Kushirikiana na jamii katika kuviendeleza vituo vya kufundishia watoto kwa njia ya redio.

b) Kutayarisha na kueneza vifaa vya kufundishia kwa njia ya michezo katika vituo vyote na skuli zenye madarasa ya "Tucheze Tujifunze*" (TUTU).*

c) Kuwajengea uwezo walimu na wafanyakazi wengine wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuandaa programu za kufundishia watoto kwa njia ya redio na video, na kompyuta pamoja na ufuatiliaji wake.

d) Kutoa taaluma kwa Maafisa wa Mkoa, Wilaya, TC na walimu juu ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, Idara inakusudia kuandaa mafunzo ya matumizi ya kompyuta kwa walimu wawili kwa kila skuli zitakazoanza katika mradi wa "*21st Century Basic Education*". Ili kuhakikisha mafunzo hayo ya teknohama yanakuwa na mafanikio na endelevu, Idara inakusudia kutoa mafunzo maalum ya teknohama kwa wakufunzi 15 ambao watatumika katika kutoa mafunzo kwa walimu kupitia vituo vyote vya Ualimu Unguja na Pemba. Mafunzo haya pia yatawalenga washauri ya vituo vya uwalimu.

Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kusambaza taarifa mbali mbali kwa washirika wake na jamii kwa ujumla. Wizara imeanzisha tovuti yake ambayo ina taarifa mbali mbali yakiwemo matokeo ya Mtihani wa kidato cha pili. Hatua hii pia itawawezesha watu mbali mbali walioko nje ya nchi kupata taarifa mbali mbali za maendeleo ya elimu yetu kwa urahisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 57,000,000/- kwa Unguja na Tsh. 10,000,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar imeanzishwa katika nafasi ya Idara ya zamani ya Ukaguzi wa Elimu. Ofisi hii ni chombo kitakachojitegemea na ina jukumu la kuzikagua skuli zote za serikali na za binafsi ili kuhakikisha kuwa ubora wa elimu inayotolewa ni kwa mujibu wa mitaala na mihutasari inayokubaliwa na Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, kazi za ukaguzi ziliimarika zaidi hasa baada ya kupatikana usafiri wa mabasi mawili madogo mapya yaliyonunuliwa kwa ajili ya kuimarisha zaidi shughuli za ukaguzi. Jumla ya skuli 213 Unguja na Pemba zilifanyiwa ukaguzi. Idadi hii ni kubwa ukilinganisha na lengo la kukagua skuli 180. Jumla ya skuli 19 zilifanyiwa ukaguzi mkuu, 52 ukaguzi wa ziara, 83 ukaguzi wa ziara fupi fupi, 14 ukaguzi wa usajili, 09 ukaguzi maalumu na 36 ufuatiliaji. Skuli zilizokaguliwa zilishauriwa na baadaye kupatiwa ripoti. Vikao vya pamoja baina ya wadau wa elimu viliandaliwa mwishoni mwa kila ukaguzi mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha utendaji, semina zilifanyika ambapo mada 15 ziliwasilishwa kwa wakaguzi. Wakaguzi wenyewe waliandaa mada hizo na kuziwasilisha wakisaidiana na baadhi ya watendaji kutoka Idara nyengine. Miongoni mwa mada zilizowasilishwa ni pamoja na ukaguzi na usimamizi wa elimu, mafunzo kazini, utafiti wa vitendo, '*Quality Assurance*", uandishi wa ripoti, mchakato wa ukaguzi na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu inalengo la kuzikagua skuli 190 zikiwemo skuli 140 za serikali na 50 za binafsi. Kati ya hizo, skuli 20 zitafanyiwa ukaguzi mkuu, skuli 5 ukaguzi wa ziara, skuli 83 ukaguzi wa ziara fupi fupi, skuli 14 ukaguzi wa usajili, skuli 11 ukaguzi maalumu na skuli 11 ukaguzi wa ufuatiliaji. Ofisi pia inakusudia kuyaendeleza mafunzo ya wakaguzi, kuvipitia, kuvirekebisha na kuviweka pamoja viwango vya elimu ya lazima.

Pia inakusudia kuandaa mswada wa sheria inayounda Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Pia, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu itatayarisha ripoti ya mwaka ya tathmini ya ukaguzi, itaendesha mafunzo ya uongozi kwa wasaidizi walimu wakuu na kuendelea kufanya ufuatiliaji wa mafunzo ya uongozi yaliyotolewa kwa walimu wakuu katika kipindi kilichopita. Ili kufanikisha malengo ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, idadi ya wakaguzi itaongezwa ili kuwezesha kufanywa ukaguzi wa zaidi ya skuli moja kwa wakati mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi hii imepangiwa ruzuku ya Tsh. 80,000,000/- kwa kazi za kawaida.

TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu imeanzishwa kutokana na iliyokuwa Idara ya Mitaala na Mitihani. Taasisi hii ina majukumu ya kutayarisha mitaala na mihutasari ya masomo, utungaji na uchapishaji wa vitabu na usanifu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka 2010/2011, Taasisi ilisimamia ukusanyaji wa maoni juu ya ubora wa vijitabu vya wanafunzi wa elimu ya maandalizi vya masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha. Vile vile, ilisimamia ukusanyaji wa maoni juu ya ubora wa mihutasari ya skuli za maandalizi. Taarifa zilizokusanywa kuhusu ubora wa vitabu na mihutasari ya maandalizi zimeanza kufanyiwa kazi kwa ajili ya kufanya marekebisho katika vitabu na mihutasari hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi iliandaa mafunzo ya awali kwa wakaguzi wa elimu 28 pamoja na walimu wakuu 240 wa skuli za msingi za Serikali, juu ya matumizi ya mihutasari mipya ya elimu ya msingi ambayo hivi sasa inatumika maskulini kwa darasa la kwanza na pili. Pia Taasisi ya Elimu Zanzibar imetoa mafunzo kwa walimu 450 wa darasa la pili juu ya matumizi ya mihutasari mipya ya elimu ya msingi. Pia, Taasisi kwa msaada wa *UNICEF* ilifanya utafiti juu ya ubora wa mtaala wa stashahda ya Ualimu wa msingi. Taarifa za utafiti zitatumiwa kufanyia marekebisho ya mtaala huo.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ilisambaza mihutasari mipya ya elimu ya msingi kwa skuli zote za Unguja na Pemba. Pia, vitabu vya sekondari vya masomo ya Kiswahili, *English*, *Geography*, *Civics*, *History*, masomo ya ufundi, Biashara na Kompyuta vilisambazwa maskulini. Vitabu hivi vilinunuliwa chini ya Mradi wa Elimu ya Lazima.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa 2011/2012, Taasisi ya Elimu Zanzibar itasambaza vifaa vya maabara kwa skuli za sekondari 25 Unguja na Pemba pamoja na vituo vya walimu. Pia itasambaza vitabu vya maktaba kwa skuli za sekondari, vituo vya walimu na vyuo vya ualimu. Kazi nyengine zitakazofanywa ni hizi zifuatazo :-

i. Kurekebisha mihutasari ya Elimu ya Maandalizi.
ii. Kutayarisha viwango vya kubainisha ufikiwaji wa malengo ya elimu kwa madarasa ya nne hadi sita.
iii. Kushirikiana na Idara ya Mafunzo ya Ualimu katika kuupitia na kuurekebisha Mtaala ya Diploma ya Ualimu Msingi.
iv. Kuandika, kuchapisha na kusambaza vitabu vya wanafunzi na viongozi vya wanafunzi wa skuli za maandalizi.
v. Kuandika, kuchapisha na kusambaza vitabu vya wanafunzi na viongozi vya walimu kwa madarasa ya kwanza hadi darasa la tatu.
vi. Kuendeleza mafunzo ya awali ya matumizi ya mihutasari mipya ya elimu ya msingi kwa walimu wa darasa la tatu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Taasisi hii imepangiwa ruzuku ya Tsh. 54,000,000/- kwa kazi za kawaida.

IDARA YA ELIMU MBADALA NA WATU WAZIMA (KISOMO)

Mhe. Mwenyekiti, Juhudi za kufuta ujinga wa kutojua kusoma na kuandika zimeendelezwa. Katika mwaka 2010/2011, idadi ya wanakisomo ilikuwa ni

6,910 wakiwemo wanawake 6,048 na wanaume 862 Unguja na Pemba. Jadweli Namba 35 inatoa uchambuzi zaidi. Wanakisomo 6,263, kati yao wanawake walikuwa ni 5,470 na wanaume 793, wamefanyiwa upimaji katika hatua zote nne. Katika upimaji huo, jumla ya wanakisomo 509, kati yao wanawake 412 na wanaume 97 walikombolewa. Vilevile, Idara ilikamilisha utungaji wa vitabu vya Kiswahili na Hisabati, pamoja na miongozo ya vitabu hivyo kwa ajili ya madarasa ya kisomo. Aidha, Idara imetoa mafunzo kwa walimu wa kisomo 430 (202 Unguja 228 Pemba). Katika mwaka 2011/2012, Idara itaendelea na juhudi za kufungua madarasa mengi zaidi ya kisomo kila ambapo wananchi watakapojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika juhudi za kuhamasisha na kufanikisha kisomo cha Watu Wazima, Idara iliadhimisha Sherehe za Juma la Elimu ya Watu Wazima siku ya tarehe 8/9/2010 katika viwanja vya skuli ya Mwanakwerekwe ‘C’ kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba sherehe hizo zilifanyika kiwilaya, katika vituo vyote vinne vya walimu. Katika sherehe hizo vikundi vya Sayansi Kimu, na vikundi vya programu za wanawake vilipata fursa ya kuonesha bidhaa zao wanazozalisha pamoja na kuuza bidhaa hizo kwa wananchi waliohudhuria katika sherehe hizo. Maadhimisho ya sherehe hizo yataendelezwa katika mwaka 2011/2012 na kufikiria mbinu mpya za uhamasishaji wa jamii ili watu wengi zaidi wajiunge na kisomo cha watu wazima.

ELIMU MBADALA

Mhe. Mwenyekiti, Elimu mbadala inalenga kuwapatia elimu vijana wenye umri kati ya miaka 10 hadi 15 walioko nje ya skuli, wakiwemo walioacha masomo njiani kutokana na sababu mbali mbali. Katika mwaka 2010/2011, Elimu Mbadala imetolewa katika madarasa 38 Unguja na Pemba yenye jumla ya wanafunzi 879. Wanafunzi 604 wa madarasa ya elimu mbadala wameingizwa katika madarasa ya kawaida katika skuli mbali mbali baada ya kufikia viwango vinavyohitajika.

Pia, wanafunzi 06 kutoka kwenye madarasa ya elimu mbadala wamefaulu mtihani wa darasa la saba na kuchaguliwa kuingia katika madarasa ya kidato cha kwanza ya michepuo na wanafunzi 05 wamejiunga na kidato cha kwanza katika skuli za sekondari za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Elimu Mbadala cha Rahaleo, kina jumla ya wanafunzi 256 wakiwemo wanawake 67 na wanaume 179. Wanafunzi 127, kati yao wanawake 36 na wanaume 91 wametunukiwa vyeti baada ya kufaulu mafunzo katika fani za umeme, utunzaji wa nyumba na uchongaji.

VITUO VYA KUJIENDELEZA

Mhe. Mwenyekiti, Idara pia inashughulikia vituo vya kujiendeleza kwa vijana waliomaliza kidato cha pili, nne na sita ambao wanalengo la kujiendeleza kielimu. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya wanafunzi 4,826 kati yao wanawake 2,587 na wanaume 2,239 walisajiliwa katika vituo vya kujiendeleza. Jadweli Namba 36 inatoa uchambuzi zaidi. Kati ya watahiniwa wa faragha 9,383 waliofanya mitihani ya kidato cha Nne, mwaka 2010, watahimiwa 4,521, sawa na asilimia 48.18 wamefaulu mitihani yao. Kwa upande wa mitihani ya kidato cha sita, kati ya watahiniwa wa faragha 1,454 waliofanya mitihani hiyo, watahiniwa 782 walifaulu ikiwa ni sawa na asilimia 53.78 ya watahiniwa wote. Jadweli Namba 37 (a-c) inatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa somo la sheria kituo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 141 wakiwemo wanawake 52 na wanaume 89. Wanafunzi 100 kati ya hao ni wa kiwango cha stashahada na 41 ni kwa ngazi ya cheti. Wanafunzi 51 wa ngazi ya stashahada wamehitimu mafunzo yao wakiwemo wanaume 40 na wanawake 11. Kwa upande wa cheti, wanafunzi waliohitimu ni 19, wanawake 10 na wanaume 9.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, Idara itaendelea na juhudi zake za kufungua vituo zaidi vya kujiendeleza kila itapohitajika, na itaongeza wanafunzi wa somo la sheria kila itakapobidi kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 176,537,000/- kwa Unguja na Tsh. 10,143,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ina majukumu ya kusimamia na kuratibu maendeleo ya mafunzo ya amali hapa Zanzibar katika vituo vilivyoanzishwa na serikali na taasisi binafsi. Kwa jumla vituo vya mafunzo ya Amali vya Serikali vya Mwanakwerekwe, Mkokotoni na Vitongoji vina jumla ya wanafunzi 587 kati yao wanawake ni 139 na wanaume ni 448. Vijana hawa wanachukua mafunzo katika fani mbali mbali za ufundi zikiwemo useremala, ushoni, uungaji vyuma, uchoraji na uandishi, uwashi, ufundi bomba, umeme, teknolojia ya mawasiliano, huduma za mahoteli na mapishi, elektroniki, ufundi magari na ufundi mafriji.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka pia inaratibu shughuli mbali mbali za maendeleo ya mafunzo ya amali ikiwemo mitihani ya biashara "*National Business*

Examination (NABE)" na ile ya ufundi stadi (*Trade Test)* na "*Competency Based Education and Training*" *(BET)* inayotahiniwa na Mamlaka ya Elimu na Ufundi Stadi ya Tanzania. Jumla ya vijana 1,207 kati yao wanawake 426 na wanaume 781 walifanya mitihani hiyo. Jumla ya wanafunzi 652 (wanawake 273 na wanaume 400) walifaulu mitihani yao ikiwa ni sawa na asilimia 62. Jadweli Namba 41 (a – b) inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka inawaendeleza wafanyakazi na walimu wake ili waweze kufanya kazi zao kwa umakini na ufanisi zaidi. Jumla ya wafanyakazi 13 wamepatiwa nafasi za masomo katika ngazi za cheti (2), stashahada (10) na shahada ya Uzamili (1). Kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo ya Ualimu wa Ufundi Stadi, Morogoro, Mamlaka imewapatia walimu 60 wa vituo vya mafunzo ya amali, mafunzo ya mbinu za ufundishaji katika mfumo wa *CBET*. Mafunzo hayo yaliwajumuisha pia walimu kutoka vituo visivyokuwa chini ya Mamlaka.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, katika kuongeza ufanisi wa kazi, Mamlaka iliajiri walimu na wafanyakazi wapya 68 pamoja na kununua zana na vifaa vya kufanyia kazi katika ofisi zake na vya kufundishia katika vituo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Amali na Mafunzo ya mwaka 2005 na Sheria ya Mafunzo ya Amali Namba 8 ya 2006.
b) Kuijengea uwezo Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Bodi ya Wakurugenzi ya Mafunzo ya Amali kwa mujibu wa Sheria ya Mafunzo ya Amali Na 8 ya mwaka 2006 kama ilivyofanyiwa marekebisho kwa sheria Namba 11 ya 2007.
c) Kuanza ujenzi wa ofisi ya Mamlaka
d) Kuijengea uwezo jamii na wadau kuhusu muundo na taratibu, mipaka na majukumu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Bodi ya Wakurugenzi ya Mafunzo ya Amali.
e) Kuimarisha zaidi Mamlaka kwa kuongeza wafanyakazi na kuipatia vifaa, usafiri wa uhakika ili kuweza kufanya kazi mbali mbali za ufuatiliaji, mafunzo na shughuli nyengine za Mamlaka kwa ufanisi zaidi.
f) Kuongeza uwezo wa wafanyakazi wa Mamlaka kwa kuwapatia mafunzo kwa mujibu wa kazi na fani zao ndani na nje ya nchi.

g) Kuendelea kutoa mafunzo ya Ualimu na mafunzo ya viwandani kwa walimu watakaofundisha vituo vya mafunzo ya amali vyote vilivyosajiliwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.
h) Kuongeza ununuzi wa vifaa, zana, nyenzo na mitambo ya kufanyia kazi na kufundishia kwa lengo la kutoa mafunzo kwa walimu watakaofundisha vituo vyote vilivyosajiliwa vya Mafunzo ya Amali, vikiwemo vya Mwanakwerekwe, Mkokotoni na Vitongoji.
i) Kusajili upya vituo vyote vinavyotoa mafunzo ya Amali Unguja na Pemba
j) Kutoa na kusimamia mafunzo ya Amali kwa vijana 3,000 katika vituo mbali mbali vya Mafunzo ya Amali ndani na nje ya nchi.
k) Kuratibu Mafunzo ya Amali kwa vijana katika vituo mbali mbali vya Mafunzo ya Amali ndani na nje ya nchi.
l) Kutoa mafunzo ya Stadi za Maisha kwa wakufunzi, wafanyakazi na wanafunzi wa Vituo vya Mafunzo ya Amali.
m) Kutoa mafunzo ya Ujasiriamali kwa wakufunzi, wafanyakazi na wanafunzi wa vituo vyote vya Mafunzo ya Amali vilivyosajiliwa.
n) Kuendeleza uhusiano na mashirikiano kati ya Mamlaka na Mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yanayohusika na Mafunzo ya Amali kwa kuhudhuria mikutano na makongamano mbali mbali yanayojadili mafunzo ya amali.
o) Kuangalia maeneo ya uzalishaji na uwekezaji ili kuweza kutunisha mfuko wa Mamlaka.
p) Kwenda sambamba na malengo ya MKUZA na utekelezaji wa maazimio mbali mbali ya Umoja wa Mataifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara hii imepangiwa ruzuku ya Tsh. 1,200,000,000/- kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MAFUNZO YA UALIMU

Mafunzo ya Ualimu

Mhe. Mwenyekiti, Idara inasimamia mafunzo ya ualimu yanayotolewa katika chuo cha Kiislamu, Mazizini, Chuo cha Kiislamu, Micheweni na Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa cha Wete Pemba. Kwa mwaka 2010/2011, vyuo hivyo vilikua na jumla ya wanafunzi 355, kati yao wanaume 118 na wanawake 237.

Kati ya wanafunzi hao 31 walihudhuria mafunzo ya cheti cha ualimu wa elimu mjumuisho, 63 stashahada ya ualimu wa sekondari na 108 stashahada ya

ualimu msingi na 153 stashahada ya Dini na Kiarabu. Jadweli Namba 30 (a – c) inatoa ufafanuzi. Aidha jumla ya wanafunzi 619 wakiwemo wanaume 315 na wanawake 304 wamehitimu mafunzo ya ualimu katika vyuo hivyo mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, vyuo vya ualimu vinatarajiwa kuendelea kutoa mafunzo ya ualimu kwa kuandikisha wanafunzi wapya katika ngazi ya stashahada ya Ualimu Msingi na Sekondari na cheti cha Elimu Mjumuisho. Jumla ya wanafunzi wapya 461 wamechaguliwa kujiunga na mafunzo hayo kuanzia Julai 2011. Wizara inakusudia kuviimarisha vyuo vya ualimu kwa kuvipatia walimu wenye ujuzi, vifaa na usafiri. Mafunzo ya ualimu katika Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa yanatarajiwa kuimarika zaidi hapo mwakani baada ya kukamilika kwa ujenzi na kufunguliwa rasmi kwa kampasi mpya huko Mchanga Mdogo, Pemba.

MAFUNZO YA UALIMU KAZINI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Vituo vya Walimu vimeendelea kuratibu mafunzo ya ualimu kazini. Warsha mbali mbali za masomo zimeendeshwa ili kuweza kukidhi mahitaji ya walimu na skuli. Aidha wakufunzi 44 wanaofundisha masomo ya Kiingereza na Ualimu kwa njia ya elimu masafa wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imeendelea na utoaji wa mafunzo ya ualimu kwa njia ya elimu masafa kwa walimu wa skuli za msingi wasiosomea ualimu. Walimu 686 wakiwemo wanaume 122 na wanawake 564 wanaendelea na mafunzo katika ngazi ya daraja la *IIIB* kwenye vituo vyote tisa vya walimu vya Unguja na Pemba. Walimu hawa wamemaliza mafunzo yao ya daraja la *IIIB* katika mwezi wa Juni 2011 na kuanza mafunzo ya daraja la *IIIA* kuanzia mwezi Julai 2011.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imeendesha mafunzo ya kukuza uwezo wa kufundisha kwa walimu 500 wa Sayansi na Hisabati ngazi ya sekondari *(kidato cha tatu na nne).* Mafunzo hayo yameandaliwa kwa nia ya kuinua uwezo wa walimu hasa kutokana na wanafunzi wengi kufanya vibaya katika mitihani ya masomo ya Sayansi na Hesabati. Pia, Idara iliandaa mafunzo ya lugha ya Kiingereza na Mawasiliano kwa walimu wa Kiingereza msingi *(madarasa ya tano hadi sita)* kwa awamu ya kwanza.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha walimu hao kufundisha masomo ya madarasa ya tano na sita kwa kiingereza kwa mujibu wa mtaala mpya. Vile vile, jumla ya walimu 420 wamepatiwa mafunzo hayo. Aidha, Idara kwa kushirikiana na "*British Council*" imetoa mafunzo ya matumizi ya Kiingereza

kama ni lugha ya kufundishia kwa wakufunzi 22 kutoka katika Vyuo vya ualimu na vituo vya walimu Unguja na Pemba. Wakufunzi hao wameandaliwa kuendesha mafunzo kama hayo kwa walimu wa sekondari katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Idara ilitoa mafunzo ya *"data base"* kwa wafanyakazi wake 17. Aidha makarani 14 walipatiwa mafunzo ya udhibiti wa Ofisi Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Idara, inakusudia kuyaimarisha mafunzo ya ualimu kwa kuviimarisha vituo vya walimu. Pia, Idara itaendelea kutoa mafunzo mbali mbali kwa walimu kuhusiana na masomo wanayofundisha na mbinu bora za kufundishia masomo hayo kwa kupitia Vituo vya Walimu. Vile vile, Idara itaendeleza programu ya kukuza uwezo wa lugha ya Kiingereza na Mawasiliano kwa walimu wa Kiingereza msingi *(darasa la tano hadi la sita)* katika awamu ya pili.

Aidha, Idara itaandaa na kusimamia mafunzo kwa walimu wa skuli za maandalizi yatakayotolewa kwa njia ya redio kwa kupitia vituo vya walimu. Pia itatoa mafunzo ya elimu mjumuisho kwa walimu wote na mafunzo ya matumizi ya teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa walimu 300 wa Skuli za Sekondari na Vyuo vya Ualimu na kukamilisha Sera na Mafunzo ya Ualimu kazini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 130,000,000/- kwa Unguja na Tsh. 19,884,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

TAASISI ZA ELIMU YA JUU

Mhe. Mwenyekiti, Zipo taasisi nne za elimu ya juu hapa Zanzibar. Taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Chuo Kikuu cha Zanzibar, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume.

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimeendelea kuimarika zaidi. Katika mwaka 2010/2011, chuo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 774 wanaochukua mafunzo ya Shahada ya ualimu *(sayansi 141 na sanaa 633*), wanafunzi 40 wa shahada ya sayansi ya kompyuta, wanafunzi 47 wa stashahada ya ualimu *(sayansi),* wanafunzi 36 wa stashahada ya sayansi ya kompyuta na wanafunzi 19 wa cheti cha kompyuta.

Pia, Taasisi ya Elimu endelevu imeendelea kutoa huduma za kuwapatia elimu wananchi wanaopenda kujiendeleza katika fani mbali mbali. Jadweli Namba 26 (a) inatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar pia hutoa mafunzo ya lugha na elimu ngazi ya stashahada kupitia Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya wanafunzi 460, wakiwemo wanaume 141 na wanawake 319 wameendelea na masomo ya stashahada ya lugha. Pia wanafunzi 163 wa kigeni (wanaume 62 na wanawake 101) wamejiunga na *TAKILUKI* kujifunza lugha ya Kiswahili.

Mhe. Mwenyekiti, Mahafali ya sita ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar yalifanywa tarehe 17 Oktoba 2010. Aliekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ambae ni Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume aliwatunuku Shahada, Stashahada na vyeti wahitimu katika fani mbali mbali. Katika mahafali hayo jumla ya wahitimu 164, wakiwemo wanawake 49 walitunukiwa shahada ya kwanza. Kati yao, wanafunzi 105 walitunukiwa shahada ya Sanaa na Elimu; wanafunzi 43 walikuwa ni wa fani ya Sayansi na Elimu; na wahitimu wa shahada ya Sayansi na Kompyuta walikuwa ni 15. Kwa ngazi ya stashahada, wahitimu 99 walitunukiwa stashahada ya Lugha na Elimu na 11 wa fani ya Sayansi ya Kompyuta. Pia wahitimu 8 walitunukiwa vyeti katika fani ya Sayansi ya Kompyuta.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar kiliandaa sherehe rasmi za kumtawaza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, siku ya tarehe 29 Machi, 2011. Pia Rais amechagua Baraza jipya la Chuo kutokana na Baraza lilopita kumaliza muda wake.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/11, Chuo kiliimarisha mashirikiano yake na taasisi na vyuo vikuu mbali mbali vya nje. Miongoni mwa vyuo hivyo ni chuo kikuu cha "*South Carolina State University"* cha huko Marekani, Edward Mondlane cha Msumbiji, Chuo Kikuu cha Humbold cha Ujerumani na Chuo Kikuu cha Bristol cha Uingereza. Kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo wafanya kazi wake, Chuo kimewapeleka masomoni ndani na nje ya nchi wafanyakazi wake 8 ambapo 06 wanasoma ngazi ya shahada ya uzamivu na 02 ngazi ya shahada ya uzamili.

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka 2011/2012, Chuo kinatarajia kusajili wanafunzi 273 wa shahada ya kwanza na ualimu, 24 wa shahada ya kwanza ya sayansi ya kompyuta, 72 wa stashahada ya ualimu sayansi, 50 wa stashahada ya

sayansi ya kompyuta, wanafunzi 270 kwa masomo ya stashahada ya lugha na wanafunzi wa kigeni 215 kwa mafunzo ya muda mfupi ya lugha ya Kiswahili. Chuo pia kimeanzisha programu ya stashahada ya Uongozi wa Elimu na inatarajia kuchukua wanafunzi 50. Vile vile, Chuo Kikuu kinakusudia kuanzisha somo la Kitaliana kupitia Taasisi yake ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Katika mwaka 2011/2012, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kitaendelea kuimarisha shughuli zake zaidi kwa kuwapatia mafunzo zaidi wafanyakazi wake, kununua vifaa vya kujifundishia na kujifunzia na kuendelea kuchukua wanafunzi wapya katika fani na viwango mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Chuo hiki kimetengewa ruzuku ya Tsh. 3,600,000,000/- kwa kazi za kawaida.

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU CHUKWANI

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu kiliopo Chukwani kinaendelea na juhudi zake za kujiimarisha katika nyanja mbalimbali. Kwa mwaka 2010/2011, chuo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 1,055 wakiwemo wanawake 514 na wanaume 541.

Wanafunzi hao wanatoka katika nchi za Sudan, Kenya, Uganda, Somalia, Tanzania Bara na Zanzibar. Chuo pia kimeendelea na ujenzi wa madarasa na ofisi, ambao umegharimu Tsh. 1,017,000,000/-. Chuo kimetoa wahitimu 177 wanawake 68 na wanaume 109 katika mahafali ya 5 yaliyofanyika tarehe 22/1/2011 ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein alikuwa mgeni rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma zake, chuo kimenunua genereta la *KV 120* ambalo limeondoa kabisa tatizo la upatikanaji wa umeme pindi ukizimika kutoka gridi ya Taifa. Chuo pia kimeendelea na shughuli za uchapishaji wa majarida ya wakufunzi na taasisi nyengine zilizo nje ya Chuo kupitia kiwanda chake cha uchapishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, chuo kinatarajia kusajili wanafunzi wapya 400, kuajiri wahadhiri wanane wa fani mbali mbali na kufanya ukarabati wa kituo chake cha afya. Aidha kiwanda cha uchapishaji kitaendelea na kazi zake za kuhudumia jumuia ya chuo na Taasisi nyengine za Serikali na binafsi. Chuo kitaendelea kuwasiliana na makampuni ya mawasiliano kwa ajili ya kufunga mtambo wa tovuti yake.

Pia kinakusudia kuanzisha Idara mpya za masomo ya Lugha na Kompyuta.

CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Chuo Kikuu cha Zanzibar kilikuwa na wanafunzi 1,842, kati yao wanawake 869 na wanaume 973. Wanafunzi hao wanasoma fani ya Sheria, Biashara, Uongozi wa Umma, Uchumi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Jadweli Namba 28 inatoa ufafanuzi zaidi. Pia, katika mahafali ya nane yaliyofanyika tarehe 9 Januari 2011 ambapo Rais za Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein alikuwa mgeni rasmi, wanachuo 467 walihitimu masomo yao wakiwemo wanawake 216 na wanaume 251.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukabiliana na uhaba wa wahadhiri, chuo kimeajiri wahadhiri watatu na kufanya jumla ya wahadhiri wa kudumu kufikia 36 wakiwemo wanaume 28 na wanawake 08. Pia, Chuo kimewapeleka masomoni wahadhiri wakitanzania 03 kwa mafunzo ya shahada ya uzamivu kwa lengo la kupunguza kutegemea wahadhiri kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Chuo kinakusudia kujiimarisha zaidi kitaaluma na kimajengo. Chuo kitaanzisha masomo ya "*Project Planning and Execution" na "Procurement and Logistics Management*" katika kiwango cha stashahada. Chuo pia kinatarajia kuanzisha shahada za masomo ya uhandisi katika fani za mawasiliano *(Telecommunication Engineering)* na Kompyuta *(Computer Engineering)*

TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA YA KARUME

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume ni chombo kinachojitegemea kinachotoa mafunzo ya stashahada katika fani za ufundi na teknolojia. Taasisi inakusudia hapo baadae kutoa stashahada ya juu na shahada katika fani za ufundi na teknolojia.

Pia, Taasisi hii kwa kupitia Baraza lake linajukumu la kupanga malengo ya muda mfupi na muda mrefu yatakayoiwezesha Taasisi kujiendesha wenyewe mbali ya kupata ruzuku kutoka Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Taasisi limekutana katika vikao vinne tokea lilipoanzishwa. Katika vikao hivyo jumla ya ajenda arobaini na moja zilijadiliwa na maagizo thelathini na moja yalitolewa na kutekelezwa. Miswada, kanuni na taratibu za uendeshaji iliwasilishwa na kupitishwa na Baraza ni pamoja na kanuni za mitihani na yanayohusiana nayo, uteuzi wa

viongozi waandamizi na wakuu wa Idara, muundo wa utumishi kwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, mpango kazi wa miaka mitatu (2010-2013), kanuni za fedha, kanuni za uzalishaji mali na kanuni za uanzishwaji wa Serikali ya Wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka 2010/2011, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume imeweza kutekeleza kwa kiasi kikubwa malengo iliyojiwekea kama hivi ifuatavyo:

i. Kushajiisha na kuwatafutia ufadhili wanafunzi wa kike 40 kwa masomo ya awali ya Diploma.
ii. Kufanya manunuzi ya vikalio 105 kwa mashirikiano na *KOICA.*
iii. Kutengeneza vikalio 80.
iv. Kukamilisha matengenezo ya chumba cha kompyuta 25 na vifaa vya kufundishia kwa mashirikiano na Taasisi na *KOICA.*
v. Kupeleka masomoni wakufunzi watatu kuchukua shahada za juu kila mwaka na hivyo kufanya walimu waliopo masomoni kufikia 13.
vi. Kupindukia lengo la kusajili wanafunzi 100 kwa mwaka wa masomo.
vii. Kukamilisha utengenezaji wa dakhalia ya wasichana.
viii. Kuimarisha njia za ndani kwa kuweka vidaraja ili kurudisha haiba ya Taasisi.
ix. Kukamilisha kutengeneza kanuni ndogo ndogo za mitihani, fedha, wafanyakazi na uanzishwaji wa Serikali ya wanafunzi.
x. Kukamilisha mpango wa kazi wa miaka mitatu 2010 – 2013.
xi. Kukamilisha muundo wa utumishi wa walimu na wafanyakazi wa Taasisi.
xii. Kuweka mpango madhubuti wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Taasisi.
xiii. Kujenga mashirikiano mazuri na Taasisi nyengine ndani na nje ya nchi.
xiv. Kupitia mfuko wa maendeleo ya elimu ya ufundi, Taasisi imeweza kufanyia matengenezo makubwa ya vyoo, makaro yaliyobomoka, jengo la madarasa na kuweka uzio kuzunguka eneo la Taasisi.

Wafanyakazi na Wanafunzi

Mhe. Mwenyekiti, Hadi kufikia mwezi Juni 2011, Taasisi ilikuwa na wafanyakazi 71 wakiwemo walimu 51 (wanawake 20) na wafanyakazi wasiokuwa walimu 19 (wanawake 2). Wakufunzi 7 na wafanyakazi wengine 3 wamerejea kutoka masomoni. Wakufunzi waliopo masomoni kwa shahada ya pili ni 5 tu. Kurejea kutoka masomoni kwa wakufunzi hao kutasaidia sana katika kuimarisha ufanisi wa kazi katika Taasisi. Taasisi ina jumla ya wanafunzi 185 wa mafunzo ya ufundi ngazi ya stashahada kati yao, wanaume ni 149 na wanawake 36. Pia, Taasisi inaendesha mafunzo ya kujiendeleza ya ufundi stadi katika fani mbalimbali za ufundi. Jumla ya wanafunzi 474 wakiwemo 55 wanawake na 419 wanaume wanahudhuria mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka 2011/2012, Taasisi inakusudia kuendelea kutekeleza malengo mbali mbali ambayo yako katika mpango wake wa miaka mitatu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Taasisi hii imetengewa ruzuku ya Tsh. 720,000,000/- kwa kazi za kawaida.

MFUKO WA ELIMU YA JUU

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Elimu ya Juu unajukumu la kuwapatia mikopo wanafunzi wa Zanzibar wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu. Kwa mwaka 2010/2011, mfuko ulitengewa jumla ya Tshs 2,500,000,000/- kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi walioomba nafasi za elimu ya juu. Jumla ya wanafunzi 1,025 waliwasilisha maombi ya mikopo kwa ajili ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu. Hata hivyo, fedha zilizotengwa zilikuwa ni chache mno kutosheleza mahitaji ya wanafunzi wanaoendelea na wanafunzi wapya. Hivyo mfuko uliweza kuwadhamini wanafunzi wapya 653 tu. Kwa sasa tunao jumla ya wanafunzi 1,022, kati yao wanaume ni 488 na wanawake 534 katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi. Jadweli Namba (25 a – b) inatoa ufafanuzi zaidi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, fedha zote zilizokadiriwa Tsh. 2,500,000,000/- zilipatikana na kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, Kufuatia kupitishwa na Baraza lako tukufu sheria mpya ya uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar ambayo inafuta sheria iliyoanzisha mfuko wa elimu ya juu, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu itaanza kufanya kazi zake rasmi mara tu taratibu za sheria hio zitakapokamilika. Bodi itakapoundwa itaandaa kanuni zitazoelekeza uendeshaji wa mikopo ya wanafunzi. Kwa mwaka 2011/2012 jumla ya wanafunzi wapya 250 wanatarajiwa kudhaminiwa na Bodi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Mfuko umetengewa ruzuku ya Tsh. 4,000,000,000/- kwa kazi za kawaida.

BODI YA UPIMAJI NA TATHMINI

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Upimaji na Tathmini katika Elimu ilianzishwa rasmi katika mwaka 2011 kufuatia muundo mpya wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Bodi ina majukumu ya kusimamia shughuli zote zinazohusu mitihani ya SMZ ikiwemo utungaji, uchapishaji, usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya darasa la saba, kidato cha pili na mafunzo ya Ualimu (Diploma ya msingi na Diploma ya Dini na Kiarabu). Pia Bodi inajukumu la kutathmini mwenendo na matokeo ya mitihani hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/11, Bodi ilisimamia mwenendo mzima wa ufanyaji wa mitihani ya SMZ ambapo jumla ya skuli za msingi 219 *(139 Unguja, 80 Pemba)* ziliweza kufanya mitihani ya darasa la saba na skuli 178 (107 Unguja, 71 Pemba) zilifanya mitihani ya kidato cha pili. Jumla ya wanafunzi 23,269 walifanya mtihani wa darasa la saba katika mwezi Novemba 2010, kati yao wanafunzi 18,908 walifaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza ikiwa ni sawa na asilimia 81.2 ikilinganishwa na asilimia 84.8 ya wanafunzi waliofaulu mtihani huo mwaka 2009.

Kwa upande wa mtihani wa kidato cha pili kati ya wanafunzi 19,855 waliofanya mtihani, wanafunzi 11,562 ikiwa ni sawa na asilimia 58.2 walifaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha tatu katika skuli mbali mbali. Matokeo haya ni mazuri yakilinganishwa na ya mwaka 2009 ambapo asilimia 54.2 ya wanafunzi waliofaulu mtihani huo. Jadweli Namba 31 na 32 zinatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mitihani ya Taifa wa kidato cha nne, kati ya wanafunzi 17,055 wa skuli za serikali na binafsi waliofanya mtihani huo mwezi wa Oktoba 2010, wanafunzi 12,227 wamefaulu ikiwa ni sawa na asilimia 71.7. Aidha, kati ya wanafunzi waliofaulu 2,387 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika skuli za serikali mwaka 2011/2012, wakiwemo wanafunzi 1,868 kutoka skuli za Serikali, 118 wa skuli za binafsi na 401 wanafunzi wa faragha. Jadweli Namba 33 (a) na (b) zinatoa uchambuzi zaidi. Maelezo zaidi juu ya bodi ya upimaji na tathmini katika elimi yanapatikana ukurasa wa 58 na 59.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya wanafunzi 1,959 waliofanya mtihani wa Kidato cha Sita mwezi Februari, 2011 wanafunzi 1,517 sawa na asilimia 77.4 walifaulu. Kiwango hiki cha ufaulu kimeshuka ikilinganishwa na matokeo ya 2010 ambapo asilimia ya ufaulu ilifikia 84.1. Jadweli Namba 34 inatoa uchambuzi zaidi

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mitihani ya Ualimu, kati ya wanafunzi 239 waliofanya mtihani wa stashahada ya Ualimu (sekondari) katika Chuo cha Kiislam Mazizini na Chuo cha Kiislam Kiuyu Micheweni, wanafunzi 38 sawa na asilimia 15.9 walifaulu na wanafunzi 119 wamerudia mitihani yao. Aidha, kati ya wanafunzi 815 waliofanya mtihani wa stashahada ya Ualimu Msingi katika Chuo cha Kiislam Mazizini na Benjamin William Mkapa wanafunzi 291 sawa na asilimia 35.7 wamefaulu na wanafunzi 399 wamerudia mitihani yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Bodi imekusudia kuimarisha taratibu za usimamizi wa mitihani ya SMZ, ikiwemo kuendelea kuweka kumbukumbu zote za wanaotarajiwa kufanya mtihani katika mfumo wa kompyuta na kuongeza udhibiti wa mitihani hiyo. Pia, Bodi itaandaa sheria ya uanzishwaji wake, na kutayarisha kanuni na miongozo mbali mbali ya uendeshaji wa mitihani kwa mujibu wa sheria mpya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Bodi imetengewa ruzuku ya Tsh. 1,382,000,000/- kwa kazi za kawaida.

BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Huduma za Maktaba ni Shirika la huduma linalotekeleza shughuli zake kupitia Idara ya Huduma za Maktaba. Bodi imepewa jukumu la kutoa na kuendeleza huduma za maktaba visiwani Unguja na Pemba. Kazi kubwa ya Bodi ya Huduma za Maktaba ni kuhakikisha kwamba huduma za maktaba zinawafika walengwa ambao ni wananchi wa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Shirika limeendelea kupokea msaada wa vitabu kutoka "*Book Aid International*" ya Uingereza. Jumla ya vitabu 7,116 vya masomo mbali mbali vikiwemo vitabu vya "*fiction* and *literature*, "*non fiction*", vitabu vya rejea, vitabu vya watoto, vitabu vya kiada vya msingi, sekondari, elimu ya juu, masomo ya ualimu na madawa vimepokelewa. Vitabu hivyo vimegawiwa kwa skuli mbali mbali pamoja na taasisi za mafunzo ya juu vikiwemo vyuo vikuu vya hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia, Bodi ya Huduma za Makataba kwa ushirikiano na Shirika la "*Book Aid International*" limeanzisha mradi wa maktaba za masanduku katika skuli kumi za Wilaya ya Kaskazini 'A'. Skuli hizo ni Potoa, Bandamaji, Kilindi, Kigunda, Pale, Mkokotoni, Kidoti, Kigomani, Jongowe na Gamba. Baada ya kupatikana mafanikio katika skuli za awamu ya kwanza, Shirika la "*Book Aid International*" limeamua kuendeleza tena katika skuli nyengine kumi ili kuzipa fursa skuli hizo kufaidika na mradi huo.

Skuli zenyewe ni Kandwi, Kibuyuni, Kijini, Kinyasini, Chaani, Tumbatu, Mbuyu Tende, Pwani mchangani, Mfuru Matonga na Kikobweni. Wizara inalishukuru shirika la *Book Aid International* kwa misaada yake ya vitabu.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Huduma za Maktaba inaendelea kuwapatia wafanyakazi wake nafasi za kuongeza ujuzi na maarifa ya ukutubi. Wafanyakazi 02 wamepelekwa katika Chuo cha Ukutubi huko Tanzania Bara, mfanya kazi 01 amepelekwa katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ili kuongeza ujuzi na maarifa katika fani ya ukutubi.

Pia mfanyakazi 01 amepata fursa za kushiriki semina iliyotayarishwa na *Consortium of Tanzania University Libraries and Research Libraries (cotum)* iliyofanyika Tanga na wafanyakazi 03 wameshiriki semina iliyotayarishwa na *Green Stone software Workshop* iliyofanyika Bagamoyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Shirika la Huduma za Maktaba litaandaa mafunzo ya awali ya ukutubi ambayo yatatolewa kwa kipindi cha muda wa miezi mitatu. Mafunzo haya yatatolewa katika jengo la Huduma za Maktaba Unguja. Kwa upande wa Pemba bado kitengo cha "*American Corner*" kilichopo katika jengo la Maktaba Kuu Chake-Chake kitaendelea kutoa huduma. Huduma ambazo huwakutanisha wananchi kujadili mambo ya maendeleo na kutumia fursa ziliopo kwa kujielimisha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Shirika hili limetengewa ruzuku ya Tsh. 237,000,000/- kwa kazi za kawaida.

BODI ZA ELIMU ZA MIKOA NA WILAYA

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya zilifanya vikao vyao vilivyopangwa. Bodi za Mikoa zilifanya vikao katika mwezi wa Mei 2011 ambavyo vilitathmini matokeo ya mitihani mbali mbali.

Ripoti za tathmini hizo zilitumiwa na Bodi za Elimu katika kufanya marekebisho ya dosari zilizoonekana katika Mikoa yao na pia katika kuwahamasisha wazazi na wanafunzi kuweka juhudi zaidi katika masomo. Katika mwaka 2011/2012, Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya zitaendelea kujadili mambo mbali mbali yanayohusu elimu na kutoa mchango wao katika kuimarisha huduma za elimu katika Mikoa na Wilaya.

BARAZA LA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Baraza la Elimu lilikutana mara mbili. Baraza lilifanya kikao chake mwezi wa Juni 2011 na lilijadili mapendekezo ya ada mpya ya leseni za walimu na usajili wa skuli binafsi. Baraza lilijadili maombi ya usajili wa skuli mpya na kuyafanyia maamuzi. Katika mwaka 2011/2012, Baraza la Elimu litaendelea na kazi zake kama kawaida na kuishauri Wizara ipasavyo kuhusiana na masuala mbali mbali ya maendeleo ya elimu.

KITENGO CHA UHASIBU

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Uhasibu ni kitengo kilichoanzishwa mwaka 2011. Kitengo hiki kimekuwa kikishughulikia fedha zote zinazopokelewa katika fungu la kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kitengo kimesimamia kikamilifu ulipaji wa mishahara ya walimu na wafanya kazi wengine, malipo ya wakandarasi mbali mbali. Pia kimesimamia ufungaji wa mahesabu ya serikali kwa mujibu wa sheria zilizopo. Kitengo kimekuwa na mashirikiano mazuri na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali katika matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika udhibiti wa matumizi ya fedha za umma. Katika mwaka 2011/2012, Kitengo kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Sweden (Sida) kinakusudia kumpata mshauri mwelekezi atakaesaidia katika kuimarisha utaratibu wa uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu ya serikali kwa kuimarisha matumizi ya teknohama.

KITENGO CHA HABARI, ELIMU NA UHUSIANO

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Habari, Elimu na Uhusiano, katika mwaka wa 2010/2011, kiliendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa mafanikio. Ushirikiano na nchi mbali mbali na mashirika ya Kimataifa yalikuzwa na kuimarishwa katika kipindi kilichopita. Wizara ilipata mialiko na kuweza kuhudhuria mikutano ya Kimataifa zikiwemo nchi za Brazil, Marekani, Oman, Saudi Arabia, Ufaransa, China, Togo na Uturuki. Miongoni mwa mashirika ya Taasisi za Kimataifa ni ADB, BADEA, UNDP, Chuo Kikuu cha "*South Carolina State University*", "*Qatar Foundation"*, USAID na Sida. Mikutano

na ziara tulizozifanya zimesaidia sana katika kuimarisha uhusiano wetu na washirika wa maendeleo. Pia wageni kutoka nchi mbali mbali na mashirika ya kimataifa walifika wizarani na kuonana na Mhe. Waziri na viongozi waandamizi wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka 2011/2012, kitengo kitaendelea kuongeza ufanisi zaidi katika kuendeleza mashirikiano ya karibu na Ofisi za Kibalozi ziliopo nchini pamoja na taasisi mbali mbali ya Kimataifa. Pia kitaendelea kuongeza ufanisi wa kazi kwa kujenga mawasiliano ya karibu zaidi na ofisi za Ubalozi na Mashirika mbali mbali ya kimataifa.

KITENGO CHA UNUNUZI NA UGAVI

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Ununuzi wa Ugavi ambacho ndicho Sekretariati ya Bodi ya zabuni ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kiliendelea kufanya kazi zake vizuri katika mwaka 2010/11. Kitengo kwa kushirikiana na Bodi ya Zabuni kilitayarisha, kutangaza na kuzifanyia tathmini jumla ya zabuni kumi na saba za manunuzi ya bidhaa, huduma za washauri na kazi za ujenzi zenye thamani ya jumla ya shillingi billioni nane, kumi na tisa millioni laki nane arubaini na mbili elfu, mia tatu na sita na senti saba (Tshs.8,019,842,307/7).

Miongoni mwa zabuni hizo, zabuni mbili ni za ujenzi wa Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa kilichopo Mchangamdogo Pemba na Ujenzi wa skuli ya Sekondari ya Shamiani Pemba; ukarabati wa skuli sita za sekondari Unguja na Pemba na kumalizia ujenzi ulioanzishwa na wananchi wa madarasa mia moja na ishirini ya skuli za msingi Unguja na Pemba. Aidha mikataba ya ujenzi wa skuli kumi na sita mpya za sekondari Unguja na Pemba na Ujenzi wa kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Mchanga Mdogo Pemba na ukarabati wa skuli za Utaani na Fidel Castro zimesainiwa na zinatekelezwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Kitengo kinakusudia kutiliana saini mikataba na wakandarasi wa skuli tatu za ghorofa katika Mkoa wa Mjini Magharibi na ukarabati wa skuli nne za sekondari za Unguja na Pemba. Pia Kitengo kimekusudia katika kipindi hicho hicho kutoa zabuni na kutiliana saini mikataba ya uchongaji wa madawati, kununua vifaa vya afisini na vifaa vya maabara kwa ajili ya skuli za sekondari kumi na tisa mpya zinazojengwa hivi sasa, skuli sita zitazofanyiwa ukarabati na Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa kilichopo Mchangamdogo Pemba.

Aidha, kitengo kinakusudia kutayarisha, kutangaza na kufanyia tathmini zabuni za ununuzi wa vifaa vya ukamilishaji wa ujenzi ulioanzishwa na wananchi wa madarasa mia mbili na uchongaji wa madawati 5,000 Unguja na Pemba: kutangaza na kufanyia tathmini ya ujenzi wa skuli mbili mpya za sekondari za Kibuteni Unguja na Mkanyageni Pemba na kutayarisha, kutangaza na kufanyia tathmini zabuni za ununuzi wa samani na vifaa vya Habari na Mawasiliano kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kampasi ya Tunguu.

KITENGO CHA UKAGUZI WA HESABU ZA NDANI

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani cha Wizara kina jukumu la kukagua hesabu za mapato na matumizi katika idara zote za wizara na skuli zote za serikali za Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2010/2011, kitengo kimeweza kukagua hesabu zote za ndani katika makao makuu ya wizara pamoja na kufuatilia vifaa vilivyopelekwa katika skuli mbali mbali ambavyo hununuliwa kutoka bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo ili kuangalia thamani halisi ya bidhaa zilizopelekwa na ujenzi uliofanyika. Kitengo pia kimeweza kukagua skuli 80 za maandalizi, msingi na sekondari. Aidha kitengo kimekagua taasisi za wizara zinazopokea ruzuku ambazo hujitegemea katika kutekeleza mipango yake. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Shirika la Huduma za Maktaba. Pia kitengo kimeweza kukagua vyuo vinavyopokea fedha za wanafunzi kutoka Mfuko wa Elimu ya Juu ikiwemo *Zanzibar University*. Kwa upande wa Tanzania Bara vyuo vilivyokaguliwa ni :-

- Kampala *Islamic University* –Tawi la DSM
- Chuo Kikuu Mzumbe – Morogoro
- Chuo cha Kilimo Sokoine – Morogoro
- Chuo Kikuu cha Kiislam – Morogoro
- Chuo Kikuu cha Dodoma – Dodoma
- Chuo cha Elimu ya Biashara – Dodoma
- Taasisi ya Mipango ya Maendeleo – Dodoma
- Chuo cha Uhasibu – Arusha
- Chuo cha Ushirika – Moshi
- Chuo cha Afya (KCMC) – Moshi
- Chuo Kikuu cha Dar - Es - Salaam
- Chuo cha Usimamizi wa Fedha – DSM.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 kitengo kimetekeleza mwongozo wa usimamizi wa fedha kwa walimu wakuu na washika fedha wa skuli za Unguja na Pemba ili kufanikisha usimamizi wa michango inayotolewa na

wazazi kwa maendeleo ya skuli. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, kitengo hiki kitaendelea kufanya ukaguzi wa mahesabu ya Idara zake, Taasisi na skuli mbali mbali za Unguja na Pemba.

KITENGO CHA URATIBU WA ELIMU YA JUU

Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki ni kipya na kimeundwa baada ya kufutwa kwa Idara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Kitengo hiki kina jukumu la kuratibu maendeleo ya elimu ya juu na kuwa na mashirikiano ya karibu na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania *(Tanzania Commission for Universities)*, vyuo vikuu mbali mbali vilivyoko Zanzibar na vilivyoko Tanzania bara. Katika kipindi hiki kitengo kilifuatilia mapendekezo ya Wizara ya kutaka Sheria iliyoanzisha TCU ifanyiwe marekebisho ili impe madaraka Rais wa Zanzibar katika kusimamia shughuli zote za Elimu ya Juu kwa upande wa Zanzibar. Katika mwaka 2011/2012, Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu kitaimarisha mahusiano yake na Taasisi za Elimu ya Juu za Zanzibar na Tanzania bara.

KITENGO CHA ELIMU MJUMUISHO NA STADI ZA MAISHA

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kimetokana na kuunganishwa kwa kitengo cha Elimu Mjumuisho, kitengo cha Ushauri Nasaha, seksheni ya UKIMWI na seksheni ya masuala ya jinsia na kufanya kitengo kimoja. Kitengo hiki kina majukumu ya kuwapatia haki ya elimu watoto wote wenye ulemavu, kutoa ushauri nasaha, kusaidia kutatua matatizo ya wanafunzi yanayowarejesha nyuma katika masomo yao, kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutoa elimu ya stadi za maisha kwa walimu na wanafunzi ili kujikinga na maambukizo ya UKIMWI na kuwahamasisha watoto wa kike kuhusu umuhimu wa elimu.

ELIMU MJUMUISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011, kitengo kimeendelea kuwaandalia mazingira rafiki ya kujifunza wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Wapo wanafunzi 4,300 wenye mahitaji maalum kati yao 2,254 ni wanaume, na 2,046 ni wanawake katika skuli 86 za Unguja na Pemba. Walimu wa skuli hizo 2,390 (808 wanaume, 158 wanawake) wamepatiwa mafunzo maalum ya kufundisha madarasa yenye wanafunzi wenye mahitaji mbali mbali ya kujifunza. Baadhi ya mafunzo waliopatiwa yalikuwa ni ya maandishi ya nukta nundu (*Braille*), lugha ya alama, upimaji wa wanafunzi, urekebishaji wa tabia za wanafunzi na namna ya kuzifanyia kazi changamoto mbali mbali zinazowakabili wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaendelea kupeleka walimu wa elimu mjumuisho katika Chuo cha Kiislamu, mazizini na vyuo vya Tanzania Bara na Uganda kwa ajili ya mafunzo mbali mbali ya ualimu wa elimu mjumuisho. Wapo walimu watatu wenye stashahada (1) na shahada ya kwanza (2) katika fani ya elimu mjumuisho na kupangiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo kimeweka utaratibu kila mwaka wa kuwapima wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza kwa madhumuni ya kuweza kugundua matatizo yanayowakabili katika kujifunza na kuyafanyia kazi mapema ili wanafunzi hao waweze kujifunza kwa ufanisi zaidi. Jumla ya wanafunzi 2,483 (wanaume 1122 na wanawake 1361) walipimwa na wanafunzi 1446 (626 wanaume, 800 wanawake) waligunduliwa na matatizo mbali mbali. Matatizo makubwa yaliyobainika yalikuwa ni pamoja na maradhi ya mifupa, pumu, kifafa, maradhi ya ngozi, ulemavu na kichocho. Wanafunzi wote walioonekana kuwa na matatizo walifikishwa Hospitalini kwa uchunguzi zaidi na hatimae kupatiwa vifaa kama vile miwani, shime sikio na wengine kutibiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Baadhi ya watendaji wa kitengo wameshiriki mikutano inayohusiana na watu wenye ulemavu na watu wenye mahitaji maalum iliyofanyika katika nchi mbali mbali zikiwemo Norway, Nigeria, Uganda na Tanzania Bara. Washiriki wa mikutano hiyo wameweza kubadilishana uzoefu na utendaji bora katika jitihada za kuwapatia elimu bora wanafunzi wenye ulemavu na mahitaji mengine ya kielimu.

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio tuliyoyapata katika utoaji wa Elimu Mjumuisho yameweza kuwavutia nbaadhi ya nchi jirani ambazo zimeleta wataalamu wao kuja kujifunza. Ujumbe wa watu 14 kutoka nchi ya Madagascar ukifuatiwa na ujumbe mwengine wa watu 6 kutoka nchi hiyo hiyo walifika Zanzibar. Pia, Kitengo kilipokea ugeni kutoka nchi ya Niger kwa dhamira hiyo hiyo ya kujifunza.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kimezidi kukuza ushirikiano na jumuiya kama vile jumuiya kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa akili (ZAPDD), Umoja wa Watu wenye Ulemavu Zanzibar (UWZ), Jumuiya ya wasioona (ZANAB), Chama cha Viziwi Zanzibar (CHAVIZA) na *"Zanzibar Outreach Programme (ZOP*)". Kwa upande wa CHAVIZA, tunaendelea na mpango wa kuandaa mazingira mazuri ya kielimu kwa wanafunzi viziwi. Kitengo kinakusudia, kuanzisha kamusi la lugha ya alama lenye istilahi za Kizanzibari. Vile vile walimu na watu wengine wamepatiwa mafunzo ya ukalimani wa lugha ya alama. Aidha, mafunzo yametolewa kwa walimu juu ya namna ya kuwafundisha kusema wanafunzi wenye matatizo ya kuongea.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, kitengo kimekusudia kuendeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendeleza mafunzo mbali mbali kwa walimu na watendaji kutoka taasisi nyengine.

ii. Kuendeleza uhamasishaji kwa wazazi na jamii ili watoto wenye mahitaji maalum wapelekwe skuli.

iii. Kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa elimu mjumuisho.

iv. Kuendeleza upimaji wa wanafunzi walioko skuli.

v. Kuendeleza ushirikiano baina ya taasisi mbali mbali za Kitaifa na za Kimataifa.

vi. Kuwajengea uwezo washauri wa elimu mjumuisho walioko katika vituo vya walimu ili waweze kusimamia na kuendeleza elimu mjumuisho katika skuli zilizo katika maeneo yao.

USHAURI NASAHA

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kwa kushirikiana na Jumuiya ya FAWE kimeweza kutoa mafunzo ya stadi za maisha kwa wanafunzi 455 wa skuli ya Kijini.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo hutoa ushauri nasaha kwa wazazi na wazee wa wanafunzi kwa madhumuni ya kusaidia katika kutatua baadhi ya matatizo ya wanafunzi. Katika jitihada za kupambana na unyanyasaji wa kijinsia na mimba za utotoni, Kitengo kwa kushirikiana na WEZA ilifanya mazungumzo na wazazi na walimu katika maeneo ya Mchangani, Chwaka, Ukongoroni na Kisauni.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Kitengo kitaendelea na juhudi zake za kupambana na mimba za utotoni, ndoa za mapema na madawa ya kulevya. Pia kitaendelea na kuelimisha stadi za maisha kwa walimu, wazee na wanafunzi katika skuli zote za Unguja na Pemba.

MASUALA YA JINSIA

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Kitengo kiliendeleza kampeni juu ya umuhimu wa elimu kwa wanawake na watoto wa kike. Kampeni hizo

zilifanywa Kitaifa kwa Unguja na Pemba katika maadhimisho ya Juma la Elimu kwa Wote tarehe 2 mpaka tarehe 8 Mei, 2011 na kudhaminiwa na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNICEF na UNESCO. Shughuli mbalimbali za kitaaluma zilitayarishwa zikiwemo;

- Uchapishaji wa mabango yenye ujumbe wa elimu kwa wote "Elimu kwa Mtoto wa Kike na Wanawake ni haki na tuifanye kuwa ni haki"

- Midahalo ya mjadala ya wanafunzi juu ya masuala muhimu ya elimu kwa wote Zanzibar.

- Makongamano kwa kinamama (wanawake wanakisomo) na kuzawadia wanakisomo waliofanya vizuri.\

- Chemsha bongo za masuala ya sayansi na taaluma kwa ujumla kwa wanafunzi wa sekondari za Unguja na Pemba.

- Uandaaji na urushaji wa vipindi vya Radio na Televisheni kuhusu elimu kwa mtoto wa kike na elimu kwa wote Zanzibar kwa lengo la kufikisha ujumbe wa elimu kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, wizara kwa kushirikiana na UNESCO imetengeneza miongozo juu ya utoaji wa elimu ya afya ya uzazi, UKIMWI pamoja na stadi za maisha kwa wanafunzi, walimu, wakufunzi na wafanyakazi wengine Unguja na Pemba. Lengo la muongozo huo ni kuongoza watendaji katika uratibu, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za utoaji wa elimu ya afya ya uzazi, UKIMWI na stadi za maisha

Mhe. Mwenyekiti**,** Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Ukimwi imetengeneza mwongozo unaoelekeza utoaji wa elimu ya afya ya uzazi, UKIMWI na stadi za maisha kwa ajili ya wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu Zanzibar. Mafunzo ya kutumia mwongozo huo yametolewa kwa wakufunzi 45 wa Chuo cha Kiislamu Mazizini Unguja, pamoja na wakufunzi 38 kutoka katika Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa na Chuo cha Kiislamu cha Kiuyu Pemba. Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha wakufunzi kuwa na mbinu bora za kufundishia pamoja na elimu kamili itakayowawezesha kujikinga na UKIMWI pamoja na kuwasomesha walimu na juu ya kupambana na janga la UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara inakusudia kuweka mikakati madhubuti ya kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU). Mafunzo ya stadi za maisha ya kujikinga na

UKIMWI yatatolewa kwa walimu, kuimarisha klabu za afya maskulini na kusambaza vipeperushi kwa ajili ya kuelimisha wanafunzi pamoja na walimu wao juu ya kujikinga na UKIMWI.

KITENGO CHA URAJIS

SHERIA YA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, katika kuitekeleza Sera Mpya ya Elimu ya mwaka 2006, Kitengo kimeandaa rasimu ya sheria mpya ya elimu. Pia rasimu ya sheria ya uanzishwaji wa Taasisi ya Elimu ya Zanzibar imeandaliwa. Katika mwaka 2011/2012, Kitengo kitakamilisha rasimu ya sheria hizi na kuandaa rasimu ya Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu na Bodi ya Upimaji na Tathmini.

KESI ZA ARDHI ZA SKULI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011, Kitengo cha Urajis wa Elimu imeshughulikia kesi tatu ambazo zinahusiana na uvamizi wa maeneo ya ardhi ya skuli. Kesi hizo zinahusiana na Skuli ya Kizimkazi Mkunguni, Skuli ya Welezo na Skuli ya Potoa. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya mwanasheria Mkuu inafuatilia mwenendo wa kesi hizo.

LESENI ZA WALIMU

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo kiliendelea na juhudi zake za kutoa leseni kwa walimu wa skuli za serikali na za binafsi. Jumla ya walimu 812 walipatiwa leseni za kusomeshea kati yao walimu hao 664 walisomea na 208 wasiosomea. Pia, Maafisa wa Kitengo walitembelea skuli za serikali na binafsi kukagua kama walimu wote wanazo leseni za kusomeshea.

Vile vile wakaguzi wa elimu wakati walipofanya ukaguzi wa elimu katika maskuli, walikagua leseni za walimu. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Mrajis wa Elimu itaendelea kushughulikia maombi ya leseni za walimu kutoka skuli za serikali na binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilipokea maombi 22 ya usajili wa skuli za Serikali na skuli 43 za binafsi. Skuli zote 22 za serikali zilipata usajili na skuli 18 za binafsi pia zilipewa usajili baada ya kufanyiwa ukaguzi. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Mrajis wa Elimu itaendelea kushughulikia maombi ya usajili wa skuli za serikali na binafsi.

KESI ZA UJAUZITO NA NDOA ZA WANAFUNZI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, kesi 28 za ujauzito wa wanafunzi ziliripotiwa, ambapo kesi tatu zilikuwa za wanafunzi kwa wanafunzi. Kesi 10 kati ya hizo zilijadiliwa katika ofisi ya mrajis wa elimu na wanafunzi 8 walikubali kuendelea na masomo, wawili walikataa kuendelea na wanafunzi 18 hawakuhudhuria katika kikao cha majadiliano.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki kesi 22 za ndoa za wanafunzi ziliripotiwa, na kati ya kesi hizo kesi mbili zilikuwa baina ya wanafunzi kwa wanafunzi. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 6 ya mwaka 1982 kifungu cha 20 (3) wanafunzi 22 wa kike na wanafunzi wawili wa kiume walifukuzwa skuli. Hivyo jumla ya wanafunzi 24 walifukuzwa skuli. Katika mwaka 2011/2012, Kitengo cha Urajis kitaendelea kushughulikia kesi za ujauzito na ndoa za wanafunzi. Na Ishallah Mungu ajaalie zisitokee.

KITENGO CHA MICHEZO NA UTAMADUNI

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka 2010/2011, kitengo cha Michezo na Utamaduni kimeendelea kufanya juhudi kubwa zaidi katika kuimarisha fani mbalimbali za michezo. Kitengo kimetoa mafunzo mbalimbali ya michezo kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazojishughulisha na michezo hapa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Kamati ya Olimpiki ya Tanzania ambayo iliwapatia walimu 30 mafunzo yaliyohusu Maadili ya Olimpiki (*Olympic Values*). Mafunzo hayo yatawasaidia walimu wetu kupata taaluma ya kuwasaidia kuhamasisha vijana na wanafunzi kutekeleza baadhi ya malengo ya millennia yaliyowekwa kupitia michezo. Aidha yatasaidia kuwajengea ufahamu walimu na wanafunzi wetu juu ya dhana pana ya michezo.

Mhe. Mwenyekiti, Mnamo mwezi wa Juni 2011, timu zetu za elimu zilishiriki katika mashindano ya UMISSETA yaliyofanyika Kibaha Tanzania Bara. Katika mashindano hayo, timu za mpira wa mikono na mpira wa meza (Wanaume) zimepata ushindi wa kwanza; timu za mpira wa wavu na mpira wa meza (Wanawake) zimepata ushindi wa pili; na timu ya riadha (Wanaume) zimepta ushindi wa tatu. Katika Mashindano haya kanda ya Zanzibar imeshika nafasi ya tatu kati ya kanda kumi na mbili zilizoshiriki. Pia mwanafunzi Moh'd Ali wa Skuli ya Sekondari ya Nyerere amechaguliwa kuwa mlinda mlango bora wa mchezo wa mpira wa miguu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, Kitengo kitaendelea kuwapatia taaluma ya michezo walimu wa fani mbalimbali za michezo katika skuli zetu za Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yanatarajiwa kutolewa kwa mashirikiano kati ya kitengo na wataalamu wengine wa michezo kutoka ndani na nje ya nchi yetu kadiri hali ya kifedha itakavyoruhusu.

Aidha kwa kushirikiana na taasisi nyengine za elimu Zanzibar kitengo kimedhamiria kutoa mafunzo kwa walimu wa skuli za msingi juu ya muhutasari wa somo la michezo uliondaliwa na Wizara mwaka 2009. Mafunzo hayo yataendeshwa kwa mashirikiano na mtaalamu kutoka Japan ambaye yupo hapa kwa kipindi cha miaka miwili. Vile vile, kwa kushirikiana na Kamati ya Olimpiki ya Tanzania na "*British Council"* kitengo kimedhamiria kuendesha mafunzo ya michezo mbali mbali katika maeneo ya Dole Wilaya ya Magharibi Unguja. Mradi huu uko katika hatua ya majaribio.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kitaendelea na utaratibu wake wa kufanya tathmini ya kila mwaka ya michezo kupitia sherehe za Tamasha la Elimu bila Malipo kuanzia ngazi ya skuli, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Pia kitaendelea kushiriki na katika mashindano ya michezo itakayoandaliwa na Shirikisho la FEASSSA kwa Afrika Mashariki yanayofanyika kila mwaka katika mwezi wa Agosti kwa lengo la kuendelea kuibua, kuinua, kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana wetu na kuitangaza Zanzibar kupitia midani za michezo nje ya mipaka yake.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kitaendelea na kutoa mafunzo kwa vijana yanayohusiana na UKIMWI na Madawa ya Kulevya kupitia michezo ili kusaidia kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI kwa vijana na kuwafanya vijana wawe karibu zaidi katika shughuli za michezo badala ya kujiingiza katika anasa na starehe zitakazowapelekea kupata magonjwa ya zinaa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha hotuba hii hata nikaweza kuiwasilisha Barazani leo hii. Shukrani maalum zimwendee Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa michango yake mbali mbali pamoja na mashirikiano mazuri katika kuiendesha Wizara yetu. Halikadhalika napenda kumshukuru Katibu Mkuu kwa kusimamia vizuri kazi zote za kitaalamu na kiutendaji pamoja na udhibiti wa fedha za Serikali. Aidha namshukuru Naibu Katibu Mkuu na Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi na watendaji wote waliosalia. Pia nawashukuru wenyeviti wote wa Mabaraza na Bodi mbali mbali kwa miongozo na ushauri wao wenye manufaa.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani zangu za dhati ziwaendee walimu, wafanyakazi wengine wa Wizara, wanafunzi wa ngazi zote za Elimu, wazazi pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa juhudi zao katika kusukuma mbele maendeleo ya Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru viongozi wote wa Mikoa, Wilaya na Majimbo kwa msaada na mashirikiano wanayoendelea kunipa. Pia naishukuru Wizara ya Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ushirikiano mkubwa inayotupa kila tunapoikabili kwa matatizo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Napenda kuchukua nafasi ya pekee kushukuru nchi wahisani na mashirika ya misaada ya kimataifa kwa kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza elimu nchini. Shukurani za pekee nazitoa kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa china, Serikali ya Oman, Serikali ya India, Shirika la Misaada la Sweden (*SIDA*), Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Misaada ya Maendeleo (*USAID*), Shirika la Umoja wa Mataifa ya Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*), Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

Pia napenda kuyashukuru mashirika yasio ya kiserikali yanayoshirikiana na sisi kwa misaada yao kwetu. Mashirika hayo ni ZAYADESA, FAWE, *Save the Children Funds* na *Emirate Foundation.* Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Mbunge wa jimbo la Kitope kwa msaada wa madawati na hivyo kuondosha kabisa tatizo la vikalio vya wanafunzi kwa skuli za Jimbo Lake.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa uvumilivu na utulivu. Aidha natanguliza shukrani zangu kwao kwa michango yao watakayoitoa katika kujadili hotuba hii, ambayo natarajia itakuwa na msaada mkubwa kwangu na kwa Wizara yangu. Napenda niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuwa nitatoa mashirikiano kwa hali zote katika majimbo yote ya Unguja na Pemba na kuhakikisha kuwa ufanisi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali unaongezeka.

MAPATO

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya Tsh. 10,000,000/- kutoka vianzio vya Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale na Ada za leseni za walimu pamoja na uandikishaji wa skuli za binafsi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, Tsh.

10,151,000/- zilikusanywa na kuwasilishwa ikiwa sawa na asilimia 102 ya makadirio. Kati ya fedha hizo Tsh. 1,286,400/- zilitokana na vianzio kutoka Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale na Tsh. 8,864,600/- zilitokana na ada za leseni za walimu na uandikishaji wa skuli binafsi.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakusudia kukusanya jumla ya Tsh. 15,000,000/- na kuziwasilisha hazina. Jadweli Namba 49 inatoa ufafanuzi zaidi.

JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kwa unyenyekevu liidhinishe matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya jumla ya Tsh. 101,099,854,000/-. Kiasi hicho kinajumuisha Tsh. 43,789,008,000,000/- kwa ajili ya kazi za kawaida na Tsh. 57, 310,054,000/- kwa kazi za maendeleo. Fedha za maendeleo zinajumuisha Tsh. 4,500,000,000/- fedha za ndani na Tsh. 52,810,054,000/- fedha kutoka kwa wahisani. Jadweli namba 46 na 47 zinatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii maalum kumpongeza kwa dhati Mzee wetu Mzee Ali Mzee kwa kuteuliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Tunategemea sana msaada wake hata uliosababisha sisi tumwite profesa kwa hivyo ataendelea na uprofesa wake na Ishallah tutashirikiana naye kwa dhati kabisa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunijaalia jioni ya leo kunipa pumzi ya kuweza kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binasfsi kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wa Kamati yangu juu ya Makadirio ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Pili Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kuniamini na kunipa jukumu hili la kuwa Mwenyekiti wa Kamati yao na pia kupata nafasi ya kuwasilisha maoni yao.

Mhe. Spika, napenda kuwatambua kwa kuwataja Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Amina Iddi Mabruok	Mwenyekiti
2.	Mhe Hija Hassan Hija	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Asha Abu Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Ashura Ali Sharifu	Mjumbe
5.	Mhe. Jaku Hashim Ayubu	Mjumbe
6.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
7.	Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
8.	Mhe. Saleh Nassor Juma	Mjumbe
9.	Ndg. Shemsa Maabad Mohamed	Katibu
10.	Ndg. Talib Enzi Talib	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuiweka Sekta ya Elimu kuwa moja ya vipaumbele vinne vya Taifa katika bajeti ya Mwaka huu. Hii inaonyesha jinsi gani serikali inavyofanya kazi kwa umakini, kuhakikisha kuwa wananchi wake na vijana wanaelimika na kupata fursa za kuweza kushindana na vijana wengine katika Mataifa mengine.

Mhe. Mwenyekiti, ubora wa taifa lolote duniani, linajengeka kwa elimu wanayoipata wananchi wake. Hivyo na sisi hatuna budi pamoja na umasikini wetu kuwekeza katika Elimu, kwani ndio njia pekee itakayotuwezesha kufika kule ambako tunaota kufika.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo tunaishauri Serikali kuona kuwa kuna haja kubwa ya kuwekeza rasilimali za kutosha katika Elimu. Kimataifa inapendekezwa kutumia asilimia 20 ya bajeti kwa ajili ya elimu.

Hapa kwetu bajeti ya elimu haijawahi hata mara moja kufikia asilimia hiyo. Hivyo ni vyema tukaanza kuchukuwa hatua ya kuipandisha bajeti yetu ya Elimu ili ifikie asilimia 20 kama viwango vya kimataifa vinavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuongeza ubora wa Elimu limesisitizwa pia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar aliyoitioa alipokuwa akilizindua Baraza hili, kuwa Serikali ya awamu ya saba ya Muundo wa Umoja wa Kitaifa itahakikisha kuwa elimu ya nchi yetu inapanda.

Azma hiyo ndani ya Bajeti ya mwaka mpya wa fedha 2011/2012 bado haijatekelezeka.

Elimu ya Maandalizi
Elimu ya maandalizi ni sehemu ya Elimu ya lazima kwa kila Mtoto wa Zanzibar, ni jambo la faraja kuona kuwa idadi ya Skuli za Maandalizi zinaongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo tunaishauri wizara kuzifanyia ukaguzi Skuli hizo na kuzitolea miongozo ya njia bora za kuwafundisha watoto hao. Hivi sasa skuli nyingi za maandalizi zimeonekana kuweka mkazo kwa watoto wa skuli hizo kujua kusoma na kuandika hali ya kuwa kutokana na umri wao bado hawakutakiwa kufunzwa mambo yao. Tunavyofahamu ni kwamba katika miaka miwili ya mwanzo kwa wanafunzi wa Skuli za maandalizi hutakiwa wapate muda wa kucheza zaidi na kufunzwa baadhi ya tabia zetu nzuri zinazoendana na utamaduni wetu wa Zanzibar ikiwemo kujifunza dua, maamkizi n.k.ili waweze kukua katika misingi ya maadili mema ya maisha.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na maelezo ya ndani ya kitabu chake Mheshimwa Waziri ni skuli 29 za Maandalizi ni za Serikali na Skuli 215 za maandalizi ni za watu binafsi hali ambayo inaonyesha kuwa idadi ya kubwa ya watoto wa Kinzanzibar wapo katika Skuli za binafsi. Tunaiagiza Wizara ya Elimu kuhakikisha kuwa Skuli zote za Maandalizi hasa zile za binafsi zinafanyiwa ukaguzi wa kina ili kuweza kufahamu maendeleo ya skuli hizo. Aidha, utaratibu huo utasaidia kuweza kufahamu mbinu zinazotumiwa iwapo zinafaa na zinakubalika kulingana na utaratibu wa kutoa mafunzo hayo.

Kamati yangu pia inaishauri wizara kutoa mkazo maalum wa kuwafundisha walimu wa maandalizi kuanzia ngazi ya cheti, diploma hadi shahada hasa ukizingatia kuwa Elimu ya Maandalizi hivi hasa imegeuzwa kuwa ni Elimu ya Lazima.

Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani
Mhe. Mwenyekiti, hapa Zanzibar ilitangazwa kuwa elimu itatolewa bure tangu mwaka 1964. Lakini kwa kipindi kirefu sasa wazazi wamekuwa wakitoa michango kwa maendeleo ya skuli. Wanafunzi wa ngazi zote kuanzia Skuli za Msingi, Sekondari hadi vyuoni. Kamati yangu imeridhishwa na utaratibu uliowekwa katika kitabu cha bajeti cha mwaka huu wa fedha kuwa kitengo kimetayarisha muongozo wa usimamizi wa fedha kwa Walimu Wakuu na washika fedha.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo basi katika kuitekeleza azma hii nzuri tunaiagiza wizara kuhakikisha kuwa fedha zote za michango inayotolewa na wazazi kwa maendeleo ya skuli ziainishwe katika kitabu cha bajeti mwakani ikiwa ni sehemu ya mapato yatakayokusanywa na wizara hii. Aidha, wale wote watakochangia kuandaliwa utaratibu maalum wa kuwapatia risiti. Katika

kuweka kumbukumbu hizo sawa vitabu vyote vya risiti vikaguliwa na wakaguzi wa ndani na pia wakaguzi wanaotoka katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

ChuoKikuu cha Taifa SUZA

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Taifa hapa Zanzibar ni mwanzo mzuri na mafanikio yake yameonekana. Kwanza kwa kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi mwaka hadi mwaka, lengo la Serikali limeingia kasoro kubwa kwa kupangiwa fedha kidogo sana katika bajeti ya mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kimepangiwa bajeti ambayo kutokana na mahitaji ya chuo haikidhi haja hata kidogo ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi katika chuo hicho. Tunaishauri Serikali isifanye mzaha, ikiangalie chuo hicho kwani kwa tathimini ya kamati yetu na hali halisi ilivyo ni kuwa chuo hicho kitashindwa hata kuwaleta Maprofesa kutoka nje ya nchi kuja kuwafundisha wanafunzi wetu katika chuo hicho .Tunaiomba Serikali katika kukisaidia chuo hicho ili lengo la kuwaleta walimu kutoka nje ya nchi liweze kufanikiwa na kupatikana kwa ufanisi na maendeleo ya chuo hicho.

Ofisi ya Ukaguzi wa Elimu

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza uwamuzi uliofanywa na wizara kwa kuifanya Idara ya Ukaguzi kuwa ni Ofisi ya Ukaguzi ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, ofisi hiyo bado ikabiliwa na changamoto kubwa kwani idadi ya shule zilizokaguliwa ni kidogo sana na pia idadi hiyo haikuingiza skuli za maadalizi hasa zile za binafsi. Hivyo tunaiomba wizara kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa idadi ya skuli zilizofanyiwa ukagazi wa aina mbali mbali inaongezeka katika mwaka huu wa fedha. Aidha, ofisi inongezewe uwezo na nyezo ili iweze kufanya kazi zake kwa ubora na ufanisi zaidi.

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyokumbuka hivi karibuni tulipitisha Mswada wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwa taarifa, sheria hii tayari Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameshaitia saini hivyo itawawezesha wizara kupata fursa ya mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu waliopo nje na ndani ya nchi .Ushauri wetu ni kuwa wizara ijitahidi kufanya haraka kutengeneza kanuni ili vijana wetu waweze kupata mikopo kwa wakati. Aidha, tunaiomba wizara kuhakisha kuwa wale wote waliokopeshwa awali kabla ya kuanzishwa kwa sheria hii mpya, kuandaliwa utaratibu mzuri wa kuweza kurudisha fedha hizo kwa vile tayari wameshamaliza mikopo hiyo na wengine wameshapata ajira. Hivyo, ni vyema

kuharakisha kuzikusanya fedha hizo ili kuongezea mfuko huo wa fedha wa Bodi ya Mikopo.

Sayansi na Teknolojia
Mhe. Mwenyekiti, tunapongeza juhudi zilizochuliwa na Serikali kwa kuwashajiisha wanafunzi wa kike kupenda masomo ya Sayansi na Hesabati ambapo kambi mbali mbali zimeanzishwa kwa ajili ya wanafunzi hao. Tunaishauri wizara kufanya juhudi za kuwahamasisha wanafunzi wa kike kwa kuanza katika ngazi za chini kabisa hasa katika Elimu ya Msingi kwa kuwa na vivutio na motisha hizo ili wakifia katika ngazi ya Elimu ya Sekondari .

Changamoto kwa Serikali katika Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kuhakikisha kuwa fedha ambazo zitaidhinishwa na Baraza hili kwa ajili ya Bajeti ya Wizara ya Elimu katika mwaka huu wa fedha zinapatikana zote kwa asilimia mia moja. Kutopatikana kwa fedha hizo sio tu ni kikwazo kwa maendeleo ya elimu, bali pia ni jambo lisilokubalika kuwa Baraza tumepitisha maamuzi ya kiasi cha fedha na utekelezaji wake ukawa vyenginevyo

Mhe. Mwenyekiti, moja ya kasoro ya bajeti hii ni kuwa ushirikishwaji wa wadau wengine wa elimu ulikuwa mdogo sana. Hii ilipelekea hata upangaji wa vipaumbele vya bajeti kuwa na mapungufu. Mfano, wakati katika hotuba yake Rais wa Zanzibar katika ufunguzi wa Baraza aliahidi mafunzo zaidi kwa walimu na nyumba zaidi kwa walimu bajeti hii haikuweka wazi kuhusu ujenzi wa nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine ambayo kamati yangu inahitaji majibu ya haraka hususan kwa upande wa Serikali ni kuwa bado kuna tatizo la ukosefu wa hati miliki kwa majengo mengi au karibu yote ya skuli za Serikali. Skuli hizo nyingi zao zinamiliki ramani tu za majengo hayo lakini hazina hati za umiliki wa hati hizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili linaendelea kuzusha migogoro mingi na kesi nyingi za kuvamiwa maeneo ya skuli hizo zimeripotiwa Mahkamani, hivyo tuomba Serikali itoe muongozo kuhusu utaratibu wa upatikanaji wa hati miliki za majengo ya skuli ili kuepusha migogoro zaidi isitokee, ni mategemeo yetu kuwa Serikali itawajibika katika kutoa muongozo huo haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kama mnavyokumbuka leo ilikuwa ni siku ndefu sana kwetu na kwa kweli tunahitaji muda wa kuweza kwenda kusoma hotuba hii ili kesho tuweze kuichangia vizuri. Kwa sababu hiyo naomba tuahirishe mpaka kesho siku ya Ijumaa saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 15/07/2011 saa 3:00 asubuhi)